Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Tano – Tarehe 27 Aprili, 2009**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

***D U A***

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, natumaini mmekuwa na mapumziko mema ya *weekend* hii. Kutokana na kifo cha mwenzetu Phares Kabuye, ambaye alikuwa Mbunge wa Bunge hili la Tisa na ambaye sijatangaza kwamba kiti cha Biharamulo Magharibi kuwa wazi, bado tunastahili kumuenzi.

Kwa hiyo, nawaombeni tusimame kwa dakika moja kwa kumbukumbu yake.

(*Hapa Waheshimiwa Wabunge walisimama kwa dakika moja kuomboleza kifo cha Marehemu Phares Kashemeza Kabuye)*

**SPIKA:** Ahsanteni sana. Basi tunamwomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu Phares Kabuye, mahali pema peponi.

Waheshimiwa Wabunge, labda tu nitoe taarifa kwamba jana tuliwawakilisheni wengi wenu kwa kuwapo pale Morogoro Manispaa kuuaga mwili wa mwenzetu, nilikuwapo pale pamoja na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Naibu Kiongozi wa Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge kiasi cha 20 au 25 hivi. Nawashukuruni sana nyote. Katibu kwa shughuli za leo.

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:-**

Taarifa ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 (*The Annual General Report of*

*the Controller and Auditor General on the Financial Statement of the Local Government Authorities for the Financial Year 2007/2008).*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):-**

Taarifa ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu kwa Mwaka wa Fedha ulioshia tarehe 30 Juni, 2008 ( *The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of the Financial Statements of the Central Government for the Financial Year ended 30th June, 2008).*

Taarifa ya Mwaka wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu zilizokaguliwa za Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 (*The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of Public Authorities and Other Bodies for the Financial Year 2007/2008).*

Taarifa ya Mwaka ya Tathmini ya Utendaji wa Mamlaka ya Udhibiti ya Ununuzi wa Umma kwa Mwaka wa fedha 2007/2008 (*The Annual Performance Evaluation Report of the Public Procurement Regulatory Authority for the Financial Year 2007/2008).*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 53

### Fedha za Ujenzi wa Ofisi ya Wabunge

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA** aliuliza:-

Kwa kuwa, wakati wa Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge Serikali ilitoa taarifa juu ya fedha za ujenzi wa Ofisi za Wabunge Tanzania Bara na Tanzania Visiwani; na kwamba zilishatengwa shilingi bilioni moja kwa awamu ya kwanza ya ujenzi huo; na kwa kuwa, ilitolewa kauli kuwa, fedha za Bajeti ya 2008/2009 kiasi cha milioni 25 kitaongezewa pia kwa wale waliokwishakupewa mwaka uliopita wakati maeneo mengine hayajapewa kabisa:-

(a) Je, Serikali haioni ni vizuri kwa kila mwaka wa fedha maeneo ambayo hayajapata fedha hizo ndiyo yapate mgao huo?

(b) Je, kwa mfumo huo Serikali inaleta picha gani kwa jamii?

(c) Je, ni watu gani waliobuni utaratibu huo wa utoaji wa fedha?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka, lenye (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kila Mbunge anakuwa na Ofisi ndani ya Jimbo lake ili kumwezesha kuwa karibu na wananchi anaowahudumia.

Katika kutekeleza azma hii kwa kuzingatia idadi ya Majimbo kwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar Serikali imeweka vigezo vinavyotoa vipaumbele kwa utekelezaji wa mpango huu kwa awamu.

Kati ya vigezo hivyo ni pamoja na kuanza ujenzi katika Halmashauri zenye zaidi ya Jimbo moja la Uchaguzi, Majimbo yaliyoko pembezoni na Jimbo ambalo hakuna kabisa ofisi ya Mbunge.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa Bajeti ujenzi wa Ofisi hizo umeanza kutekelezwa kwa awamu. Katika awamu ya kwanza Serikali imeanza ujenzi kwenye Majimbo arobaini (40) ambapo ilipangwa kujenga ofisi 32 Tanzania Bara na Ofisi nane (8) Tanzania Zanzibar.

(b )Mheshimiwa Spika, azma ya Serikali kujenga ofisi za Wabunge ina lengo la kuonyesha jamii kuwa Serikali inawajali hivyo kuwasogezea mahali maalum wanapoweza kuwasilisha kwa karibu na wawakilishi wao na kupata utatuzi wa malalmiko yao. Katika kutekeleza programu ya ujenzi wa ofisi za Wabunge jumla ya shilingi bilioni moja zilitengwa kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha (2008/2009) programu ya ujenzi wa Ofisi za Wabunge Majimboni, imetengewa tena kiasi cha shilingi bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi hizo. Hata hivyo, baada ya ofisi yangu kupitia upya gharama za ujenzi imeonekana kwamba mahitaji halisi ya kukamilisha ofisi moja ni shilingi milioni 40.

Kwa mantiki hii kiasi cha fedha kilichotolewa mwaka 2007/2008 kingetosha kujenga ofisi 25 tu. Serikali iliona ni busara kukamilisha ujenzi wa ofisi zilizokwishaanza kwa kuziongezea shilingi milioni 15 siyo shilingi milioni 25 kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kufikia gharama halisi ya shilingi milioni 40.

(c) Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu Sera na Ofisi ya Bunge ilipendekeza Majimbo arobaini (40) ambayo yatapata mgao wa fedha za awamu ya kwanza ya ujenzi wa Ofisi za Wabunge.

Vigezo vilitumika kuchagua Wilaya ambazo Majimbo yao yatapata fedha kwa awamu, vigezo hivyo kwa ujumla ni kama ifuatavyo;-

(i)Uwiano wa Majimbo kati ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

(ii)Wilaya zenye Jimbo la Uchaguzi moja, Wabunge wamepewa Ofisi katika ofisi za Wakuu wa Wilaya na Halmashauri. *(Makofi)*

(iii)Wilaya zenye Majimbo ya uchaguzi mawili na Halmashauri mbili, Wabunge wamepewa ofisi katika Ofisi za Wakuu wa Wilaya, lakini hata hivyo wamepewa kipaumbele.

(iv)Wilaya mpya ambazo majengo mapya ya ofisi za Wakuu wa Wilaya zinajengwa, ofisi za Wabunge zimetengwa kabisa katika ofisi hizo katika ujenzi wake.

(v)Wabunge wa Viti Maalum kwa kawaida wanahudumiwa Mkoa mzima, kwa hiyo hutengewa ofisi katika Makao Makuu ya Mikoa.

(vi)Mikoa ya pembezoni na maskini zaidi kiuwezo wake hizo zimepewa kipaumbele cha kwanza.

(vii)Wilaya zenye Jimbo zaidi ya mawili katika Halmashauri moja nao wapewe kipaumbele. Kwa hiyo, lengo kuu ni huduma zote ziwe katika ofisi moja.

Mheshimiwa Spika, ofisi hizi zitazidi kujengwa kwa awamu hadi hapo zitakapomalizika.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, hali ya uchumi hivi sasa ni ngumu; na kwa kuwa Majimbo tunayo mengi sana na yote yanahitaji huduma na inawezekana mahali yalipofikia huko mbele ya safari tunaweza wenyewe kuyamalizia. *(Makofi)*

Je, Waziri haioni kwamba badala ya kuongeza fedha hizi kwa wale ambao wamejengewa wapatiwe wale ambao hawajajengewa kabisa?

La pili, kwa kuwa, fedha hizi baadhi ya sehemu toka zilivyotolewa kwenye baadhi ya Majimbo hazijafanyiwa kazi zilizokusudiwa. Je, Serikali inajua sababu za msingi hadi leo hii, kutokujengwa baadhi ya sehemu ya ofisi hizo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, Serikali iliona si busara kuanzisha jengo halafu ikaliacha ikarukia kuanza jengo lingine. Kwa hiyo, tuliona ni busara tukamaliza kwanza hizo ofisi tulizozianzisha, Ofisi 40 ili tuelewe kabisa kwamba Ofisi 40 za Wabunge zimekamilika ndipo tuanze ofisi nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa anaweza akaja ofisini nikamwonyesha maendeleo na hatua mbalimbali za ofisi za

Wabunge hatua zilizofikia. Ofisi zote mchakato wake umekwishaanza na vitu mbalimbali vilivyocheleweshа ni pamoja na kutafuta eneo husika kulikuwa na mvutano kidogo ofisi kwamba zitajengwa wapi.

Kwa hiyo, hiyo ni sababu mojawapo ambayo imecheleweshа. Lakini sababu nyingine ni pamoja na utafutaji wa viwanja katika baadhi ya sehemu kwa mfano, kule Pemba walikuwa na tatizo la mgogoro wa viwanja. Kwa hiyo, mpaka sasa hivi ofisi zote zimekwishaanza mchakato na zipo katika hatua mbalimbali na zimetembelewa, na hivi sasa tunawapa hela zile zilizobaki milioni 15 kulingana na ile *progress report*. (*Makofi*)

**SPIKA:** Maswali mafupi kabisa ya Kibunge ya nyongeza Mheshimiwa Haroub Masoud halafu Mheshimiwa Aloyce Kimaro.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, baada ya majibu ya mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wangu mimi kwanza naipongeza sana sana Serikali kwa kunipatia fedha za awamu ya kwanza; na kwa kuwa ofisi yangu ilikwishafikia hatua kubwa sana, ninachomuuliza Mheshimiwa Waziri, je, upo tayari kuja kuweka jiwe la msingi na pia kuniletea hundi kwa ajili ya kumalizia?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nimpe tu taarifa Mheshimiwa Haroub Masoud kwamba wafanyakazi wa ofisi yangu tayari wamekwisha tembelea ofisi zote zilizopo Pemba na Unguja na ripoti tunazo na hundi zimekwishaandaliwa kwa ajili ya fedha za awamu ya pili. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri unakwepa anakutaka uende huko! (*Kicheko*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu kwenda kuweka jiwe la msingi hiyo tutajiandaa mimi na Naibu Waziri wangu tuone ni nani ambaye anaweza akaenda huko. *(Kicheko)*

**WABUNGE:** Anakutaka wewe!

**SPIKA:** Kwa Mheshimiwa Haroub Masoud ningependekeza aende Naibu Waziri tu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikubaliane naye. (*Kicheko*)

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kujenga ofisi na ofisi ni pamoja na kuwepo kwa wafanyakazi na vifaa. Ningependa kumwuliza Waziri ofisi hizo zitakuwa na wafanyakazi wangapi na wataalum gani na vifaa gani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, fedha za ofisi hizo kati ya hizo fedha shilingi milioni 40 ni pamoja na samani ambazo zitawekwa katika ofisi hizo. Kuhusu wafanyakazi wangapi kama tunavyotambua Waheshimiwa Wabunge tuna wasaidizi Majimboni, wale wasaidizi wetu ndiyo watakaokaa katika ofisi hizo ili kupokea malalamiko mbalimbali ya wananchi. (*Makofi*)

Na. 54

**Kujenga Makumbusho ya Pamoja ya Waasisi**

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD** aliuliza:-

Kwa kuwa, nchi hii ina Waasisi wakubwa yaani Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Hayati Sheikh Abeid Aman Karume:-

Je, Serikali haioni kuwa, hivi sasa iko haja ya kujenga Makumbusho ya pamoja ya Viongozi hao, moja iwe Tanzania Bara na ya pili iwe Tanzania Zanzibar?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENT YA UTUMISHI WA UMMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mbunge wa Jang'ombe, ambalo limekaa mwaka mmoja lakini limefika katika Ofisi yangu kama wiki mbili zilizopita. Kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinatambua mchango mkubwa wa Waasisi wa Taifa letu, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume.

Michango yao kwa Taifa hili inajionyesha katika nyanja mbalimbali za kiuchumi, Kisiasa na kijamii. Kwa kutambua mchango wao, Serikali imekuwa ikifanya juhudi mbalimbali ili kuhakikisha kuwa urithi tulioachiwa na Waasisi wetu hawa unadumishwa.

Kwa umuhimu huo Bunge lako Tukufu lilipitisha sheria ya kuwaenzi Waasisi wa Taifa letu Sheria Na. 18 ya mwaka 2004. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kujenga Makumbusho ya kumuenzi Hayati Sheikh Abeid Amani Karume.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mbunge wa Jang'ombe, kama ifuatavyo:-

Sheria Na. 18 ya mwaka 2004 kifungu cha 4(1) kinatamka kuanzishwa kwa kituo cha pamoja cha Waasisi wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Hayati Sheikh Abeid Amani Karume.

Pia kifungu hicho hicho cha 4(2) kinatoa mamlaka ya kuanzisha vituo vingine mahali popote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa madhumuni ya kuhifadhi urithi waliotuachia waasisi wetu.

Mheshimiwa Spika, katika kuzingatia matakwa ya Sheria ofisi yangu imeanza kutekeleza mambo mbalimbali yaliyoelekezwa katika sheria ya kuwaenzi Waasisi wa Taifa letu kama ifuatavyo:-

- Kutafuta eneo kwa ajili ya kujenga kituo cha Waasisi wa Taifa letu ambacho pamoja na mambo mengine kitakuwa na Maktaba na Makumbusho.

- Kutafuta majengo la kupangishwa ili kuanzishwa ofisi za muda za kituo cha kuwaenzi Waasisi wa Taifa letu, ili kazi za kuratibu utekelezaji wake ziendelee kwa kasi.

- Pia kutafuta mtaalam mshauri atakayeishauri Serikali namna ya kuanzisha kituo na atandaa mpango wa utekelezaji.

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwanza kwa kujivua kwamba kwake imefika wiki mbili, lakini Bungeni liko mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, lengo la swali hili ni kuweka makumbusho ya pamoja, vijana wengi walioko Bara wanajua historia zaidi ya Mwalimu Nyerere, walioko Zanzibar wanajua zaidi historia ya Mzee Karume. Kuna mpango gani wa kuweko Makumbusho ya pamoja hilo ndiyo lengo kubwa zaidi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyomweleza kwamba mpango tuliokuwa nao sasa hivi tunatafuta kiwanja na tayari sasa hivi tumeshatafuta jengo ambalo tutalipanga kwa ajili ya kuanzisha Makumbusho ya pamoja.

Tumeshamtafuta mshauri mwelekezi ambaye ataanza kazi mwezi Mei, 2009 ili atuelekeze na awe anatuongoza katika kuanzisha Makumbusho ya pamoja.

Kwa hiyo, hayo yote niliyoyaeleza ni mkakati wa kuwa na Makumbusho ya pamoja.

Na. 55

**Utekelezaji wa Miradi ya TASAF**

**MHE. ERNEST G. MABINA** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwepo na utata juu ya utekelezaji wa miradi ya *TASAF* katika Wilaya ya Geita ambapo kijiji cha Kikubilo kilikuwa na mradi wa zahanati na Kijiji cha Nyabalasama kiliibua mradi wa barabara, lakini mradi mmoja tu wa zahanati ndiyo uliopata fedha; na kwa kuwa majibu yaliyotolewa na mratibu wa *TASAF* ni kwamba vijiji vyote vichangie kwa sababu zahanati ni muhimu kwa jamii:-

Je, ni kwa nini *TASAF* inatekeleza mawazo ya kijiji kingine na kuwakilisha kijiji cha jirani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ernest Gakeya Mabina, Mbunge wa Geita, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, taratibu za *TASAF* hazilazimishi jamii za jirani na jamii lengwa kuchangia katika utekelezaji wa mradi wowote. Ni jamii husika tu ndiyo inayolazimika kuchangia kulingana na mkataba unaoingiwa kati ya Halmashauri husika kwa niaba ya *TASAF* na jamii husika. Jamii za jirani huhamasishwa kuchangia miradi hii endapo miradi husika itanufaisha zaidi ya kijiji kimoja au jamii zaidi ya moja. Kwa mfano ujenzi wa shule ya sekondari na zahanati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa ujenzi wa barabara uliobuniwa na kijiji cha Nyabalasama bado Ofisi ya *TASAF* Makao Makuu haijapokea ombi hilo kwa kuwa mchakato wa kuweza kupata mchango wa Halmashauri haukuendelezwa kutokana na Halmashauri husika kuishiwa fedha zilizotengwa kama mgao wake. *(Makofi)*

Aidha, Kijiji cha Nyabalasama kilijulishwa kuhusiana na ukosefu huo wa fedha za mgao wa Halmashauri na hivyo kushindwa kuchangia mradi huo katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa miradi ya *TASAF* inatekelezwa kwa ubia kati yake na Halmashauri kwa niaba ya jamii husika, Halmashauri ya Wilaya ya Geita ndiyo ilitakiwa kuchangia utekelezaji wa maombi ya vijiji vyote viwili kupitia mgao wake. Aidha, miradi ilioombwa ni ya gharama kubwa, hivyo haikuwa rahisi kwa Halmashauri ya Wilaya ya Geita kuweza kutekeleza miradi yote miwili kwa wakati mmoja. Wanakijiji cha Nyabalasama wanaombwa kuvuta subira iwapo *TASAF* awamu ya pili itapata fedha za ziada za kukamilisha maombi kama hayo ambayo pia hutoka kwa wananchi wa Halmashauri nyingine.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa, wanakijiji wa Nyabalasama walihamasishwa na kuweza kuchangia ile asilimia 20 na sasa hivi wameshakusanya mawe katika eneo husika la barabara. Je, Serikali kwa kuwaonea huruma inasemaje katika suala hili au watoe katika mfuko wa Serikali Kuu?

La pili, kwa kuwa, hata hii hospitali au zahanati ya Kakubilo ambayo imepitishwa na mpango wa *TASAF* bado haijaanza kujengwa na wala hatujui fedha hizi zitakuja lini. Je, Serikali inasemaje kuhusu ujenzi wa zahanati hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza kwamba wananchi walikwishachangia asilimia 20 na huo mradi haukupata fedha Serikali inasemaje? Nimesema kwamba wawe na subira kama *TASAF* awamu ya pili itakapata fedha za ziada, basi na wenyewe watafikiriwa. Lakini pia niiombe Halmashauri iangalie kama kuna uwezekano wa kutoka katika vyanzo vyake vingine kuweza kuupatia huo mradi husika.

Kuhusu suala la ujenzi wa zahanati ni kweli fedha sijapelekwa, lakini Makao Makuu *TASAF* imekwishapokea na sasa hivi ipo katika mchakato wa kuwapatia hizo fedha. Kwa hiyo, hizo fedha watazipata kwa sababu maombi yao yalikwishafika *TASAF* Makao Makuu.

**SPIKA:** Swali la mwisho fupi la nyongeza Mheshimiwa Esther Nyawazwa.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja ndogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa vijiji hivi viwili katika Wilaya hii ya Geita hawakutendewa haki, kijiji cha Kakubilo kiliomba zahanati, na kijiji cha Nyabasalama kiliomba barabara. Je, Serikali sasa haioni kuitendea haki Wilaya hii ya Geita angalau mradi mmoja utekelezwe ili Mbunge wa Jimbo hili naye aende vizuri mwaka 2010? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, nafahamu na yeye pia ni Mbunge wa huko, kwa hiyo, pia yakifanikiwa na yeye pia anakuwa amefanikiwa. Ni kama nilivyosema kwamba miradi hii yote miwili yote ina gharama kubwa ndiyo Halmashauri ilishindwa kuweza kuichangia miradi yote miwili kwa wakati mmoja.

Lakini pia fedha zao za mgao ambazo zilikuwa zinatolewa na *TASAF* Makao Mkuu zilikuwa zimekwisha. Kwa hiyo, Halmashauri ya Wilaya ya Geita ikaamua

kuupeleka mradi mmoja ambao ni wa zahanati, na ninaamini kabisa huu mradi wa zahanati utavinufaisha vijiji vyote viwili.

Kwa hiyo, naiomba Halmashauri wakati sasa *TASAF* Makao Makuu inashughulikia mradi wa *TASAF*, basi Halmashauri ya Wilaya ya Geita na yenyewe ione uwezekano wa kuupatia fedha mradi huo ili Waheshimiwa Wabunge wote wawili hao mwaka 2010 mambo yao yawe mazuri. (*Makofi/Kicheko)*

Na. 56

**Kesi Dhidi ya Serikali**

**MHE. PONSIANO D. NYAMI** aliuliza:-

Kwa kuwa, mara zote Serikali inaposhtaki wahalifu hasa wanaotokana na wizi au ufujaji wa mali ya umma au kutowajibika hushindwa Mahakamani na kwamba pale Serikali inaposhtakiwa mara zote hushindwa na walalamikaji:-

(a) Je, kuna tatizo gani hasa kati ya Mahakama na Serikali?

(b) Je, kwa nini kesi zilizofunguliwa na Serikali hukaa muda mrefu Mahakamani kuliko zile ambazo Serikali hushtakiwa?

(c) Je, kati ya mwaka 2000 hadi sasa ni kesi ngapi za Serikali zilipelekwa Mahakamani na zipi Serikali ilishinda, kushindwa zilifutwa au zinaendelea?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ponsiano Damiano Nyami, Mbunge wa Nkasi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, hakuna tatizo lolote kati ya Mahakama na Serikali. Maamuzi mbalimbali yanayofanywa na Mahakama katika Mashauri yanayoihusu Serikali daima yanazingatia Katiba, Sheria na Sera za Nchi.

(b) Kukaa muda mrefu au mfupi kwa kesi Mahakamani kunakotokana na sababu nyingi kama vile upatikanaji wa mashahidi, ugumu au urahisi wa upatikanaji wa vielelezo vinavyotakiwa Mahakamani, uchache wa Watumishi wa Mahakama, uhaba wa vitendea kazi na sababu za kisheria.

Mheshimiwa Spika, vigezo hivi havijali pande hizi zinazohusika katika kesi.

(c) Mheshimiwa Spika, zipo kesi za aina mbalimbali zinazofunguliwa na Serikali.

Kwa upande wa kesi za jinai, ni vigumu kupata takwimu kwa urahisi kuhusu kesi zilizofunguliwa, zilizofutwa na zinazoendelea Mahakamani kwa sababu kesi hizi zinaendeshwa na mamlaka mbalimbali.

Kwa mfano, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Uhamiaji, Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*, Polisi, TAKUKURU, *TANAPA* na kadhalika. Wizara yangu inatarajia kuandaa utaratibu wa kuziratibu kesi mbalimbali za jinai zinazoendeshwa na mamlaka zingine ili kuwa na takwimu zake. Lakini pia kujua yanayoendelea kuhusu kesi husika kwa kufuata mwongozo wa Sheria Mpya ya Uendeshaji na Usimamizi wa Mashtaka ya Jinai nchini.

Kwa upande wa kesi za Madai dhidi ya au yaliyofunguliwa na Serikali, kuanzia mwaka 2000 hadi sasa, mashauri yaliyofunguliwa Mahakamani ni 3,617, mashauri yaliyoamuliwa dhidi ya Serikali ni 1,314, mashauri ambayo Serikali imeshinda ni 736 na mashauri ambayo bado yanaendelea ni 1,567.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa majibu haya ambayo siyo mazuri sana wala siyo mabaya sana. Nina maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa katika ukaguzi wa mahesabu ya Serikali Kuu, Serikali za Mitaa pamoja na Mashirika ya Umma, imejionyesha waziwazi kwamba Serikali imekuwa ikipeleka kesi nyingi Mahakamani, lakini huwa inashindwa na mali ya umma hulazimishwa na Mahakama wapewe hao watu binafsi ambao wanashinda hizo kesi kwa hila.

Je, huku siyo kuihujumu Serikali na kuashiria wingu la rushwa kwa vile Serikali huwa haitoi rushwa bali watu binafsi ndiyo wanajitahidi kutoa rushwa ili Serikali ishindwe?

La pili, kwa kuwa Serikali inapoamua kumshtaki kama vile mtumishi wa umma au pengine hata taasisi yoyote ambayo imeitendea visivyo inakuwa na ushahidi ambao kwa kweli huwa unajitosheleza. Je, katika hali hii inakuwaje Serikali inashindwa na halafu inalazimishwa kwamba ni lazima iweze kulipa fidia ambayo inakuwa kubwa na hivyo kuwatia hasara wananchi walio wengi? (*Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza jibu lake ni kwamba tunavyofahamu sheria ilivyo hivi sasa hairuhusu mtu binafsi kukamata mali ya umma. Huwezi mtu hata kushinda kesi ukakamata mali ya Serikali, sheria inakataza. Vivyo hivyo hata mali ya Halmashauri za Wilaya, Manispaa sheria ndio inakataza mtu aweze kukamata mali ya Umma.

Lakini endapo mtu atashinda kesi yoyote Mahakamani kama ni haki yake kupata fidia kutoka Serikalini, Serikali ina wajibu wa kumlipa huyo mtu fedha zake huenda

ikawa ukienda Mahakamani kwa sababu kuna upande pia wa pili unaweza kujitahidi ili kuonyesha kwamba ule ushahidi ambao ulionao sio sahihi.

Sasa kama Mahakama itaona kwamba ule ushahidi ulio nao sio sahihi itampa upande wa pili haki na haki inapatikana Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninachosema ni kwamba lazima tuiheshimu Mahakama huo uamuzi waliotoa lazima uheshimiwe na Serikali pamoja na mtu mwingine yoyote ambaye anapewa haki. *(Makofi)*

Na. 57

**Uboreshaji wa Mahakama na Ofisi za Watumishi wa Mahakama**

**MHE. FELIX N. KIJIKO** aliuliza:-

Kwa kuwa, kumekuwa na msongamano wa mahabusu wanaosubiri kesi zao husikilizwa katika Mahakama nyingi nchini; na kwa kuwa, Mahakama pamoja na vyumba vya mahabusu vimekuwa ni finyu kulingana na idadi ya mahabusu wanaopelekwa huko na pia hakuna *strong cabinets* za kutosha kuhifadhia majalada, Ofisi haziridhishi na vyumba vya Mahakama ni vidogo:-

(a) Je, Serikali imejipanga vipi kufanya upanuzi wa Mahakama na Ofisi za Watumishi wa Mahakama ya Kisutu inayopokea watuhumiwa wengi?

(b) Je, Serikali haioni kuwa, kuboresha vyumba vya Mahakama hasa Mahakama ya Kisutu kutatoa nafasi nzuri ya kuwapo na uamuzi sahihi?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko, Mbunge wa Muhambwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Serikali inalifahamu tatizo la ufinyu wa jengo la Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu ukilinganisha na wingi wa kazi zilizopo. Serikali kwa kulitambua hilo, imeiweka Mahakama ya Kisutu katika Mpango wa Ukarabati na ununuzi wa samani mbalimbali katika Bajeti yake ya mwaka wa fedha 2009/2010.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inakubali kuwa uboreshaji wa vyumba vya Mahakama, vikiwemo vile vya Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, ni muhimu sana kwa ufanisi wa Mahakama na utoaji haki kwa ujumla. Serikali inafahamu kuwa Mahakama nyingi tulizonazo zilijengwa miaka mingi iliyopita na kwamba kwa mazingira ya sasa miundombinu yake inahitaji kukarabatiwa au kuundwa upya. Juhudi za kuiboresha miundombinu ya Mahakama zinaendelea ingawa kwa taratibu kutokana na ufinyu wa Bajeti inayotolewa kwa Mahakama kila mwaka. Hata hivyo Serikali kwa

kushirikiana na wadau wengine wa ndani na nje imenuia kuendeleza juhudi za kuboresha majengo ya Mahakama ili kuondoa upungufu uliopo sasa.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ambayo yametolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Lakini kwa hisani kubwa ambayo mimi niliona ni kwamba ningependa kuelewa kama tatizo liko kwenye Mahakama kubwa ya Kisutu. Kama tunavyojua kwamba ni Mahakama ambayo inapokea wahalifu wa kila aina. Je, anaweza akatueleza mikakati iliyopo kwa Mahakama zingine ambazo ziko mikoani na mawilayani kwa sababu ninahisi matatizo ya Mahakama huko yatakuwa ni matatizo makubwa zaidi ya Mahakama ya Kisutu?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**: Mheshimiwa Spika, programu ya kuboresha Mahakama iko kwa ajili ya nchi nzima, sio Mahakama ya Kisutu peke yake tu. Kwa hiyo, tunakwenda awamu kwa awamu, inawezekana kabisa baada ya miaka miwili, mitatu, minne, mitano ijayo Mahakama zote nchi nzima zikawa katika hali inayoridhisha.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali nilitaka kujua kwa kuwa hali ya utoaji haki nchini na hasa vijijini imeachwa kwa watu wasio wataalam wa sheria na hasa katika kesi za ardhi na nyingine nyingi ambazo zinaamuliwa na Mabaraza ya Kata yasiyokuwa na wataalam wa sheria na sababu kubwa ni ufinyu wa Bajeti katika Wizara hii.

Je, Serikali inasema nini maana hili janga ni kubwa mno huko vijijini juu ya kuiongezea Wizara hii Bajeti ili iweze kufanya kazi zake vizuri?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama anavyosema kesi nyingi za ardhi katika vijiji pamoja na Wilaya husikilizwa na Mabaraza ya Kata pamoja na Baraza la Wilaya la Ardhi. Mabaraza yote hayo yako chini ya Wizara ya Ardhi hayako chini ya Wizara ya Katiba na Sheria.

Lakini hivi sasa kuna mchakato ambao unaendelea ili kuangalia namna ya kuboresha utoaji haki katika maeneo hayo yote mawili Mahakama ya Ardhi pamoja na Vijiji.

Na. 58

**Zoezi la Kusajili Vizazi na Vifo**

**MHE. DAMAS P. NAKEI** aliuliza:-

Kwa kuwa, zoezi la usajili wa vizazi na vifo lina umuhimu mkubwa na taratibu zake ni kwamba linafanyika Makao Makuu ya Wilaya hususan Babati:-

Je, kwa nini Serikali isipeleke huduma hiyo karibu na wananchi, angalau kwenye hospitali au vituo vya afya au kwenye Kata ili kupunguza usumbufu mkubwa wa kufuata huduma hiyo Wilayani?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Eng. Pascal Damas Nakei, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kutambua umuhimu wa usajili wa vizazi na vifo kwa Taifa. Serikali kwa kutambua umuhimu huu, kupitia Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) inashirikiana na Hospitali na Vituo vya Afya kutoa huduma za usajili katika maeneo husika ikiwemo vijijini.

Hata hivyo, upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa unafanyika Wilayani kwa mujibu wa sheria. Serikali imekuwa ikifanya juhudi mbalimbali kupitia Wakala katika kuhakikisha kwamba zoezi la usajili wa vizazi na vifo na umuhimu wake kwao na kwa Serikali kwa ujumla linafahamika na wananchi. Kupitia juhudi hizi, Wakala umefanikiwa kufanya uhamasishaji na uelimishaji katika Wilaya kumi na sita (16) ambazo ni Magu, Temeke, Bagamoyo, Makete, Hai, Mtwara Vijijini, Siha, Hanang, Mpanda, Kigoma Vijijini, Kasulu, Kibondo, Ngara, Ukerewe, Tanga na Nachingwea.

Mheshimiwa Spika, Wakala pia umefanya uhamasishaji na uelimishaji kuhusu usajili wa vizazi na vifo katika Mkoa wa Arusha. Mafunzo haya yametolewa kwa Maafisa Tarafa na Watendaji wa Kata na Vijiji ili waweze kufanya shughuli za usajili wa vizazi na vifo.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika kuhakikisha kwamba huduma za usajili wa vizazi na vifo zinaboreshwa na kuwa karibu zaidi na wananchi imeifanyia marekebisho Sheria ya Uandikishaji wa Vizazi na Vifo kupitia Bunge lako Tukufu katika Mkutano wa Kumi na Nne. Katika sheria hii Msajili Mkuu wa Vizazi na Vifo amepewa uwezo wa kuteua Wasajili ambao watakuwa na mamlaka ya kusajili na kutoa vyeti.

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nifanye sahihisho moja katika jina langu. Jina langu ni Damas Paschal Nakei sio Paschal Damas Nakei. Swali la kwanza la nyongeza, kwa kuwa mpaka sasa hivi inaonyesha ni Wilaya 16 tu nchi nzima ambako Wakala ameweza kufika. Je, kwa kasi hii hawa Wakala watafika Babati lini na kwa nchi nzima.

Swali la pili, kwa kuwa sheria inataka utoaji wa vyeti hivi uweze kufanyika Makao Makuu ya Wilaya peke yake, lakini hii inaonyesha kabisa kwamba inamwingizia gharama kubwa mzazi kiasi kwamba lazima asafiri kwenda Wilayani na pale Wilayani lazima akae labda siku moja au mbili ndipo apate huduma hiyo, je, Serikali bado haifikirii kwamba kuna haja ya kupeleka huduma hii kwenye Makao Makuu ya Kata?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba hadi hivi sasa RITA imefanya uhamasishaji katika Wilaya 16 Tanzania Bara makusudi ni kuwa na uhamasishaji na uelimishaji wa Wilaya zote nchini. Kwa bahati mbaya ufinyu wa bajeti ndio unaofanya RITA ishindwe kusambaza huduma hii nchi nzima. *RITA* kama itawezeshwa inaweza kuelimisha na kuhamasisha Wilaya zote za nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni kweli kwamba hadi hivi sasa vyeti hupatikana tu Makao Makuu ya Wilaya. Lakini kama alivyosema kufuatia mabadiliko yaliyofanyika katika sheria hii kwenye Mkutano uliopita wa Bunge juhudi za RITA ni kuhakikisha kwamba huduma hiyo inasambaa mpaka vijijini. Katibu Kata na Mtendaji wa Kijiji aweze kuwa na uwezo wa kuandikisha vizazi na vifo na kutoa vyeti sehemu hizo huko Wilayani na kwenye Kata na Vijijini

Na. 59

**Matatizo ya Usafiri Katika Kituo cha Mkwajuni**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA (K.n.y. DR. GUIDO G. SIGONDA**) aliuliza:-

Kwa kuwa, matukio ya uhalifu hasa yale ya ujambazi kwenye Jimbo la Songwe yameongezeka zaidi kuliko ilivyo kuwa kwenye miaka ya nyuma; na kwa kuwa, hali hiyo imesababishwa na ukosefu wa vyombo vya usafiri kama gari, pikipiki au baiskeli kwenye kituo cha Polisi kilichoko Mkwajuni:-

(a) Je, ni lini Serikali itakipatia kituo hicho usafiri ili kiweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi?

(b) Je, askari walioko kwenye kituo hicho watafanyaje kazi zao inavyopaswa bila nyenzo za utendaji kama vyombo vya usafiri?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Guido Gorogolio Sigonda, Mbunge wa Songwe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali haina uwezo wa kuvipatia vitendea kazi vya kutosha vituo vyote vya Polisi hapa nchini kutokana na uwezo mdogo wa kiuchumi ukilinganisha na mahitaji halisi ya nchi. Hali hii inasababisha askari wetu kufanya kazi katika mazingira magumu sana na hili tumekuwa tunalisema mara kwa mara hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kwa kutambua umuhimu wa kuwa na gari katika kituo cha Kikwajuni, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya tayari amepeleka gari moja *Landrover* TDI Na. PT 0655 ili liweze kuhudumia wananchi wa eneo hilo.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Chunya ni kati ya Wilaya kongwe sana hapa nchini. Lakini kwa bahati mbaya ni Wilaya peke yake ambayo haina Makao Makuu ya Polisi ya Wilaya. Pamoja na uhaba wa Bajeti ya Serikali je ni lini Serikali itajenga Makao Makuu ya Polisi Wilayani Chunya ili kuwa na mahabusu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nitakuambia Mheshimiwa Mbunge kama unavyoelewa tatizo tulilonalo ni maeneo mengi wanadai na wanaomba na ni haki yao kwamba wawe na vituo vya Polisi na Makao Makuu ya Polisi kama ulivyotaja.

Lakini kama inavyofahamika Bajeti tuliyonayo kwa kweli ina matatizo, isipokuwa nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala lako nimelipokea na tutatazama jinsi tutakavyoweza kulifanyia kazi katika Bajeti hii inayokuja. Ingawaje siwezi nikaahidi sana lakini nilitaka nikuambie kwamba matatizo tuliyokuwa nayo ni makubwa na nakushukuru sana Mheshimiwa Mbunge.

Na. 60

**Kuongezeka kwa Matukio ya Ujambazi Kijiji cha Tandala**

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE** aliuliza:-

Kwa kuwa, matukio ya ujambazi yanaongezeka kwa kasi sana katika kijiji cha Tandala kilichopo Wilayani Makete na kwa kuwa wananchi wamejenga kituo cha Polisi kwa nguvu zao lakini kituo hicho hadi sasa hakina Polisi na hivyo kuwafanya wananchi waishi kwa mashaka wakati wote:-

Je, ni lini kituo hicho kitaanza kufanya kazi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Binilith Satano Mahenge, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na kumalizika kwa ujenzi wa kituo hicho kilichojengwa kwa nguvu za wananchi, ambao kwa niaba ya Waziri wangu

tunawashukuru sana wananchi wa Tandala na pia tunamshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa jitihada zake kuhakikisha kwamba kituo hicho kinajengeka watalaam wa ujenzi wa Jeshi la Polisi na wale wa Idara ya Ujenzi ya Halmashauri ya Wilaya Makete walikaguwa uimara wa jengo hilo na kubaini kuwa linahitaji kuimarishwa kabla halijaanza kutumia rasmi na jumla ya mahitaji ambayo yanahitajika mpaka liweze kuwa sawasawa ni takribani Tshs. 7,730,450.00.

Mheshimiwa Spika, pale maombi na Bajeti ya Wizara yangu yatakapokuwa yamepitishwa nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutatazama jinsi ya kukamilisha ujenzi wa kituo hicho na kupeleka askari ambao itawalazimu kuishi uraiani ingawa kwa mujibu wa kanuni kuu za Jeshi la Polisi *(PGO)* askari wote wanatakiwa kuishi kambini. Wizara yangu itaendelea na juhudi zake za kutafuta fedha za kujenga nyumba za kuishi askari ikiwemo kuwashirikisha wananchi na wadau wengine wa usalama wa Raia.

**MHE. DK. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa tarehe 3 Agosti, 2008 wakati Rais alipotembelea kijiji cha Tandala wananchi waliwakilisha kilio kikubwa cha ujambazi kutua katika kijiji hiki na Rais aliagiza wanaohusika wafuatilie kwa haraka iwezekanavyo, ni mwezi Aprili hakuna kilichofanyika. Waziri anasema kwamba Serikali imeshindwa kupata shilingi 7,000,000/= anataka kuwahakikishia wananchi kwamba Serikali yao wanayoipenda ya Awamu ya Nne Wizara imeshindwa kabisa kupata shilingi 7,000,000/= ili kutatua tatizo hili hasa ukizingatia kwamba wiki mbili baada ya Rais kuondoka majambazi mawili yaliuawa kwa hasira na wananchi pale Tandala?

Swali la pili wananchi wa Tandala pamoja na wafanyabiashara wako tayari kuchangia nguvu kazi pamoja na vifaa vya ujenzi. Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kwa busara na kwa hekima na kwa huruma ya hawa wananchi kutumia uzoefu unaotumika na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi wakati wa ufunguzi wa shule za Kata kupunguza baadhi ya vigezo ili watoto waweze kuanza shule na hivyo ikiwezekana atoe agizo hapa kituo kianze wakati shughuli zinaendelea kufanyika?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli na hatupingani na hilo agizo la Rais alipotembelea eneo hilo tunalikumbuka na tunalizingatia sana na hakuna pahali popote ambapo tumesema hilo halitatekelezwa isipokuwa tulichosema tu ni kwamba hapa katikati tumekuwa na ufinyu wa fedha ambazo zinaweza zikakamilisha ahadi hiyo. Nataka nimhakikishie na ndio maana katika jibu langu la msingi nimemwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba hilo kwa kweli litafanyika. Lakini kwa kuwa katika suala lake la pili Mheshimiwa Mbunge amesema kwamba wapo wananchi na wafanyabiashara ambao wako tayari kutoa hizo fedha kuweza kukamilisha hiyo azma ya jengo basi mimi nataka nitamke hapa kwamba Wizara yangu kwa kweli inakaribisha mchango huo na kwa maana hiyo nitamwomba RPC wa huko aweze kuonana na Mheshimiwa Mbunge wakati Bunge litakapokuwa limekwisha waweze kufanya maandalizi ambayo yanahitaji kwa mujibu wa fedha ambazo zitakuwa

zimepatikana na kama maandalizi yote yatakuwa yamekuwa tayari basi nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kituo hicho kitafunguliwa. Ahsante sana.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa vitendo hivi vya ujambazi vimeongezeka sana hasa katika Wilaya ya Mkoani na kuna matukio mengi sana ya ujambazi yaliyofanyika Chokocho, Michenzani na mpaka leo hakuna yoyote aliyekamatwa wakati wengine majambazi hao wanakuja kwa njia ya boti kutokea Tanga. Je, ni kwa nini Jeshi la Polisi linashindwa kufanya kazi hii ni kwa sababu ya ukosefu wa vifaa au pia kuna tatizo la utaalam?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mnyaa anajua kwamba suala la ujambazi ni agenda kubwa ambayo tuliyonayo katika Jeshi la Polisi. Tunapambana nalo na maeneo aliyoyataja ni sehemu kubwa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tatizo ambalo nimekuwa nalisema na nitaendelea kulisema hapa ni kwamba tumekuwa na uhaba wa vitendeakazi na hilo ni jambo ambalo halifichiki. Lakini kwa utaalamu na kwa uwezo Jeshi letu la Polisi liko sawasawa liko imara na wale ambao mlishuhudia baadhi ya *exercise* ambazo zilifanyika jana wakati tunaadhimisha miaka 45 ya Muungano mliona jinsi Jeshi la Polisi lilivyoweza kujiandaa barabara isipokuwa tatizo tulilokuwa nalo ni uhaba wa fedha nyenzo za kutuwezesha kufanya kazi zetu kikamilifu.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa wananchi wa jimbo la Longido wamejenga kituo cha Polisi kule Natron na kwa muda mrefu Wizara hii wanaipangia bajeti kila mwaka kuanzia mwaka 2005 mpaka bajeti hii iliyoishia juzi lakini hawatoi hizo fedha na jengo hilo linaanza sasa kupata nyufa. Je, Waziri atakubaliana nami kutoa fedha walizopangia kwenye bajeti hii iliyoisha ili jengo hilo likamilike na Polisi waingie kwa ajili ya kulinda mali za wananchi pamoja na raia walioko mpakani huko?

**NAIBU WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Spika, ni kweli na nadhani Mheshimiwa Laizer anafahamu kwamba Wizara yangu imekuwa inapenda inavyowezekana tuweze kuweka vituo vya Polisi pale pote nchini na ni wajibu tufanye hivyo.

Lakini tatizo bado liko pale pale ni tatizo ambalo linatukabili la bajeti. Kama mnavyofahamu Waheshimiwa Wabunge kwa kweli wakati mwingine bajeti inapokuwa imepita lakini ndani katikati ya kipindi kile cha utekelezaji wa Bajeti yanajitokeza mambo fulani fulani ambayo inakuwa ni operesheni maalum ambazo inabidi *resources* ambazo tulikuwa tumezipangia huku zitumike mahali pengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nichukue nafasi hii nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Laizer kwamba maombi yake na kilio chake cha kituo cha Polisi Longido tunacho na katika Bajeti hii inayokuja tutatazama jinsi gani tutaweza kuhakikisha kwamba hili linafanyika.

Na. 61

**Wanawake Kupatiwa Soko la Bidhaa Zao na Mikopo**

**MHE. ANNA MAULIDAH KOMU** aliuliza:-

Kwa kuwa, wakati wa Siku ya Wanawake mwaka jana kauli mbiu yao ilikuwa "Mwanamke na Kikapu" na kwamba wanawake wameitikia wito huo kwa kutengeneza vikapu kwa wingi:-

(a) Je, Serikali haioni haja ya kuwasaidia Wanawake hao kwa kuwatafutia soko nchi za nje?

(b) Je, Serikali iko tayari kuwasaidia Wanawake hao kupata elimu ya biashara na mikopo nafuu?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mbunge Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kaulimbiu ya Siku ya Wanawake Duniani mwaka 2007, ilikuwa ni "Wanawake na Mazingira" Tumia Vikapu vya Asili, Tunza Mazingira Yetuu" kaulimbiu hii, ilisisitiza umuhimu wa matumizi ya vikapu vya asili vilivyotengenezwa kwa mimea badala ya mifuko ya plastiki ili kuepuka athari za uchafuzi wa mazingira na kuhimiza matumizi ya vikapu ambavyo watengenezaji wake wengi ni wanawake ikiwa ni shughuli mojawapo ya kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ikishirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali la Fursa Sawa kwa Wote *(EOTF)* imekuwa ikiwawezesha wanawake wajasiriamali kushiriki katika Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa yanayofanyika kila mwaka jijini Dar es Salaam.

Pamoja na kutangaza biashara zao, wanawake hawa hupata pia fursa ya kuuza na kuunganishwa na masoko ya ndani na nje ya nchi. Hata hivyo changamoto kubwa inayojitokeza ni bidhaa nyingi kushindwa kufikia viwango na ubora unaohitajika. Hata wale wanaofikia viwango hushindwa kutosheleza soko linalopatikana.

Kutokana na idadi ndogo ya wanawake wanaopata fursa hii Wizara yangu ipo katika mchakato wa kuanzisha kituo cha biashara cha wanawake kwa lengo la kutangaza bidhaa zinazozalishwa na wanawake hapa Tanzania. Kituo hiki kitakuwa na vitengo vya kutafuta masoko, kuendesha mafunzo ya kuboresha bidhaa, pamoja na kutoa elimu ya ujasiriamali kwa wanawake.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu hutoa mafuzo kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii ikiwa ngazi mbalimbali za Halmashauri, ili nao waweze kuwajengea uwezo wanawake katika Halmashauri zao. Maafisa hawa hutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vikundi vya wanawake kabla ya mikopo kutolewa na wakati wa uhamasishaji wa kuunda au kujiunga na Vyama vya Kuweka Akiba na Kukopa (SACCOS). Wizara hutoa mafunzo kila mara tunapopata uwezo wa kifedha, kwa mfano mwaka 2007/08 tulitoa mafunzo kwa wanawake 230 na zaidi ya vikundi 500 vya wanawake wajasiriamali kupitia Halmashauri zao.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekuwa ikitafuta njia mbalimbali za kuwawezesha wanawake hasa wenye kipato kidogo kupata mikopo nafuu. Jitihada hizo ni pamoja na kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake *(WDF)* pamoja na Mifuko ya wadau wengine wanaotoa mikopo kwa wanawake katika jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuzipongeza Halmashauri pamoja na taasisi zinazochangia maendeleo ya wanawake kiuchumi.

Kwa njia ya kipekee natambua mchango mkubwa unaotolewa na Taasisi ya Wanawake na Maendeleo (WAMA) inayoongozwa na Mama Salma Kikwete mke wa Rais na Taasisi ya Mifuko wa Fursa Sawa kwa wote *(EOTF)* katika kuwawezesha wanawake kiuchumi.

**MHE. ANA MAULIDAH KOMU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ningeomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa katika jibu lake alilonipa ameniambia kwamba soko halikidhi haja kwa sababu ya viwango vidogo vya matengenezo ya vikapu hivyo.

Je, Serikali haioni haja ya sasa kufanya jitihada ya mchakato wa kuwawezesha hawa wanawake kutengeneza vikapu ambavyo vitakuwa vizuri vitakavyokidhi kwenye haja ya soko ili kutoa nafasi ya Serikali kupiga marufuku mifuko ya plastiki ambayo inaharibu mazingira?

Swali la pili, kwa kuwa wanawake wengi hao aliowasema kwamba wanapata fursa kutokana na fursa hizo zinazopatikana za wanawake kuwapa mikopo, kwa hivyo percent ya wanawake wanaopewa mikopo ni ndogo kuliko wanawake ambao wanahitaji hiyo mikopo.

Je, Serikali haioni haja sasa kuanzisha kwa makini kabisa ile Benki ya Wanawake ambayo imekuwa hadithi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba viwango vya vikapu ambavyo wanawake wanatengeneza sio vizuri sana. Wizara yangu kupitia Maafisa Maendeleo ya Jamii tumekuwa na mkakati maalum pamoja na kushirikiana na *SIDO*. Nafikiri mtu mwenye

dhamana kubwa kuhakikisha kwamba stadi za kutengeneza na kuzalisha kwa ajili ya kuboresha vipato vya wananchi ni *SIDO*. Sisi kama Wizara jukumu letu ni kuhakikisha kwamba hao akinamama wanaopata mafunzo ya kuweza kuweka vitabu vyao vizuri, mahesabu yao pamoja na kupanga mikakati.

Mheshimiwa Spika, lakini ningependa kusema kwamba Wizara yangu tuliona hilo tumeamua kwamba sasa tuanzishe kituo cha Biashara cha Kitaifa Dar es Salaam kwa ajili ya wanawake wa nchi hii. Katika kituo hicho tutakuwa tunatoa mafunzo ya ujasiriamali pamoja na mafunzo ya kuboresha vile vitu ambavyo wanawake wanazalisha pamoja na kuboresha ufungashaji wa bidhaa zinazozalishwa na wanawake ili ziweze kupata soko. Nafikiri tukifika hapo tukishaweka kituo basi tutahakikisha kwamba kwenye kila Kanda kunakuwa na kituo ambacho kitakusanya vile vitu ambavyo wanawake wanavipata wavilete Dar es Salaam kwa ajili ya kutafutiwa soko na kuboreshwa.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kweli kwamba mpaka sasa hivi ni asilimia kidogo sana ya akinamama wanaopata mikopo. Siwezi kusema kwamba Serikali ina uwezo wa kuweza kutoa mikopo kwa asilimia 100 kwa wanawake wote. Ndio sababu Halmashauri zetu zina jukumu la kutenga asilimia 10 ya mapato yao kwa ajili ya mikopo ya wanawake na vijana. Naomba Waheshimiwa Wabunge wafuatilie hilo hili tuweze tukaongezea nguvu kile kidogo ambacho Serikali inatoa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Benki, naomba kwa furaha kabisa niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara yangu imeshapata leseni ya kuanzisha Benki, kwa hiyo wakati wowote tutaizindua hio Benki na tunaomba ushirikiano wenu wa kuhamasisha wanawake na vikundi mbalimbali kununua hisa nashukuru.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa vile wanawake wa Mkoa wa Iringa ni maarufu sana katika utengenezaji wa Vikapu vya asili na ambavyo vinatumia miti na rangi yake pia ni za asili.

Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuwapa mafunzo na tukizingatia kwamba wale wakinamama wanaotengeneza hivi vikapu wengi wao ni akinamama wazee ambao hawawezi kwenda kwenye masoko na kuwa pia kuwa tayari kuja kuwatembelea kuona shughuli zao?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO**: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii kumpa pole Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o kwa sababu alimpoteza kijana wake. Sisi wote tunamwombea Mwenyezi Mungu aendelee kumpa faraja.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa pole naomba nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kuweza kuwaona wamama wa mkoa wa Iringa hususan akinamama wazee ambao wanajua wanajukumu la kuelewa kwamba vijana wadogo wameachwa nyuma na wako tayari. Tutaangalia uwezekano wa kuweza kuwasaidia hao wakinamama wazee

kuboresha bidhaa zao na kuwashirikisha katika maonyesho ya nanenane pamoja na maonyesho ya biashara ya kimataifa.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niongezee machache kwa majibu mazuri aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri hasa kufuatana na swali la mwisho la nyongeza la Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o. Naungana naye Mheshimiwa Naibu Waziri kumpa pole Mheshimiwa Mg'ong'o.

Kuhusu kutembelea vikundi vya kinamama. Nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mg'ong'o kwa sababu tayari mimi nimeshatembelea vikundi vya kinamama Njombe vinavyotengeneza juisi, nimeona na nawapongeza sana. nimetembelea kikundi kizuri kinachotengeneza vikapu vile vinavyojulikana kwa jina la viondo. Nawapongeza sana, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tunatembelea kila tunapopata nafasi na nimeshatembelea vikundi vitatu Mkoa wa Iringa. Kwa hiyo tutaendelea kufanya hivyo.

Mwisho kwenye swali la Mheshimiwa Maulida Komu ni kwamba Benki inamwomba atakapopata nafasi apite Mtaa ule wa Mkwepu, tayari kuna bango pale utafurahi. Benki ya Wanawake Tanzania, Benki pekee inayotoa huduma kwa wote.

Na. 62

**Miradi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto**

**MHE. MARIA I. HEWA** aliuliza:-

Kwa kuwa mara nyingi bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na watoto huwa ni ndogo sana ikilinganishwa na bajeti ya Wizara zingine.

Je, Wizara hiyo ilijikita katika miradi gani hasa katika matumizi ya mapato ya mwaka 2007/2008?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ibesh hewa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ni ndogo ikilinganishwa na mahitaji halisi ya Wizara kutokana na uwezo wa Serikali. Kwa kuzingatia udogo wa bajeti hiyo kwa mwaka wa fedha 2007/2008 Wizara yangu kwa upande wa miradi ilijikita kwatika vipaumbele vitatu ambavyo ni:-

Ukarabati wa majengo na miundombinu, ujenzi wa majengo, pamoja na ununuzi wa samani kwa ajili ya vyuo vya makao makuu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008 jumla ya vyuo 25 vya maendeleo ya wananchi vilipelekewa fedha za ukarabati wa majengo na miundombinu. Vyuo 10 katika ya hivyo vilipelekewa fedha kwa ajili ya ukarabati mdogo wa majengo, mifumo ya maji pamoja na umeme.Aidha vyuo 12 vilipelekewa fedha kwa ajili ya ukarabati mdogo wa majengo , mabweni , nyumba za watumishi , maktaba, bafu, maliwato, mabwalo, madarasa na kuweka mfumo wa umeme katika chuo kimoja. Wizara ilifanya pia ukarabati mkubwa wa majengo na miundombinu katika vyuo viwili vya maendeleo ya jamii ambapo mabweni, nyumba za watumishi na mfumo wa maji vilikarabatiwa na kukamilika katika mwaka huo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu pia ilitumia fedha za miradi kujenga makataba mbili katika vyuo vya Buhare na Rungembe na kukamilisha ujenzi wa ukumbi wa kusomea katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru. Aidha ujenzi wa ofisi ya Makao Makuu ya Wizara na makataba katika chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru viliendelea kujengwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ilifanya pia manunuzi ya samani kwa ajili ya madarasa, mabweni, mabwalo, na jiko kwa ajili ya chuo cha Maendeleo ya Jamii Misungwi na samani kwa ajili ya Ofisi zake za Makao Makuu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na udogo wa bajeti ya Wizara, napenda kushukuru kwa kuongezea fungu la miradi ya maendeleo kutoka tsh. 3,860,853,000 kwa mwaka wa fedha 2007/2008 hadi kufikia shilingi 6,845,477,000 kwa mwaka huu wa fedha. Ongezeko hili litasaidia sana katika kukamilisha miradi mbalimbali ambayo inakwamisha utendaji wa Wizara. Aidha, ni matumaini yangu kuwa tutaendelea kuongezewa bajeti hii kila mara hali ya uchumi wa nchi inaporuhusu ili Wizara yangu iweze kutoa matokeo yaliyokusudiwa kwa jamii.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika, napenda nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake aliyoyatoa ndani ya Bunge hili. Nina maswali mawili madogo ya nyogeza. Katika jibu lake la kwanza anasema kuna vyuo 25 ambavyo wametuma pesa kwa ajili ya kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo, lakini niseme basi kujua kwa sababu hakuvitaja vyuo hivi. Chuo cha Malya kimo ili tuweze kujua katika chuo hicho wamefanya nini wao wanyewe waweze kufuatilia kwa sababu ni chuo muhimu sana katika nchi hii.

La pili, Wizara hii Mheshimiwa Spika, huwa inanyimwa pesa na nadhani kwa sababu ya kuzungumzia kila mwaka ni vyuo. Lakini Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, swali linaulizwa miradi. Hivi miradi ya Wizara hii ni vyuo tu, niombe Naibu Waziri leo atufafanuliwe. Kama ni vyuo tu, tuweze kujua ndiyo maana labda tunapewa pesa kidogo katika Wizara hii.

Je, kuna miradi mingapi katika mwaka 2007/2008. Imefanya nini Wizara hii labda ndiyo maana inapewa fedha kidogo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ameuliza kama Chuo cha Malya kilikuwepo kwenye wakati huo na kilifanyiwa ukarabati mkubwa. Tuko tayari kwenda kutembelea chuo hicho ili tuweze kujua kwamba kwa mwaka huu wa fedha tutaendelea kuwasaidia kwa kiasi gani waweze kufikia, kiwango kinachotakiwa. Ni kweli kwamba Wizara yangu jukumu lake kubwa ni kuchochea maendeleo na kwenye kuchochea maendeleo fungu lake la fedha la miradi. Fedha ambazo sisi tunazipeleka kwenye kuchochea maendeleo zipo kwenye mfuko wa *WPF* pamoja na Benki tunayoanzisha sasa hivi.

Pili jukumu letu kubwa ni kutoa mafunzo na kwenye kutoa mafunzo kila idara ambayo iko kwenye Wizara yangu hususan Idara ya jinsia inawafungu lake la kusaidiana na Maafisa Maendeleo ya Jamii katika kutoa mafunzo katika Halmashauri zetu. Kila Wizara inajukumu lake na sisi jukumu letu tunaishia katika kuhakikisha kwamba tuna vyuo vya kutoa maafisa maendeleo ya jamii watakaokwenda kwenye Halmashauri na katika Kata zao na kwenda kuchochea maendeleo na kutoa mafunzo. La pili ambalo tunalo sisi ni kuendeleza na kuhakikisha kwamba wananchi wanapata mafunzo kwenye vyuo vya maendeleo ya jamii ili waweze kupata ustadi wa kuweza kujisaidia wao wenyewe katika kujiletea maendelo.

Mheshimiwa Spika, nafikiri katika mchepuo sasa fungu letu ndiyo hilo, pamoja na kuangalia kisera na kisheria haki za watoto, haki za wanawake na raia wote wa nchi hii kwa kupitia sera mbalimbali ambazo tunazitoa. Nashukuru.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekubali kwamba Wazira hii kila siku inapata Bajeti ndogo. Je, Mheshimiwa Waziri anashauri nini kifanyike ili Wizara hii ipate Bajeti ya kutosha kutekeleza majukumu yake?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nimshukuru yeye pamoja na Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, kwa kuona kwamba Wizara yangu inapata pesa kidogo sana. Wahenga walisema kwamba utajikuna pale ambapo mkono wako unafika na Serikali yetu inajikuna pale ambapo mkono wake unafika katika kupanga kile kidogo kilichopo kuweza kuwafikia wananchi kupitia Wizara ambazo zimepewa majukumu maalum.

Mimi ninaamin kabisa pale ambapo Serikali yetu itaweza kuwa na uwezo mkubwa kwa kufuatana kwa vipaumbele vya taifa hili, basi na Wizara yangu itapata kile ambacho Serikali inapenda kutupa.

Lakini naomba niseme kwamba pale ambapo tumejenga hoja maana yake nishukuru kwamba Serikali iliona ile hoja ndiyo sababu ikatuongezea zaidi ya shilingi bilioni 2.6. Kuhakikisha kwamba vyuo ambavyo ni jukumu letu vinakuwa kwenye hali ya kuweza kuwaweka wanafunzi vizuri na kuweza kuendelea vizuri. Tutaendelea kupiga

debe pamoja na Waheshimiwa Wabunge lakini Serikali itatusaidia kulingana na uwezo wake. Nashukuru.

Na. 63

**Barabara ya Shelui – Mtoa – Ndago**

**MHE. JUMA HASSAN KILLIMBAH** aliuliza:-

Kwa kuwa, barabara ya Shelui –Mtoa –Kisonga –Mtekente – Lusaga – Kimbiji – Urughu na Kibaya –Ndago lilishaidhinishwa na kupitishwa katika vikao vyote vya barabara kikiwemo kikao cha Bodi ya Barabara Mkoa *(TANROADS)* kuwa barabara ya Mkoa.

(a) Je, ni tatizo gani ambalo hadi sasa limezuia barabara hiyo isianze kuhudumiwa na *TANROADS* Mkoa wa Singida?

(b) Je, Serikali inatambua licha ya taratibu zote kupitishwa bado mwaka huu wa fedha barabara hiyo imefanyiwa matengenezo madogo na fedha za Mkoa wa Barabara Wilaya badala ya *TANROADS* na ni kwa sababu gani imekuwa hivyo?

(c) Kwa kuwa, kuna eneo korofi kutoka Shelui hadi Kitongoji cha Kinkungu ambapo kuna udongo wa mfinyanzi ambapo wakati wa masika inakuwa vigumu kupitika.

Je, Serikali itakuwa tayari kuifanyia matengenezo sehemu hiyo korofi kwa kuweka kifusi imara ili wananchi wa vijiji husika watumie barabara hiyo wakati wote wa mwaka?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah, Mbnge wa Iramba Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Shelui – Mtoa –Ndago ni mojawapo ya barabara zilizopendekezwa na Bodi ya Barabara ya Mkoa Singida kupandishwa hadhi kutoka barabara ya Wilaya kuwa ya Mkoa. Katika mapendekezo ya Bodi ya Mkoa wa Singida, barabara hii imependekezwa isomeke kama Shelui Mtoa – Mtekete – Urughu – Kibaya yenye urefu wa kilometa 65.5.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekamisha uandaaji wa Kanuni zitakazotumika kupanga barabara kwenye madaraja husika. Sasa hivi Wizara ipo katika mchakato wa mwisho wa kuzipanga barabara katika madaraja kulingana na vigezo zilivyoainishwa katika Kanuni hizo ikiwemo barabara hii ya Shelui – Mtoa –Mtekente – Urughu – Kibaya.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa zoezi la kupanga barabara katika madaraja stahili halijakamilika, barabara hii ya Shelui –Mtoa – Ndago inaendelea kubaki katika hadhi yake ya barabara ya Wilaya na hivyo kusimamiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Iramba. Kuhusu eneo korofi katika barabara hii kutoka Shelui hadi kitongoji cha Kinkungu, kwa sasa ningeshauri Mheshimiwa Mbunge ashauriane na Halmashauri yake ya Wilaya ya Iramba kuona namna watakavyoweza kuipangia Bajeti kutokana na fedha za mfuko wa barabara kwa ajili ya matengenezo ya eneo hilo.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninapenda niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa, maombi ya barabara hii niliyoitaja kwenye swali la Msingi yalianza toka mwaka 2006 na kwa vipindi tofauti ndani ya Bunge hili Tukufu nimewahi kuuliza maswali yasiyopungua mawili na kutoa michango kwenye vipindi vyote vya Bajeti ya mwaka 2006/2007, 2007/2008 na 2008/2009 nikielezea namna ya kuhitaji barabara hii ipandishwe daraja. Lakini majibu yamekuwa ni mchakato, mchakato, wananchi wamechoshwa na majibu ya mchakato usioisha kila siku.

Je, ni lini sasa Waziri atamke hapa ili wananchi wasikie ni lini barabara hii itaisha na taratibu za mchakato utakamilika na lini barabara hii itapandishwa kuwa ya Mkoa.

Swali la pili, katika kipengele cha mwisho Mheshimiwa Naibu Waziri ananiambia kwamba niende nishauriane na Halmashauri ya Wilaya kuhusiana na kutengeneza eneo korofi kutoka Shelui – Kinkungu. Hivi nikashauriane nini kati ya hawa Halmashauri na mimi ndiyo tuliyokaa tukaona kwamba hatuna uwezo wa kuweza kuitengeneza hii barabara. Hivi tutashauriana katika fedha zipi?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, katika hili swali la kwanza juu ya mchakato wa kuzipanga barabara katika madaraja nimeeleza hapa kwamba kuna mahitaji ya kisheria.

Sheria yetu ya Barabara ya mwaka 2007 inahitaji kwanza kanuni kutungwa baada ya kanuni kutungwa Kamati ya Kitaalam iteuliwe na hatimaye kumshauri Waziri ili aweze akatangaza hizo barabara katika gazeti la Serikali. Mchakato tunaousema sasa hivi kama nilivyojibu kwenye swali la msingi kwa sasa kwa kweli umefikia mwisho kwa sababu vigezo vimeshaanishwa Kamati ilishachambua hizo barabara sasa kinachosubiriwa ni mchakato tu wa mwisho wa kuhakikisha kwamba sasa zinatangazwa.

Lakini pamoja na hiyo nataka niongeze kwamba katika kutekeleza hilo tumeonelea kwamba itakuwa ni vizuri kuleta hapa Bungeni maelezo ya vigezo vilivyotumika ambavyo vimeanishwa kwa Wabunge wote ili waweze wakavielewa ili hatimaye barabara hizi zinatangwa kila mmoja awe anajua kwamba ni vigezo vipi vilivyotumika.

Kwa hiyo, kama nilivyosema kwamba mchakato umefikiwa mwisho ni mwisho kweli kweli muda si mrefu niseme labda kabla ya Bunge la Bajeti tutakuwa tumeshaleta

maelezo hayo kwenye Bunge na baadae barabara hizo kutamkwa rasmi kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, la pili tumesema kwamba hizi fedha za barabara zinatengwa katika makundi mawili kuna fedha ambazo zinakuja kwenye Serikali kuu ambazo zinasimamiwa na *TANROAD* lakini kuna fedha ambazo zinakwenda kwenye Halmashauri za Wilaya kupitia TAMISEMI. Sasa tunao usemi unaosema kwamba kupanga ni kuchagua; ni kiasi cha kukaa kupanga kuona kwamba umuhimu uende katika jambo lipi.

Kwa hiyo, niliposema kwamba mashauriano ni suala la kwenda kupanga kwa fedha hizo ambazo walikuwa wamepewa kutokana na Mfuko wa Barabara.

Na. 64

**Kuboresha Uchimbaji Mdogo wa Madini Katika Eneo la Lilombe**

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika eneo la Kitowelo Wilayani Liwale kuna wachimbaji wadogo wadogo wa madini kati ya 300 – 500 kutoka mikoa mbalimbali nchi ambapo machimbo hayo yamedumu kwa zaidi ya miaka kumi na tano (15) sasa; na kwa kuwa, baadhi ya wafuatiliaji wa madini hufika wilayani hapo kutafiti madini katika vijiji vya Kibutuka, Ngumbu, Mpengele kutokana na kuwa Wilaya haina Afisa Madini.

(a) Je, Serikali ipo tayari kuleta Afisa Madini wa Wilaya hata kwa muda kwa maslahi ya wananchi na wachimbaji hao?

(b) Je, Serikali inaweza kueleza aina ya madini yanayopatikana au yanayoweza kupatikana katika machimbo hayo ya Kitowelo na sehemu nyingine za Wilaya ya Liwale?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini inazo Ofisi za Madini Kanda nane (8) na Ofisi za Afisa Madini Wakazi 14 ambazo husimamia shughuli za madini katika Mikoa ya Wilaya husika.

Kwa upande Mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma ikiwemo Wilaya ya Liwale, shughuli za madini katika Mikoa hii husimamiwa na Ofisi yaAfisa Madini Kanda ya Kusini iliyoko mjini Mtwara mbapo ofisi hiyo hutoa huduma mbalimbali za ugani kwa

wachimbaji wadogo. Maafisa Madini kutoka ofisi hiyo wamekuwa wakitoa huduma ya ugani kwa wachimbaji wadogo wa madini wa Wilaya ya Liwale takriban mara tatu kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kutoa huduma za ugani kwa wachimbaji wadogo wa madini nchi nzima kwa lengo la kuwaelimisha shughuli za utafutaji na uchimbaji wa madini wakiwemo wachimbaji wadogo wa Wilaya ya Liwale kwa mfumo huu uliopo sasa kama nilivyoueleza.

(b)Mheshimiwa Spika, miamba inayopatikana katika Wilaya ya Liwale ni *Proterozoic* pamoja na *Karoo*. Katika Wilaya ya Liwale madini yanayoambatana na miamba ya *Pretorozoic* ni vito ambayo hupatikana katika maeneo ya Kitowelo na Libufu, almasi na *base metals* hususan madini ya risasi(*lead*). Dhahabu Wilayani Liwale hupatikana katika maeneo ya Kitowelo na Mto Mbemkuru. Miamba aina ya *carbonatite* ambayo huambatana na madini ya *niobium*, pia hupatikana katika maeneo ya Kusini magharibi mwaka Wilaya ya Liwale. Vilevile kuna madini ya *blue marble* katika eneo la Kitogolo. Katika miamba *karoo* Wilayani Liwale, madini ya *uranium* yanafahamika kuwepo Lukuliro na Madaba.

Licha kuwa na miamba ya Karoo inayofahamika kuwa na makaa ya mawe hadi sasa madini yanayopatikana katika machimbo ya Kitowelo ni vito hususan *sapphire* pamoja na *alexandrite* na *crysoberyl*.

Mwisho Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2005 katika Ibara ya 39 (b) imetoa mwongozo thabiti kuhusu uwezeshaji wa wachimbaji wadogo. Aidha, Serikali kama tulivyosema kwenye maelezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yetu tumeshaanza matayarisho ya mfuko wa mae na Serikalini kwa ajili ya mfuko huo.

Hata hivyo kwa sababu ya ukata wa fedha, utekelezaji na uanzishaji wa mfuko huo umechelewa kidogo. Kwa hivi sasa mpango huu unafanyiwa kazi ili kulitumia Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)* kuwa ni sehemu ya utekelezaji na usimamizi wake. Ni imani yangu kwamba wachimbaji wadogo wa Liwale nao watafaidika na mfuko huu pindi ukianza kazi zake.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri katika jibu lake la msingi umetaja madini ambayo kweli ni ya thamani mno. Lakini kwa hali halisi kwa wastani wananchi wa Liwale bado hawajafaidika. Je, Serikali inaweza kutoa msukumo ulioimara zaidi ili wananchi hawa waweze kunufaika na madini hayo ambayo yanathamani katika Wilaya ya Liwale?

La pili, kwa kuwa ziara za Afisa Madini katika Wilaya ya Liwale kutoka Mtwara karibu kilomita 400 ni nadra na huenda baadhi ya ziara hizo hazipo.

Je, Waziri atakuwa tayari nikimwomba atembelee Wilaya ya Liwale ambapo kwa kusema kweli madini haya yangeweza kuleta changamoto kwa wananchi wa Liwale, aje

na baadhi ya wataalam wake kuweka msukumo mpya wa kuweza kuyahudumia madini haya kwa kushirikiana na wachimbaji wadogo wadogo ili na wananchi waweze kufaidika haraka iwezekanavyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kwenye madini ya vito ambayo yametajwa ambayo yapo Liwale yanajulikana kuwa yana thamani kubwa sana.

Lakini ni kweli pia kwamba *activity* ile ya uchimbaji mdogo pale Liwale; haujaendelea sana kama ulivyo uchimbaji wa madini kwenye Wilaya ya Tunduru au kama ilivyo kwenye maeneo ya Mahenge na Mererani na kadhalika.

Kwa hiyo, nakubaliana naye kwamba inabidi Serikali ifanye kazi na tutaifanyia kazi suala hili kuangalia ni changamoto gani ambazo tunaweza tukapeleka kwenye maeneo haya na pia kuipatia *exposure* zaidi Wilaya ya Liwale iondokane na huu uchimbaji mdogo mdogo na uchimbaji wa kati uweze kuingia kuweka msukumo.

Kuhusu suala la ziara kwa ajili ya kuweka msukumo wa pamoja na kuambatana na wataalam wa Kanda. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba nitafanya hivyo kwa heshima kubwa na ninatarajia kufanya ziara hiyo kwa muda ambao yeye mwenyewe atakuwa tayari.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa katika nchi yetu licha ya kuwa na Maofisa wa Kanda wa Madini, kwa miaka mingi sana kumekuwepo na vitendo vya baadhi ya wafanyabiashara na wachimbaji ambao wamekuwa wakitumia Leseni za Utafiti kuchimba madini na hivyo kusababisha Serikali kukosa mapato na uharibifu mkubwa sana wa mazingira. Lakini vile vile kumekuwa na vifo vya vijana wengi sana katika machimbo haya. *(Makofi)*

Je, hivi ni kwa nini Serikali inaacha vitendo hivi viendelee hasa baada ya kugundua kwamba makaripio yake na maonyo kwa watu hawa hayasikilizwi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nilivyomwelewa ni kwamba kuna wachimbaji wanaofanya utafiti baada ya kupewa leseni. Wanatumia leseni za utafiti kufanya uchimbaji wa madini na kwenye uchimbaji huo unafanywa kiholela na unasababishwa vifo vya vijana.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya uchimbaji kusema kweli ni mengi, ni makubwa na hata mwaka jana wakati wa Bajeti tulieleza nia ya kuboresha na kuwakabidhi vitendea kazi vikubwa zaidi Ofisi za Kanda za Madini na hasa pale ambapo *activity* ya madini ni kubwa zaidi ili kuwawezesha kufuatilia kwa karibu vitendo hivi ambavyo haviwiani na utoaji wa leseni.

Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hili lipo katika sehemu ya mipango ya kazi zetu na tunalifanyia kazi na tunapobaini kwamba tumempa leseni mtu ya utafiti lakini anachimbia madini tunamchukulia hatua za haraka ikiwa ni pamoja na kumnyang'anya leseni hiyo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umepita kidogo, lakini mtakumbuka tulianza na taarifa nyingi nyingi tu ambazo zimechukua muda mrefu.

Kwa hiyo, nitaongeza muda kidogo ili kuyajibu haya yaliyosalia. Swali kwa Wizara ya Nishati na Madini bado Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi.

Na. 65

**Wilaya ya Kilwa Kukosa Umeme**

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI** aliuliza:-

Kwa kuwa, inasemekana mradi wa umeme wa *Songas* umekamilika na kwamba baadhi ya maeneo kama vile Dar es Salaam wananufaika na huduma ya umeme huo.

Je, ni sababu zipi zinazoifanya Wilaya ya Kilwa ikose huduma hii kwa muda wa wiki mbili au zaidi na wakati mwingine kupata umeme wa mgao?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maamuzi ya kupeleka gesi Dar es Salaam kutoka kisiwani Songosongo Kilwa kwa ajili ya mradi wa kuzalisha umeme kwenye mitambo ya kufulia umeme ya kampuni ya *Songas*, yalitegemea vigezo vya kibiashara vya uwekezaji kwa muda unaokubalika na kigezo kingine kwa upande wa kitaifa kilikuwa ni uwezo wa mradi wa kuchangia kwenye uzalishaji wa ziada wa umeme nafuu katika gridi ya taifa.

Mheshimiwa Spika, mradi wa uendelezaji wa gesi asilia ya Songosongo una sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza ni usimikaji wa mitambo ya kusafisha gesi kisiwani Songo Songo, bomba la gesi na mitambo ya kufulia umeme ya Ubungo. Sehemu ya pili ni miradi ya kijamii ambayo ni uendelezaji wa miundombinu kwenye makazi ya Kinyerezi na Salasala pamoja na umeme la gesi kutoka Kilwa hadi Kusini mwa Dar es salaam.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kilwa kwa hivi sasa inategemea umeme unaozalishwa kwa majenereta ya mafuta. Ukosefu wa umeme, nyakati zingine mgao wa umeme miji ya Kilwa kunasababishwa na mtambo wa *perkins* ulio kwenye matengenezo na mashine ya *Wartsilla* ambayo vipuri vyake havijapatikana. *TANESCO* imetenga jumla

ya shilingi milioni 120 kwa ajili ya kazi hii inayoendelea ya matengenezo ya jenereta za kilwa. Mahitaji ya umeme ya Mji wa Kilwa ni Kw 700, ambapo uzalishaji wa umeme kwa sasa ni kW 385.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo suluhisho la kudumu la tatizo la umeme ambao unatarajia kumaliza kabisa tatizo hili, kwa Wilaya za Kilwa na Rufiji ni kukamilika kwa mradi wa kuzalisha umeme unaotokana na gesi asilia kwenye kituo cha Somanga Fungu, Mkoa wa Lindi. Mradi huu uko kwenye hatua za mwisho za ujenzi na ufungaji wa mitambo, ambayo inatarajiwa kuzalisha MW 6 kutoka kituo hicho.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Kilwa mradi unahusisha ujenzi wa laini mbili. Laini ya Msongo wa KV 33 kutoka Somanga Fungu mpaka Singino Kilwa ambapo pana kituo cha kupoozea umeme hadi *KV 11*. Kwa upande wa Rufiji, laini ya umemepitia Muhoro, Ikwiriri, Kibiti hadi Bungu. Nyamwange, laini itajigawa na kupeleka umeme Utete, ambayo ni Makao Makuu ya Wilaya ya Rifiji, katika Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutumia nafasi hii kuwashukuru waheshimiwa Wabunge wa maeneo haya husika na viongozi wengine wa Wilaya za Kilwa na Rufiji kwa ushirikiano wa karibu tulivyokuwa nao katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa mradi wa kituo cha umeme cha Somanga Fungu. Wizara inatarajia kuitisha Mkutano wa Wataalam mwanzoni mwa mwezi Mei ili kubaini ratiba ya utekelezaji ya kukamilika mradi huu. Tutawataarifu waheshimiwa Wabunge kuhusu ratiba ya utekelezaji.

**MHE. MWAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Spiika, asante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, katika bajeti ya mwaka 2007/2008, Bunge hili lilielezwa kuwa asilimia 90 ya Mradi huu umekamilika; na kwa kuwa bajeti ya mwaka 2008/2009, bado kituo hicho hakijakamilika; Mheshimiwa Spika, naomba kumwuliza swali Mheshimiwa Naibu Waziri. Je, Serikali inaweza ikatueleza kwa nini kituo hicho hakijakamilika hadi leo?

Mheshimiwa Spika, pia napenda kumuuliza, Je, kwa nini Serikali inamwogopa Mkandarasi ambaye hadi sasa anashindwa kumaliza kazi hii?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, wakati wa maelezo ya makadirio ya Wizara yangu mwaka 2007/2008, ukweli ni kwamba hadi wakati huokwa kiasi kikubwa utekelezaji wa kazi kwenye kituo cha Somanga – Fungu kilikuwa kimekamilika.

Mheshimiwa Spika, lakini tatizo tulilokuwa nalo wakati huo na ambalo lilisimama kwa muda mrefu, ni kwamba wakandarasi, siyo mmoja, wote walisimama kazi. Na walisimama kazi kwa sababu ya migogoro ya gharama za kazi zao. Kilichotokea ni kwamba, walikuwa wanadai hela ya ziada kwa sababu ni kweli kwamba vifaa vilipanda bei kwenye masoko huko na ulipaji wa pesa hizo ulikuwa unachukua muda kidogo kufanyia tathmini madai ya gharama hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni kweli kwamba kwa tatizo lililokuwepo, ni kwamba wakandarasi wale hawawezezi kufanya kazi kwa pamoja, ni lazima mjezni amalize, halafu mfungaji wa mitambo amalize, ahalafu mfungaji nyaya amalize, hawawezi kufanya kazi simuliteniously. Kwa hiyo, ni kweli kazi ilichelewa.

Lakini, mimi nilifanya ziara kwenye kituo hicho Desemba, 2008 na Waziri wa Nishati na Madini amekwenda huko mwezi wa Tatu. Kwahiyo, tunasimamia kwa karibu na tunatarajia kwamba mwezi ujao tunawaita wakandarasi wote, siyo mmoja, wote ili kubaini utekelezaji wa ratiba hiyo na kwamba tujue haswa nani anamcheleweshа mwenzie.

Mheshimiwa Spika, hili lingine la kwamba Serikali inamwogopa mkandarasi, Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM) haiwezi kumwogopa mkandarasi. Tunafanya kazi na wakichelewa tutachukua hatua zingine.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa nafasi hii niulize swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la umeme ni kubwa sana hapa nchini na hivi majuzi Mheshimiwa Naibu Waziri alitembelea Wilaya yetu ya Misungwi na kukuta wananchi wale. Je, kazi itaanza lini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tulikwenda huko Misungwi kufuatilia utekelezaji wa miradi. Umeme kwenye maeneo ya Seke – Misungwi unapelekwa kupitia mradi wa *MCC.*

*MCC* ilisainiwa mwezi wa kumi na moja na Mshauri Mwelekezi alikuwa analifanyia kazi hilo, anatarajia kumaliza kazi yake mweziwa tano, 2009 na baada ya hapo tunaanza shughuli za manunuzi kwa kadri Mshauri Mwelekezi atakavyoainisha.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba pia nitaarifu kuwa *Millenium Challenge Account* tayari umeishafanya makubwaliano na *Exim Bank* kusimamia hela hizo za miradi.

Kwa hiyo, kimsingi tulikuwa tumechelewa hapa kidogo kwa sababu ya utekelezaji wa taratibu tu za kawaida za utoaji wa fedha hizo. Lakini ninaamini kabisa kwamba tuko vizuri na kwamba kuanzia mwezi ujao, tutaanza kuona kuhangaika kidogo kwa wakandarasi kwenye maeneo yote hayo ambayo yanasubiri utekelezaji wa *MCC. (Makofi)*

Na. 66

**Matukio ya Uchomaji Moto Mabweni ya Shule**

**MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika siku za hivi karibuni yamekuwepo matukio mengi ya uchomaji moto mabweni ya shule zetu hapa nchini kwa mfano matukio matatu yaliyotokea katika shule ya Serikali Machame, Wilayani Hai:-

Je, ni hatua gani za kukomesha matukio haya zimechukuliwa?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Archt. Fuya Gowin Kimbita, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa siku za karibuni yamekuwepo matukio ya uchomaji moto mabweni ya baadhi ya shule za Sekondari hapa nchini ikiwemo shule ya Sekondari Machame iliyopo Wiliyani Hai. Aidha ni kweli pia kwamba majanga ya moto katika shule zetu hurudisha nyuma maendeleo ya elimu kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kila tukio la moto katika shule zetu, Serikali ilichukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanya uchunguzi wa kina kubaini vyanzo vya matukio hayo. Chunguzi hizi zimebaini kuwa matukio ya uchomaji moto mabweni yanasababishwa na migogoro ya kijamii inayohusisha jumuiya ya shule au wanafunzi wenyewe na hujuma. Wizara imekuwa ikiyafanyia kazi mapendekezo yanayotokana na taarifa za chunguzi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara imewaagiza Wakuu wa shule hizo na nyingine nchini kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kuhakikisha kuwa wanafunzi hawakai na vifaa/vitu vinavyoweza kuanzisha moto shuleni na kununua vifaa vya kuzimia moto.

Pia Bodi za shule zimeagizwa kufanya uchambuzi wa kina kuhusu matukio ya moto na kupendekeza mikakati ya kuzuia matukio hayo katika shule hizo. Aidha watu wote watakaothibitika kuhusika na matukio ya kuchoma moto majengo ya shule au mali za shule, watachukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa kuwa kikao cha Bodi ya shule ya Sekondari Machame kimeshakaa na wanafunzi waliohusika watahamishiwa kwenye shule za kutwa kwa ajili ya usalama wao na usalama wa wanafunzi wenzao.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri anatuambia kwamba uchunguzi huo unafanyika kutambua kwamba ni sababu zipi zinazopelekea kuwa na matukio ya moto katika shule mbali mbali nchini. Katika shule ya Shauritanga kule Rombo kulikuwa na tukio la mto na wachunguzi walikuja kutoka *Scortland Yard* kuja kufanya uchunguzi, lakini mpaka leo, matokeo ya uchunguzi ule hayajawekwa hadharani.

Je, Serikali haioni ni wakati muafaka sasa kuweka matokeo yale hadharani pengine itasaidia kupunguza mioto katika mashule yetu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli Shauritanga ni mojawapo ya shule ambazo zilipata janga la moto na kutekeleza wanafunzi wengi.

Hata hivyo, nikiri kwako Mheshimiwa Spika kwamba moto huo ulitokea miaka mingi iliyopita, taarifa yake sisi kama Wizara lazima tukaiombe na naomba alete swali hilo la msingi nitakwenda kutafuta kwa sababu ulikuwa ni uchunguzi uliofanywa na Serikali kwa kuwashirikisha Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Usalama wa Taifa na Vyombo vingine vya Dola.

Na. 67

**Kuboresha Chuo cha Ualimu cha Mtwara**

**MHE. JUMA A. NJWAYO (K.n.y. MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa uhaba wa walimu katika mikoa ya Kusini hasa Mtwara ni mkubwa sana na tatizo hilo linaendelea kuwa sugu.

Je, Serikali haioni kuwa, kuna haja ya kuchukua hatua ya makusudi kuboresha chuo cha ualimu cha Mtwara ili kitoe walimu kwa ajili ya Mikoa ya Kusini?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya, Mbunge wa Lulindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vyuo vya ualimu kwa ujumla wake ni vyuo vya kitaifa na hutoa mafunzo ya ualimu tarajali na walimu kazini. Walimu wanaohitumu mafunzo vyuoni wanatarajiwa kufanya kazi sehemu yoyote nchini, ikiwemo Mikoa ya Kusini. Serikali ina mikakati mbalimbali ya kupanua na kuboresha vyuo vya ualimu nchini kikiwemo chuo cha ualimu Mtwara. Mikakati hii imelenga kuongeza nafasi katika vyuo vya ualimu ngazi ya Cheti na Stashahda na hivyo kupata walimu wa kukidhi mahitaji katika shule za Msingi na sekondari, zikiwemo shule za Mikoa ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, ukarabati na upanuzi wa majengo katika vyuo vya ualimu ili kuongeza nafasi za mafunzo ya ualimu utaendana na upatikanaji wa fedha. Hata hivyo, Serikali itaendelea kushawishi sekta binafsi kuanzisha na kuendeleza vyuo vya ualimu nchini kote ikiwemo mikoa ya Kusini.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, swali la msingi hapa lilikuwa lina-*base* zaidi kwenye suala la

upungufu wa walimu kwa Mikoa ya Kusini. Mkoa wa Mtwara una matatizo makubwa sana ya upungufu ya walimu hasa kwa Wilaya ya Tandahimba na Nanyumbu ambazo ni za hivi karibuni. Je, nini hatua za Serikali kumaliza tatizo hili kwa haraka?

Kwa kuwa Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2005, katika Ibara ya 62(a) inaeleza wazi kwamba chuo hiki cha Mtwara kitakuwa chuo kiambata *(Associate College)*.

Je, mchakato huu umefikia wapi ili kwenda sambasamba na Ilani ya chama chetu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Spika, nimesema walimu wetu wanafunzi wanaopelekwa katika vyuo ni kwa ajili ya nchi nzima, hatuna walimu wanapomaliza chuo wanaofundisha eneo husika.

Kwa hiyo, wanafunzi wanaomaliza katika vyuo hata kama ni chuo kiko Arusha, walimu hao hupelekwa katika shule nchi nzima, ndio maana hatuangalii chuo kama ndiyo kinachozalisha walimu kwa ajili ya eneo husika.

Kwa hiyo, ndiyo maana nimesema ukarabati wa chuo cha Mtwara ni kama ukarabati katika vyuo vingine, lakini walimu wa kupelekwa Wilaya za Kusini watapatikana kutokana na vyuo vinavyofundisha wanachuo nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, chuo cha Mtwara kufanywa chuo kiambata, zoezi hili linasubiri kuhuisha sheria mbili; sheria ya elimu na mafunzo ya ufundi ya mwaka 1978 ambayo ndiyo iliyotumika kuanzisha vyuo vya walimu pamoja na sheria inayoruhusu kuanzisha vyuo vikuu. Kwa sababu kuwa chuo kiambata maana yake chuo hiki kitoe mafunzo kikisimamiwa na Wizara ya elimu na sheria iliyoanzisha Wizara ya elimu ya uanzishaji wa vyuo vya ualimu, lakini kitoe cheti ambacho ni cha Chuo Kikuu cha Dar es salaam. Kwa hiyo, hadi hizi sheria mbili zitakapokuwa zimewekwa sawa sawa ndipo chuo hiki kitakapoweza kuwa chuo kiambata.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umepita, maswali yamekwisha. Sasa ni matangazo:-

Mheshimiwa Wasira, nakuomba radhi sana karatasi yako siioni hapa; tunaomba mgeni wa Mheshimiwa Wasira, popote alipo asimame, ahsante na karibu sana. Tukiwa tunaendelea, kama nitaipata basi naweza kuwatambulisha kwa jina.

Waheshimiwa Wabunge, kuanzia leo nimeanzisha utaratibu ambapo nitapokea ushauri wa kisheria kwa karibu zaidi. Katibu wa Bunge amefanya mpango, eneo hili mnaloliona baada ya kizuio pande zote mbili, upande mmoja atakuwa ni Mwakilishi wa Mwandishi Mkuu wa Sheria *(CPD)*, sehemu anapopita Waziri Mkuu mara kwa mara pale; na upande mwingine atakuwepo Mshauri Mkuu wa Sheria wa Bunge au Wasaidizi wake; inapotokea Mbunge kuwa na shida kidogo, unapotaka uliweke jambo vizuri na

unahitaji usahihi kisheria, sasa badala ya kutangatanga na kuulizana humu kienyeji, basi watakuwepo wataalamu hao. Karibuni sana muitumie huduma hii; tutaiweka kwa majaribio, wakikaa siku mbili, tatu, hawaulizwi chochote, basi tutajua kwamba huduma hiyo haihitajiki. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimepata jina la mgeni wa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika; anaitwa Jonathan Kenemba Irobi ni Mwenyekiti wa CCM, Tawi la Kikoleli (B), Kata ya Nyamswa - Bunda; karibu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Dkt. Ali Tarab Ali naye ana mgeni wake, ambaye ni Ndugu Ali Mohamed Busiri, anatoka Idara ya Biochemistry ya Chuo Kikuu cha Sayansi ya Afya (*MUHAS*); karibu sana. *(Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, imetoa mwaliko kwa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, kuhudhuria maadhimisho ya afya na usalama sehemu za kazi, yatakayofanyika kitaifa katika Uwanja wa Jamhuri Dodoma, kesho tarehe 28 Aprili, 2009 kuanzia saa mbili asubuhi; hivyo basi, Wajumbe wote wa Kamati hiyo wamepewa ruhusa na watapewa usafiri kuelekea katika shughuli hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani hayo ndiyo matangazo ya leo, nawashukuru kwa uvumilivu wenu.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji wa Mwaka 2009
***(The Water Resources Management Bill, 2009)***

### Muswada wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2009
***(The Water Supply and Sanitation Bill, 2009)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa ufanisi katika mijadala ya Miswada hii miwili ambayo inashabihiana, nimeruhusu utaratibu ambapo mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, atawasilisha Muswada mmoja baada ya mwingine ili tusilazimike tena kuzungumzia masuala ya maji halafu Muswada mwingine usomwe labda kesho na kadhalika. Kwa maana hiyo, hata Mwenyekiti wa Kamati husika na Msemaji wa Kambi ya Upinzani wanaelewa hivyo. Kwa hiyo na wao watatoa maoni yao, kwa kuzingatia Miswada yote miwili. Baada ya hapo, tutachangia hadi kesho asubuhi halafu mtoa hoja atamalizia kabla ya saa saba mchana kesho kwa Miswada yote miwili, wakati huo huo nitawahoji kwa kila Muswada.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Rasilimali za Maji wa Mwaka 2009 *(The Water Resources Management Act, 2009),* kama ulivyopangwa katika shughuli za leo za Bunge,

pamoja na Jedwali la Marekebisho kama lilivyoambatanishwa, sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, lengo la sheria mpya ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji ni kulinda, kutunza, kutumia, kudhibiti na kuendeleza rasilimali za maji kwa maendeleo ya kiuchumi na ya kijamii bila kuathiri mazingira. Suala la kuwashirikisha wananchi katika usimamizi wa rasilimali za maji kuanzia ngazi ya chini hadi ya kitaifa, limezingatiwa kwa kutumia misingi ya dhana mpya ya usimamizi wa pamoja wa rasilimali za maji *(Integrated Water Resources Management).*

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii, kwa niaba ya Wananchi wa Rungwe Mashariki na Wilaya ya Rungwe kwa ujumla, kutoa salamu za pole na rambirambi kwako, kwa familia na Wananchi wa Busanda, kufuatia kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Busanda, Marehemu Faustine Kabuzi Rwilomba; rafiki mkubwa wa Wilaya ya Rungwe. Naomba Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, tumepokea hivi punde kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha mama yetu, Mama Adam Sapi Mkwawa. Natoa pole kwa familia yote ya Mkwawa, Mwenyezi Mungu airehemu roho ya marehemu, Amina.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii pia kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Maji na Mifugo, chini ya Uongozi wa Mwenyekiti wa Kamati hii, Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo, Mbunge wa Ileje, kwa kuuchambua na kuupitia Muswada huu kwa kina; mbali na muda wa kawaida. Wajumbe wametumia muda wa ziada, kwa siku tatu mfululizo, kuanzia Ijumaa iliyopita hadi Jumapili katika kuuchambua Muswada huu. Nawashukuru.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru wadau wote waliotoa michango yao ya kuboresha Muswada huu. Wadau hao ni pamoja na Wizara za Serikali, Asasi zisizo za Kiserikali, watumiaji wa maji wakiwemo wakulima wakubwa na wadogo, wafugaji, Vyuo Vikuu na Sekta Binafsi. Naishukuru pia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Idara ya Mwandishi Mkuu wa Sheria na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, kwa hatua zote za maandalizi na hatimaye kukamilisha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa usimamizi na udhibiti wa matumizi ya maji kwenye vyanzo mbalimbali nchini, unafanywa kwa mujibu wa Sheria ya Kusimamia na Kudhibiti Matumizi ya Maji *(Water Utilization Control and Regulation Act, 1974).* Ili kukabiliana na changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa zikijitokeza, sheria hiyo imefanyiwa marekebisho mara tatu kama ifuatavyo:-

(i) Rekebisho Namba 10 la Mwaka 1981, ambapo dhana ya usimamizi wa rasilimali za maji kwa mfumo wa mabonde ilianzishwa kisheria. Katika rekebisho hilo, viwango vya maji na udhibiti wa uchafuzi wa maji ulipewa nguvu za kisheria;

(ii) Rekebisho Namba 17 la Mwaka 1989, ambalo liliongeza viwango vya adhabu za ukiukwaji wa sheria;

(iii) Rekebisho Namba 8 la Mwaka 1997 lilihusu idadi ya Wajumbe wa Bodi za Mabonde.

Mheshimiwa Spika**,** kutokana na mabadiliko ya sera za kiuchumi na kijamii, kupitishwa kwa Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 na ongezeko kubwa la idadi ya watu na mahitaji ya maji kwa matumizi mbalimbali, mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira unaotokana na ongezo la shughuli za kibinadamu; Sheria iliyopo ya Rasilimali za Maji haikidhi mahitaji ya kusimamia rasilimali hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha maji kinategemea idadi ya watu. Nchi yetu ina maji ya baridi yanayofaa kwa matumizi ya binadamu kiasi cha kilometa za ujazo 89. Kiasi hiki kilikuwa sawa na mita za ujazo 2,700 kwa kila Mtanzania kwa mwaka 2001, ambapo idadi ya watu ilikuwa milioni 33. Mwaka 2008/2009, Tanzania inakadiriwa kuwa na watu milioni 40; hivyo, kufanya kiasi hicho kupungua hadi mita za ujazo 2,225. Ifikapo mwaka 2025, idadi ya watu inakadiriwa kufikia milioni 60, ambapo kiasi cha upatikanaji wa maji kitapungua kwa asilimia 45 na kufikia mita za ujazo 1,500. Wakati huo nchi yetu itakuwa miongoni mwa nchi zenye uhaba wa maji duniani. Nchi ambazo zina chini ya mita za ujazo 1,700 kwa mtu kwa mwaka, zinahesabiwa kuwa zina uhaba wa maji. Hata hivyo, juhudi za kutafuta maji chini ya ardhi huko Kimbiji, Dar es Salaam na maeneo mengine nchini, zitasaidia kubadilisha picha hii kwa nchi yetu. Utafiti bado unaendelea. Hata hivyo, kuna umuhimu mkubwa wa kutunza vyanzo vya maji, kusimamia ugawaji wa maji kwa matumizi mbalimbali, kuyatunza na kuyatumia kwa tija na ufanisi ili yaendelee kutupa uhai.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto za sasa na zile zinazoendelea kujitokeza, tunahitaji kuwa na sheria inayoangalia masuala yote badala ya kuifanyia marekebisho madogo madogo na mengi sheria iliyopo. Mtazamo huu utasaidia kuondoa upungufu uliopo katika Sheria ya Mwaka 1974. Upungufu huo ni pamoja na ufuatao:-

(1) Sheria haikuzingatia usimamizi wa pamoja wa rasilimali za maji *(Integrated Water Resources Management).* Hili lisingewezekana kwa sababu hii ni dhana mpya, yenye kutumia misingi ya Azimio la *Rio de Janeiro* la mwaka 1992, lililokamilisha Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mazingira na Maendeleo Endelevu. Misingi hiyo ni pamoja na:-

(a) Utunzaji wa mazingira na vyanzo vya maji *(The Ecological Principle);*

(b) Utawala Bora katika usimamizi wa rasilimali za maji *(The Institutional Principle);*

(c) Msingi wa jinsia *(The Gender Principle);* na

(d) Kutambua maji kama bidhaa ya kiuchumi *(The Economic or Instrument Principle).*

(2) Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mwaka 1974 ilijikita zaidi kwenye kusimamia na kudhibiti matumizi ya maji na haikuzingatia ipasavyo, uhifadhi wa vyanzo vya maji na utunzaji wa rasilimali za maji. Baada ya Serikali kupitisha Sheria ya Mazingira na Sheria Na.20 ya 2004 na Mkakati wa Kuhifadhi Ardhi na Vyanzo vya Maji, imebidi tuipitie upya sheria hii.

(3) Tanzania ina majishirikishi kuliko nchi yoyote katika Bara letu la Afrika kutokana na kuzungukwa na Maziwa Makuu. Mabonde sita kati ya mabonde yote tisa ni mabondeshirikishi. Mabonde hayo ni Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, Bonde la Ruvuma, Pangani na Bonde la Kati. Sheria haitambui ipasavyo kwamba, sehemu kubwa ya rasilimali za maji nchini ni majishirikishi *(transboundary waters)* na hivyo, haitoi mwongozo kuhusu usimamizi na matumizi ya maji hayo.

(4) Sheria ya sasa haitoi taratibu za kushughulikia ulinzi na usalama wa mabwawa. Kutokana na mabadiliko ya tabianchi, nchi yetu inahitaji kuwa na akiba ya maji *(storage),* kwa matumizi mbalimbali yakiwemo ya binadamu, mifugo, viwanda, kilimo cha umwagiliaji, uvuvi, utalii na mengineyo. Katika tathmini inayoendelea, tumebaini kwamba, kati ya mabwawa 160 katika Mabonde ya Kati (mabwawa 102) na Pangani (Mabwawa 58); mabwawa 15 yanavuja; mabwawa 80 yamemomonyoka matuta; 62 yana njia za mchwa *(antihills and holes);* 38 yana utoro *(spillway)* uliomomonyoka; 41 yamepungua ujazo *(reduced dam capacity);* na 8 yamejaa tope *(silted).* Tathmini inaendelea katika Mabonde yote kwa kutumia Wataalam wa Wizara yangu. Hali hii inahitaji ufumbuzi tukizingatia kwamba, mabwawa ni muhimu. Tutaendelea kuyajenga kwa ubora zaidi ili kuhakikisha uhakika wa upatikanaji wa maji *(water security),* kwa nchi yetu. Tutahakikisha tunayalinda ipasavyo.

(5) Mheshimiwa Spika**,** Sheria ya sasa pia haitambui haki za kimila za kutumia maji. Kama sote tunavyofahamu, jamii mbalimbali zimekuwa na taratibu za kijadi na kiasili za kutumia maji na kulinda vyanzo vya maji visiharibiwe. Mifumo ya maji ilikuwa na uongozi rasmi na aliyekiuka miiko alipewa adhabu. Wananchi wameendelea kutumia maji kimila bila kuwa na hati za haki ya kuyatumia. Kwa mfano, katika Bonde la Pangani kuna mifereji, 2,015 ya kijadi. Kati ya hiyo; mifereji 1,617 haina hati za haki ya kutumia maji. Maana yake ni kwamba, mifereji hii (ambayo ni asilimia 80 ya mifereji yote), haitambuliwi kisheria. Suala hili lisiposhughulikiwa, litasababisha migogoro mikubwa ya maji ikizingatiwa kuwa rasilimali za maji zinazidi kupungua.

Sheria inayokusudiwa kutungwa, itatambua haki za kimila za kutumia maji. Watumiaji wa maji kijadi watapewa muda wa miaka miwili kuomba hati na hawatatakiwa kulipa gharama za kuomba hati. Hati hizo zitakuwa na haki sawa na hati nyingine na kuandikwa katika daftari la hati.

(6) Mheshimiwa Spika, sheria ya sasa haitoi muda maalum wa hati za haki za kutumia maji. Utaratibu wa kutoa hati zisizo na ukomo, umesababisha migogoro ya matumizi ya maji kwa sababu ya ongezeko la idadi ya watu na mahitaji makubwa. Sheria

mpya itatoa muda maalum wa hati kwa kuzingatia madhumuni ya matumizi ya maji hayo na muda unaohitajika kwa mtumiaji kurudisha gharama, pale ambapo anayeyatumia maji hayo anayatumia kwa uwekezaji.

(7) Mheshimiwa Spika, pia sheria iliyopo haitoi maelezo kuhusu namna ya kutatua migogoro. Migogoro ya matumizi ya maji inazidi kuongezeka kutokana na shughuli za kiuchumi na kijamii na idadi ya watu kuongezeka. Sheria mpya itaweka bayana taratibu za kushughulikia migogoro hiyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kushughulikia upungufu uliopo katika sheria ya sasa, mambo muhimu yafuatayo yamezingatiwa:-

(1) Uhifadhi na matumizi ya maji chini ya ardhi: Tukiondoa maji yaliyo chini ya ardhi, ambayo bado yanafanyiwa utafiti; nchi yetu ina kilomita za ujazo 40 za maji chini ya ardhi, ambayo ni karibu ya nusu ya maji baridi yote nchini (kilomita za ujazo 89). Matumizi ya maji chini ya ardhi ni kidogo mno wakati maji juu ya ardhi yanazidi kupungua. Sheria mpya itaweka utaratibu bora wa matumizi ya maji hayo na uhifadhi wa maeneo yenye maji chini ya ardhi *(Groundwater Controlled Arears*).

(2) Kuimarisha utawala bora wa rasillimali za maji: Majukumu ya vyombo vyote vinavyohusika na usimamizi wa rasilimali za maji yameainishwa kuanzia ngazi za chini hadi ngazi ya Taifa. Watumiaji maji watakuwa na vyama vyao vya watumiaji maji *(Water Users Associations),* kuanzia ngazi za mabonde madogo hadi Bonde. Katika ngazi ya Taifa, inapendekezwa kuundwa Bodi ya Taifa ya Maji *(National Water Board)* ambayo itamshauri Waziri mwenye dhamana ya maji kuhusu sera, utekelezaji wake na masuala ya kitaifa na kimataifa yanayohusu rasilimali za maji.

(3) Mipango ya pamoja ya Rasilimali za Maji *(Integrated Water Resouces Management Plans):* Nchi yetu haijawahi kuwa na mipango ya aina hii. Katika miaka ya 70, tulikuwa na Mipango Kabambe ya Maji *(Water Master Plans).* Mipango hii ilihusu zaidi utoaji wa huduma ya maji *(water supply)* na ilifuata mfumo wa kimkoa. Kila mfadhili alichagua Mkoa alioupenda na hivyo tukawa na mipango 20 yenye mitazamo tofauti. Katika sheria mpya tutakuwa na mipango ya pamoja ya usimamizi wa rasilimali za maji kwa mfumo wa mabonde yote tisa, ambayo hatimaye itaunganishwa na kuwa na Mpango wa Kitaifa. Mipango hii itaonyesha mizania ya maji *(water balance),* upatikanaji na mahitaji ya maji kwa kila Bonde na jinsi ya kukidhi mahitaji. Mipango hiyo itafanyiwa mapitio kila baada ya miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Taifa ya Maji itatayarisha Ripoti ya Hali ya Rasilimali za Maji Kitaifa kila baada ya miaka miwili. Ripoti hiyo itawasilishwa Bungeni na Waziri mwenye dhamana ya maji.

Mheshimiwa Spika, kutungwa na kutekelezwa kwa Sheria ya Rasilimali za Maji kutaleta matokeo yafuatayo:-

(1) Kufutwa kwa Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Matumizi ya Maji ya Mwaka 1974;

(2) Kuundwa kwa Bodi ya Taifa ya Maji; na

(3) Kutambuliwa kisheria kwa ngazi mbalimbali za maamuzi juu ya usimamizi, utunzaji na uendelezaji wa rasilimali za maji, kuanzia ngazi ya chini hadi ngazi ya Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, naomba kutoa muhtasari wa masuala yaliyomo katika Muswada huu. Muswada umegawanyika katika sehemu kumi na sita kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza**,** inahusu jina la sheria, tarehe ya kuanza kutumika na tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika ndani ya Sheria inayopendekezwa kutungwa.

Sehemu ya Pili, inahusu msingi na malengo ya sheria inayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu, inahusu umiliki wa rasilimali za maji, madaraka na majukumu ya Waziri mwenye dhamana ya maji. Vile vile sehemu hii inabainisha haki ya matumizi ya maji kwa shughuli za kibinadamu na uvunaji wa maji ya mvua.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne, inahusu majukumu ya Waziri kuhusu usimamizi wa rasilimali za maji na mamlaka ya kukasimu baadhi ya majukumu yake. Sehemu hii pia inahusu masuala ya mfumo wa kitaasisi wa Bodi ya Taifa ya Maji, Bodi za Maji za Mabonde, Maafisa wa Mabonde, madaraka na majukumu yao. Sehemu hii inaelezea vyanzo vya mapato vya taasisi hizo, bajeti zao, hesabu na taratibu za ukaguzi wa hesabu. Sehemu hii pia inaelezea uundwaji wa vyombo vya wadau katika ngazi ya bonde dogo *(Catchment Water Committees)*, uendeshaji wa shughuli katika ngazi hiyo na vyanzo vya mapato.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano, inapendekeza kuwepo kwa mipango ya pamoja ya rasilimali za maji itakayotayarishwa kwa kushirikisha wadau katika ngazi ya bonde dogo *(Catchment Water Committees)*, Bodi za Mabonde na Bodi ya Taifa ya Maji. Mpango huo pamoja na mambo mengine utazingatia mizania ya maji katika kila Bonde nchini; uhamishaji wa maji kutoka Bonde moja kwenda Bonde lingine na; kiasi cha maji kitakachobaki kwenye mkondo wa maji *(reserve)*, kwa ajili ya mazingira, bioanuai na watumiaji wengine.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu utasaidia kuweka mipango ya pamoja ya matumizi ya rasilimali za maji kuanzia ngazi ya bonde dogo hadi Taifa na mipango hiyo itakuwa na nguvu za kisheria.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita, inasisitiza utunzaji wa vyanzo vya maji na utaratibu wa kuainisha rasilimali za maji ili kujua ubora wa rasilimali hizo. Rasilimali za maji zitaainishwa kwa kuzingatia aina, matumizi, eneo la kijiografia au kutumia vigezo vingine vitakavyowekwa. Sehemu hii inapendekeza hatua za kuchukuliwa na Bodi za Mabonde nyakati za kiangazi na nyakati za majanga. Vile vile sehemu hii inatoa maelezo ya kuwepo kwa Kanda za uhifadhi wa rasilimali za maji ili kuzilinda zisichafuliwe, kuzuia mmomonyoko wa ardhi au uharibifu wowote mwingine. Waziri mwenye dhamana ya maji, amepewa mamlaka ya kutangaza eneo kuwa *Protected Zone* au *Ground Water Controlled Area*. Lengo ni kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Saba, imeweka mchakato wa kupata hati ya haki ya matumizi ya maji juu ya ardhi na chini ya ardhi. Vile vile Muswada unapendekeza kutambuliwa kwa matumizi ya maji ya kimila yanayotumiwa na jamii au watu husika kwa rasilimali iliyo katika eneo lao.

Mheshimiwa Spika, sehemu hii inarekebisha mfumo wa hati ya matumizi ya maji ambayo imepewa pamoja na hati ya haki ya kumiliki ardhi. Sehemu hii pia imeweka utaratibu wa uhamisho wa vibali kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine ilimradi asikiuke mipango ya rasilimali za maji. Muswada umependekeza mchakato utakaotumika katika kumwaga maji taka na taratibu za kupata kibali cha kumwaga maji taka kwenye mikondo ya maji.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nane**,** inapendekeza uundaji wa jumuiya za watumiaji maji na taratibu za kuzisajili. Sheria mpya inapendekeza jumuiya za watumiaji maji zisajiliwe katika ngazi ya Bodi za Mabonde. Kwa sheria ya sasa, Waziri ndiye anayefanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tisa, inaelezea taratibu za ujenzi wa miundombinu kwenye Mabonde kwa ajili ya kuleta maendeleo endelevu na ufanisi katika usimamizi wa rasilimali za maji.

Sehemu ya Kumi, inahusu ulinzi na usalama wa mabwawa, usajili na udhibiti wa mafuriko. Kanuni zitatayarishwa kwa ajili ya ulinzi, udhibiti na usalama wa mabwawa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Moja, inapendekeza vyanzo vya mapato na jinsi mapato hayo yatakavyotumika. Vyanzo vya mapato vitakuwa kama ifuatavyo:-

(a) Malipo ya matumizi ya maji;
(b) Malipo ya kutupa maji taka;
(c) Malipo kwa huduma za mazingira *(payment for environmental services);* na
(d) Malipo kwa vibali vitakavyotolewa.

Mheshimiwa Spika Sehemu ya Kumi na Mbili, inahusu majishirikishi (*transboundary waters).* Lengo ni kuwezesha utekelezaji wa mikataba na makubaliano ambayo Tanzania imeridhia kuhusu usimamizi, udhibiti na matumizi ya majishirikishi kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Tatu, inahusu makosa, adhabu na taratibu nyingine za kimahakama.

Sehemu ya Kumi na Nne, inahusu rufaa. Waziri anaweza kuunda Kamati ya Rufaa ya kumsaidia kusikiliza rufaa mbalimbali zitakazoletwa kwake.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Tano, inahusu mambo ya jumla.

Sehemu ya Kumi na Sita, inahusu masuala ya kipindi cha mpito na kufutwa kwa sheria ya zamani ya kusimamia na kudhibiti matumizi ya maji.

Mheshimiwa Spika, baada ya Sera ya Taifa ya Maji ya Mwaka 2002, umepitishwa mkakati wa kutekeleza Sera hiyo na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Sheria itakayotungwa itakuwa nyenzo muhimu katika utekelezaji wa Sera na usimamizi wa Rasilimali za Maji kwa ajili ya kizazi cha sasa na vizazi vinavyokuja.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo haya, kwa heshima naomba Waheshimiwa Wabunge waujadili Muswada ulio mbele yao na hatimaye kuupitisha kuwa Sheria ya Rasilimali za Maji ya Mwaka 2009 *(The Water Resources Management Act, 2009).*

Mheshimiwa Spika, **'Maji ni Uhai na Usafi wa Mazingira ni Utu.'**

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA**: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyokubaliana, naomba sasa Waziri aendelee na hoja ya pili, baada ya hoja hiyo kuungwa mkono.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2009 *(The Water Supply and Sanitation Act, 2009)* kama ulivyorekebishwa kwa mujibu wa jedwali la marekebisho, sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, lengo la sheria inayokusudiwa kutungwa ni kuweka utaratibu wa kisheria utakaosimamia, kuendeleza na kutoa fursa kwa wananchi, vyombo vya kijamii na sekta binafsi katika kubuni, kujenga, kuendesha na kumiliki miradi ya maji na usafi wa mazingira.

Mheshimu Spika, naomba kutumia fursa hii, kwa niaba ya Wananchi wa Rungwe Mashariki, kutoa salamu za pole na rambirambi kwako, kwa Wananchi wa Biharamulo

na kwa familia, kufuatia kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Biharamulo, Marehemu Phares Kashemeza Kabuye.

Mheshimiwa Spika, Ijumaa, tarehe 24 Aprili, 2009, nilibahatika kupita eneo la ajali, robo saa baada ya ajali kutokea. Nasikitika juhudi zetu pamoja na Wananchi wa Magubike, kumuwahisha yeye na majeruhi wengine Hospitali ya Berega hazikufanikiwa. Nawashukuru wamiliki wa magari waliokubali kuwapeleka majeruhi wote hospitali. Naomba Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya Marehemu Kabuye na wengine waliofariki katika ajali ile, mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, huduma za maji na usafi wa mazingira nchini zinatolewa kwa mujibu wa Sheria ya Miundombinu ya Maji *(Waterworks Act)* ya Mwaka 1949 na marekebisho yake ya mwaka 1997. Marekebisho hayo yalilenga katika kuwezesha mambo yafuatayo:-

Uundaji wa Mamlaka za Maji Safi na Maji Taka na uunganishaji wa huduma za maji safi na maji taka ambapo hapo awali huduma za uondoaji maji taka zilikuwa chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa *(Local Government Authorities).*

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Sheria hiyo yalikuwa ni kusimamia usambazaji na kudhibiti huduma ya maji katika kipindi cha ukoloni na mara tu baada ya uhuru wa nchi yetu. Kutokana na mabadiliko ya sera za kiuchumi na kijamii yaliyotokea hapa nchini, vilevile kutokana na kuwepo kwa Sera ya Maji ya Mwaka 2002 na ongezeko kubwa la idadi ya watu na mahitaji ya maji kwa matumizi mbalimbali; Sheria ya Miundombinu ya Maji ya Mwaka 1949 kwa sasa haikidhi mahitaji ya kusimamia utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira mijini na vijijini.

Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa maelezo kuhusu mpangilio wa Muswada huu, naomba kutoa ufafanuzi kuhusu upungufu uliopo katika sheria inayotumika sasa, umuhimu wa kuwa na sheria mpya na mambo muhimu yanayozingatiwa katika Muswada wa Sheria ninayoiwasilisha kama ifuatavyo:-

(i) Sheria haitoi fursa ya kutosha kwa jamii, vikundi vya wananchi na sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika kubuni, kujenga, kuendesha na kumiliki miradi ya maji. Sheria mpya itatoa nafasi kubwa katika kuimarisha ushirikishwaji wa wananchi na wadau wengine katika kuendeleza sekta ya maji ili kufanikisha kufikiwa malengo ya Kitaifa na ya Kimataifa.

(ii) Imejengeka taswira kwamba, uendelezaji na uendeshaji wa miradi ya maji ni jukumu la Serikali peke yake. Sheria mpya imeainisha majukumu ya vyombo vyote vinavyohusika na usimamizi, uratibu, uendelezaji, ujenzi, uendeshaji na utunzaji wa miundombinu ya maji na usafi wa mazingira na udhibiti wa bei na ubora wa huduma ya maji. Sheria haiiondolei Serikali wajibu wake katika kusimamia na kuendeleza sekta ya maji.

(iii) Katika sheria ya sasa, majukumu ya usimamizi na utekelezaji wa miradi ya maji na usafi wa mazingira kwa makundi mbalimbali ya wadau, hayajawekwa bayana. Sheria mpya imezingatia majukumu ya Wizara yenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Sekretarieti za Mikoa, Serikali za Mitaa, yaani Halmashauri na Wizara yenye dhamana ya maji, ambayo ina majukumu katika kusimamia utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira, pamoja na taasisi na vyombo vingine.

(iv) Kwa mujibu wa Sheria ya sasa, Waziri mwenye dhamana ya maji, amepewa mamlaka ya usimamizi na uteuzi wa bodi za mamlaka za maji na usafi wa mazingira na usimamizi katika ngazi zote zinazohusu utoaji wa huduma ya maji, hata zile ambazo kawaida zinasimamiwa na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Ili kuleta ufanisi zaidi, lakini bila kuondoa umuhimu wa Wizara yenye dhamana ya maji katika usimamizi wa sera, mipango na utekelezaji katika ngazi zote; Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kupitia sheria inayopendekezwa, zimepewa majukumu makubwa zaidi, ikiwa ni pamoja na kuwa na mamlaka za uteuzi katika ngazi husika.

(v) Miradi mingi ya maji huwa haikamiliki au inapokamilika huharibika baada ya muda si mrefu. Pamoja na mambo mengine, hii inatokana na kwamba, hakuna usimamizi wa kisheria wa taaluma zinazohusiana na ujenzi, ukarabati na uendeshaji wa miradi ya maji. Sheria inayopendekezwa imeweka utaratibu wa kusimamia taaluma na ithibati, kuweka viwango na miongozo kuhusu teknolojia zitakazotumika katika ujenzi na usimamizi wa miundombinu na masuala ya nidhamu, kupitia Bodi ya Usimamizi.

(vi) Watoa huduma ya maji mbali na wale waliopewa leseni ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), wanapanga viwango vya malipo ya maji bila kuzingatia mwongozo. Sheria mpya inaelekeza kuwepo na miongozo ya kupanga bei za maji na viwango vya utoaji huduma ambavyo vitazingatiwa na watoa huduma ya maji.

(vii) Suala la mazingira halikupewa uzito na umuhimu unaostahili, hasa baada ya kutungwa kwa Sheria ya Mazingira, Sheria Na. 20 ya Mwaka 2004 katika kubuni, kujenga na kuendesha miradi ya maji. Sheria mpya inaweka bayana vigezo vitavyozingatiwa katika utekelezaji wa Sheria ya Mazingira, ambayo ni sheria mtambuka, hususan miradi ya maji. Vilevile itaweka msukumo katika hifadhi ya mazingira na utunzaji wa vyanzo vya maji.

(viii) Kukosekana kwa rasilimali ya fedha katika kuendeleza sekta ya maji kumekwamisha utekelezaji wa mipango na miradi mingi ya maji na kupunguza kasi ya kuyafikia malengo ya kitaifa na ya kimataifa. Sheria mpya inaunda Mfuko wa Taifa wa Maji *(National Water Investment Fund).* Mfuko huo utatoa mikopo yenye masharti nafuu kwa vyombo vya watumiaji maji na mamlaka za maji zinazojiendesha kibiashara ili kupanua wigo na kuboresha huduma na hivyo kupunguza mahitaji ya ruzuku kutoka Serikalini.

(ix) Kwa kuzingatia mfumo wake katika maeneo ambapo huduma ya maji inatolewa, sekta ya maji ni hodhi. Hivyo, udhibiti wa sekta ni muhimu ili kulinda

maslahi ya watumiaji bila kuathiri ubora wa huduma na maendeleo ya sekta yenyewe. Utoaji wa huduma ya maji kisheria hudhibitiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA).

Baada ya kuanzishwa kwa EWURA, imebidi itungwe sheria inayoiwezesha EWURA kusimamia sekta ya maji katika maeneo iliyopewa jukumu hilo kisheria. Sheria inayokusudiwa kutungwa inaitambua EWURA na kuainisha majukumu yake katika sekta ya maji.

(x) Katika baadhi ya maeneo nchini, huduma ya maji hutolewa na vyombo au vikundi vya watumiaji maji ambavyo vimechangia sana katika kupunguza kero kwa wananchi na vimeisaidia Serikali kutekeleza majukumu yake. Vyombo hivi sasa vinasajiliwa chini ya sheria mbalimbali. Kumekuwa na migogoro mingi kutokana na suala hilo. Imekuwa si rahisi kuviratibu wala kuvisaidia. Kwa kutumia sheria inayokusudiwa kutungwa, vyombo vyote vya wananchi vya watumiaji maji vitatambuliwa, kusimamiwa, kuendelezwa na kusaidiwa ipasavyo.

(xi) Hivi sasa huduma za maji na usafi wa mazingira zinatolewa na mamlaka za Serikali zenyewe au vyombo vya wananchi wenyewe. Kupitia sheria hii, mamlaka na vyombo vya wananchi vinaweza, mazingira yakiruhusu, kukasimu shughuli za uendeshaji kwa Wakala kwa mikataba.

(xii) Miradi mikubwa ya maji inayojumuisha vijiji vingi au zaidi ya Wilaya moja kama vile Miradi ya Makonde, Chalinze, Wanging'ombe, Maswa, Mugango - Kiabakari, Bomba Kuu la Mradi wa Handeni *(Handeni Trunk Main)* na Mradi wa Ziwa Victoria Kahama - Shinyanga, hivi sasa inasimamiwa kitaifa. Kupitia sheria hii, miradi ya aina hiyo na miradi ya aina hiyo itakayotekelezwa miaka ijayo, inatambuliwa rasmi na itaendelea kusimamiwa na Serikali kupitia Wizara yenye dhamana ya maji.

(xiii) Hivi sasa baadhi ya mamlaka za maji na usafi wa mazingira zina upungufu wa watumishi na nyenzo za kazi. Kupitia sheria hii mamlaka katika maeneo ya jirani, zitaweza kuunganishwa ili kuimarisha na kupunguza gharama za uendeshaji kutumia ya dhana ya klasta.

Mheshimiwa Spika, kutungwa na kutekelezwa kwa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira kutaleta matokeo yafuatayo:-

(i) Kufutwa kwa Sheria ya Miundombinu ya Maji ya Mwaka 1949 na marekebisho yake ya mwaka 1997;

(ii) Kuundwa kwa Mamlaka za Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira;

(iii) Kuundwa kwa Jumuiya za Wananchi za Huduma za Maji *(Community Owned Water Supply Organisations);* na

(iv) Kuanzishwa kwa Mfuko wa Taifa wa Maji.

Mheshimiwa Spika, katika Jiji la Dar es Salaam na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Pwani, huduma hizo za maji zinasimamiwa na Sheria ya Mamlaka ya Maji na Uondoaji wa Maji Taka ya Dar es Salaam *(Dar es Salaam Water Supply and Sewerage Authority Act, No. 20 of 2001)*.

Sheria ya DAWASA iliandaliwa na kutungwa sambamba na mchakato wa kutayarisha Sera ya Maji ya Mwaka, 2002. Hivyo basi, inakidhi matakwa ya sera na mikakati inayotumika sasa. Jiji la Dar es Salaam lina wakazi zaidi ya milioni nne. Nina hakika kwa siku moja kila siku watu wanaweza kuwa hata milioni saba. Changamoto za utoaji wa huduma za maji kwa wakazi hao ni kubwa na ni tofauti na miji mingine nchini, ambayo ni midogo ikilinganishwa na Dar es Salaam. Hakika siwezi kulinganisha Dar es Salaam na Tukuyu. Hali hii inahitaji sheria mahususi ya kusimamia huduma hiyo Dar es Salaam na maeneo mengine. Hivyo basi, Sheria ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira inayotarajiwa kutungwa, haitahusu maeneo yaliyo chini ya Sheria ya DAWASA.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, naomba sasa kutoa muhtasari wa masuala yaliyomo katika Muswada huu ambao umegawanyika katika sehemu kumi na tano, kama ifuatavyo:-

Sehemu ya Kwanza, inahusu jina la Sheria, tarehe ya kuanza kutumika, matumizi na tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika ndani ya Sheria hii inayopendekezwa.

Sehemu ya Pili, inahusu misingi na malengo ya Sheria inayopendekezwa.

Sehemu ya Tatu, inahusu masuala ya kiutawala. Sehemu hii inaainisha majukumu ya vyombo mbalimbali kama vile Wizara yenye dhamana ya Maji, Wizara yenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Majiji, Manispaa, Miji na Wilaya. Madhumuni ya hatua hii ni kuweka usimamizi wa utoaji huduma na utekelezaji karibu na wananchi ambao ni watekelezaji wakuu wa sera na Sheria inayopendekezwa.

Sheria hii mpya itasaidiana na Sheria za Serikali za Mitaa *(Local Government Authorities Cap. 287 & 288)* ili kuondoa migongano ya kisheria. Vyombo vya watumiaji wa huduma ya maji vitasajiliwa na Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji. Lengo ni kuwa na miradi ya maji endelevu katika ngazi ya chini inayomilikiwa na jamii kisheria.

Sehemu ya Nne, inahusu mfumo wa kitaasisi wa kuunda Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira, uteuzi wa Bodi zake na Watendaji Wakuu wa Mamlaka hizo. Sehemu hii inatoa mamlaka kwa Waziri mwenye dhamana ya maji kwa kushirikiana au kushauriana na Waziri mwenye Mamlaka ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kuunda Mamlaka hizo na vilevile kuunda mamlaka ambazo ni *cluster* ya mamlaka zaidi ya moja. Sheria itaendelea kutambua kuwepo kwa Mamlaka ambazo tayari zimekwishaundwa ilimradi ziendeshwe kwa mujibu wa sheria mpya.

Sehemu ya Tano, inahusu vyanzo mbalimbali vya mapato kwa Mamlaka zitakazoundwa na taratibu za matumizi na ukaguzi.

Sehemu ya Sita, inaelezea majukumu ya chombo cha udhibiti (EWURA), mchakato wa kutoa leseni na kusimamia viwango vya bei ya maji. Sheria hii ndiyo itakayosimamia utekelezaji wa majukumu ya EWURA katika Sekta ya Maji.

Sehemu ya Saba, inapendekeza kuundwa kwa vyombo vya jumuiya za wananchi katika maeneo yao, majukumu yake, usajili na jinsi vitakavyoendeshwa. Vyombo hivyo vitasajiliwa katika ngazi ya Halmashauri kwa kutumia kanuni zikazotengenezwa na Waziri mwenye dhamana ya maji. Kwa mifumo hii, inakuwa rahisi kwa Serikali kuvisaidia vyombo hivyo.

Sehemu ya Nane, inaelezea vyanzo vya mapato na masharti ya kupata ruzuku kwa vyombo vya jumuiya za wananchi.

Sehemu ya Tisa, inahusu usimamizi na ufuatiliaji wa utendaji wa vyombo vya jumuiya za wananchi. Miongozo mbalimbali itatolewa na Waziri mwenye dhamana ya maji. Waziri amepewa madaraka ya kukasimu majukumu ya kudhibiti vyombo hivyo kwa Serikali za Mitaa.

Sehemu ya Kumi, inaelezea majukumu ya Serikali za Mitaa kwa vyombo vyote vitakavyoundwa. Sera ya Maji inasisitiza Serikali za Mitaa kupitia Halmashauri, kuwajibika katika kupanga, kuendeleza miradi ya maji na kutunga sheria ndogo zinazohusu usimamizi wa Sekta ya Maji.

Sehemu ya Kumi na Moja, inatambua kuwepo kwa miradi ya maji kitaifa na inaelezea majukumu ya Serikali kuhusu miradi hiyo ya kitaifa.

Sehemu ya Kumi na Mbili, inahusu usimamizi wa utendaji *(Code of Workmanship)* kuhusu masuala ya ujenzi wa miundombinu ya huduma za maji. Waziri anapewa majukumu ya kuunda Bodi za Utambuzi (*Accreditation Boards)* na kutoa leseni kwa fani mbalimbali. Eneo hili la uhandisi wa maji, ufundi bomba, uashi na ujenzi wa miundombinu ya maji, halikuwa na utaratibu ulio bayana. Kanuni mbalimbali zitawekwa ili zisaidie katika kusimamia eneo hili, ikiwa ni pamoja na suala zima la nidhamu.

Sehemu ya Kumi na Tatu, inapendekeza kuundwa kwa Mfuko wa Kitaifa wa Maji, muundo wake, madhumuni, majukumu yake na vyanzo vya mapato. Mfuko huo utaanzishwa na Serikali kwa kushirikiana na Washirika wetu wa Maendeleo.

Sehemu ya Kumi na Nne, inahusu makosa na adhabu mbalimbali.

Sehemu ya Kumi na Tano, inahusu mambo ya mpito na mambo ya jumla. Vile vile sehemu hii inafuta Sheria ya Miundombinu ya Maji ya Mwaka 1949.

Mheshimiwa Spika, hatua tuliyofikia ni mchakato mrefu ambao umehusisha wadau wengi, ikiwa ni pamoja vyombo vya wananchi vya watumiaji maji, Mamlaka za Maji na Uondoaji wa Maji Taka Mijini, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Serikali za Mitaa na wegine. Washirika wetu wa Maendeleo wakiwa ni pamoja na Shirika la *World Wide Fund for Nature* (WWF), Mashirika ya Maendeleo ya Ujerumani (*GTZ* na *KfW),* Shirika la Maendeleo la Japan *(JICA)*, Benki ya Dunia, Shirika la *Water Aid* na Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Elimu kwa Watoto *(UNICEF),* wamehusika kikamilifu katika zoezi hili.

Vilevile napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Mawaziri walionitangulia, ambao wameniwekea misingi ya kuwasilisha Miswada hii. Nawashukuru wote kwa dhati kabisa. *(Makofi)*

Napenda kuchukua fursa hii vilevile kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mwandishi Mkuu wa Sheria na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, kwa hatua zote za maandalizi na hatimaye kukamilika kwa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, nichukue fursa hii kuwashukuru kwa dhati kabisa, Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Maji na Mifugo, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo**,** Mbunge wa Ileje, kwa kuupitia kwa undani kabisa Muswada ulio mbele ya Bunge lako Tukufu. Matokeo ya uchambuzi wao wa kina ni jedwali la mabadiliko kama lilivyosambazwa. Ushauri na maelekezo ya Kamati yatazingatiwa kikamilifu katika utekelezaji wa sheria. Nawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya Sera ya Taifa ya Maji iliyopitishwa 2002, umepitishwa mkakati wa kutekeleza Sera hiyo na vilevile imeandaliwa na inatekelezwa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji na inatekelezwa katika mpango wa muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. Sheria itakayotungwa itakuwa nyenzo muhimu katika utekelezaji wa Sera na utekelezaji wa programu. Ili sheria isiwe kikwazo, sheria iliyopo imepitiwa kwa kina na kufanyiwa marekebisho makubwa kiasi kwamba, sheria mpya haina budi kutungwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, kwa heshima Kubwa naomba Waheshimiwa Wabunge waujadili Muswada ulio mbele yao na kuuridhia na hatimaye kuupitisha kuwa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya 2009 *(The Water Supply and Sanitation Act, 2009).*

Mheshimiwa Spika, **'Maji ni Uhai na Usafi wa Mazingira ni Utu.'**

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA**: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, kwa hoja zote mbili na kwa mtiririko huo huo sasa namwita Mwenyekiti au Mwakilishi wa Kamati ili aweze kutoa maoni ya Kamati. Mheshimiwa Charles Keenja.

**MHE. CHARLES N. KEENJA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, napenda kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Miswada miwili ya maji. Muswada wa kwanza ni ule Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji wa Mwaka wa 2009 (*The Water Resources Management Bill, 2009*) na Muswada wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira wa Mwaka wa 2009 (*The Water Supply and Sanitation Bill, 2009*).

Naomba katika hatua hii, nieleze pia kwamba, natoa maelezo haya kwa niaba Mwenyeki wangu wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mbunge wa Ileje.

Naomba nichukue nafasi hii, kukupa pole na kuipa pole familia ya Mheshimiwa Kabuye, kwa msiba uliowapata. Mwenyezi Mungu, ailaze roho yake mahali pema peponi na awaimarishe. Amina.

Mheshimiwa Spika, maji sio tu kwamba ni muhimu, kama inavyoelezwa katika Sera ya Maji, bali ni ya lazima kwa maisha ya viumbe vyote duniani; bila maji hakuna uhai. Aidha, maji ni ya lazima kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kiwango cha maendeleo ya jamii yoyote kinategemea kuwepo kwa maji ya kutosha na yenye ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, maji yanaendelea kupungua siku hadi siku kutokana na sababu mbalimbali, zikiwemo za kuongezeka kwa matumizi kama alivyosema Mheshimiwa Waziri na uharibifu wa mazingira. Inakisiwa kwamba, upatikanaji wa maji Vijijini umefikia asilimia 50 tu. Mahitaji ya maji mijini yanakisiwa asilimia 73 ya mahitaji, lakini miji yetu mingi ina kiwango kidogo cha upatikanaji wa maji likiwemo Jiji la Dar es Salaam.

Kutokana na umuhimu wa maji kwa maisha ya Watanzania na kwa maendeleo yao ya kiuchumi na kijamii, kutokana na umuhimu wa kulinda na kuendeleza vyanzo vya maji ili kuhakikisha upatikanaji endelevu wa maji na kutokana na umuhimu wa kuwapo kwa mipango madhubuti ya kuwahakikishia wananchi wote upatikanaji wa uhakika wa maji, Kamati inaridhika kwamba, Miswada hii ni muhimu na imeletwa kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Waziri wa Maji alivyoeleza hivi punde, Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji wa Mwaka wa 2009,

unakusudia kufuta Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Matumizi ya Maji ya Mwaka 1974. Aidha, Muswada huu wa Sheria unakusudia kuweka utaratibu wa kulinda, kutunza, kutumia, kudhibiti na kuendeleza rasilimali za maji kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira unakusudia kufuta Sheria ya Miundombinu ya Maji ya Mwaka wa 1949 na marekebisho yake yaliyofanywa Mwaka wa 1997, ambao haukidhi mahitaji ya sasa ya kusimamia utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira mijini na vijijini. Aidha, sheria hii mpya inalenga kuweka utaratibu wa kisheria utakaosimamia, kuendeleza na kutoa fursa kwa wananchi na sekta binafsi katika kubuni, kujenga, kuendesha na kumiliki miradi ya maji. Kama Mheshimiwa Waziri alivyoeleza kwa kirefu, Muswada huu hautahusu Jiji la Dar es Salaam na maeneo yanahudiwa na DAWASA, ambao wako chini ya sheria tofauti ambayo inakidhi mahitaji.

Mheshimiwa Spika, Miswada hii ililetwa Bungeni kwa Hati ya Dharura ya Rais na iliwasilishwa kwenye Kamati tarehe 24 Aprili, 2009.

Kamati ilifanya jumla ya vikao vitatu Dodoma ili kujadili Miswada hii. Kikao cha kwanza kilifanyika tarehe 24 Aprili, ambacho kilihudhuriwa na Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wengine wa Wizara. Katika kikao hicho, Waziri aliwasilisha Hati ya Maelezo na Madhumuni ya Miswada yote miwili kwa pamoja.

Tarehe 25 Aprili, 2009, kilifanyika kikao cha pili ambacho kilikutanisha Kamati na Wadau na kuwapa Wadau fursa ya kujadili na kutoa maoni yao juu ya Muswada. Wadau walioshiriki ni pamoja na Wawakilishi wa Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dodoma (*DUWASA*), Bonde la Ziwa Victoria, Shirika la Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam (*DAWASCO*), Wakala wa Maji Mpwapwa, Wakala wa Maji Chiseyu, Serikali ya Kijiji cha Berega na Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati ya Umeme na Maji (*EWURA*).

Wadau wote hawa walitoa maoni muhimu sana, ambayo yamezingatiwa katika Jedwali la Marekebisho kama lilivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri leo asubuhi. Baadhi ya wadau walitupa ushahidi kwamba, walikuwa wameshirikishwa katika hatua mbalimbali za kuandaa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kikao cha tatu kilifanyika tarehe 26 Aprili, 2009 na kilihusisha tena Wizara na Kamati. Katika Kikao hicho Kamati ilipata fursa ya kutoa maoni na ushauri na kufanya marekebisho na masahihisho katika Miswada kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali la marekebisho ambalo limeshasambazwa kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza na kuishukuru Wizara, kwa kukubaliana na ushauri wa Kamati na mawazo ya Wadau. Kamati pamoja na Wadau, tumeridhishwa na Miswada na tunatoa maoni ya kuboresha utekelezaji kama ifuatavyo:-

(a) Baada ya Miswada hii kupitishwa na kuwa sheria, Serikali ihakikishe kwamba, Kanuni zinatengenezwa mapema iwezekanavyo ili kuwezesha utekelezaji mzuri kwa mamlaka zote zinazohusika.

(b) Serikali iendelee kuhamasisha na kutoa elimu kwa umma na wadau wote juu ya umuhimu wa kutunza na kulinda rasilimali za maji.

(c) Kwa kuwa maji ni ya lazima kwa uhai wa binadamu na ni haki ya msingi kwa kila mwananchi, Serikali iendelee kutoa kipaumbele cha pekee kwa kuitengea Sekta ya Maji fedha za kutosha kwenye bajeti zake ili kuiwezesha kupanua upatikanaji wa maji kufikia wananchi wote. (*Makofi*)

(d) Sheria itakapokuwa imekamilika kutungwa iwe msaada katika kutatua migogoro ya huduma za maji iliyopo, hasa katika miradi inayosimamiwa na asasi za kijamii.

(e) Serikali iweke mfumo utakaowezesha Halmashauri za Wilaya na Miji kuwajibika na kuhakikisha pesa za miradi zinazotengwa katika maeneo yao zinatumika kama ilivyokusudiwa.

(f) Serikali iwe na mipango endelevu ya upatikanaji wa maji ya kutosha kwa matumizi ya sasa na ya baadaye na kuepuka ukosefu wa maji kutokana na ukame na majanga mengine kama ambavyo imetokea huko nyuma.

(g) Serikali iandae mpango wa kufufua miundombinu ya maji iliyopo ambayo kwa sasa haifanyi kazi ili kupunguza tatizo la maji nchini.

(h) Upangaji wa bei za maji uzingatie kipato cha wananchi wa eneo husika na upatikanaji wa maji. Ihakikishwe kwamba, mtu hakosi maji kutokana na umaskini wake.

(i) Kutokana na kushamiri kwa wizi wa maji, Serikali haina budi kuwaelimisha na kuwashirikisha wananchi ili waweze kutumia njia sahihi za kupata maji.

(j) Katika maeneo yenye mfumo wa maji taka *(central sewerage system)*, wananchi wahimizwe kuunganisha nyumba zao na mfumo huo ili kuepuka milipuko ya magonjwa ambayo imekuwa ikitokea mara kwa mara.

(k) Sekta ya maji inakabiliwa na tatizo kubwa la ukosefu wa watumishi wenye ujuzi na uzoefu wa kazi. Hili amelieleza pia Waziri. Hali ni mbaya sana kwenye Serikali za Mitaa, ambako kuna watumishi wachache sana wenye sifa zinazotakiwa. Aidha, watumishi wengi wamestaafu au wanakaribia kustaafu na wataongeza pengo kubwa lililopo.

- Kamati inaishauri Serikali ihamishe baadhi ya watumishi wenye sifa zinazotakiwa kutoka Wizarani na kutoka kwenye asasi zilizoko chini ya Wizara na kuwapeleka kwenye Serikali za Mitaa ambako ndiko kwenye utekelezaji.

- Pia Serikali iandae Programu Maalum ya Kufundisha Wataalamu wa Maji ili kuhudumia sekta hii vizuri katika ngazi zote.

(l) Kamati inakubaliana na utaratibu wa Mamlaka za Maji kumilikishwa maeneo ambako mabomba ya maji yanapita. Mamlaka hizo ziandae ramani zitakazoonyesha mabomba hayo yanakopita na waweke alama zinazoonekana kwa urahisi ili wananchi wasijenge juu ya mabomba hayo au kufanya vitendo vyovyote vingine ambavyo vinaweza kuharibu mabomba hayo.

Mamlaka za maji zitambue kwamba, kwa kumilikishwa maeneo yanakopita mabomba, wanaweza kuathiri mashamba na mali nyingine za wananchi. Ni muhimu athari hizo zikapunguzwa kadiri inavyowezekana na pale maeneo ya wananchi yatakapohusika, walipwe fidia kwa viwango vinavyostahili.

(m) Serikali ihakikishe mgawanyo wa maji katika maeneo mbalimbali nchini unazingatia mahitaji halisi ya watu katika maeneo yao.

(n) Chini ya Miswada hii, Serikali za Mitaa zimepewa majukumu mbalimbali ya utekelezaji, usimamizi na hata uwezeshaji wa Bodi na Mamlaka zinazoundwa chini ya sheria hizi. Wizara ya Maji na Umwagiliaji na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, zihakikishe kwamba, Serikali za Mitaa zinaelewa majukumu hayo na kadiri itakavyowezekana, ziwezeshwe kuyatekeleza.

(o) Vyombo vya kusimamia ugavi wa maji vilivyoandikishwa chini ya sheria nyingine vihamasishwe kujisajili chini ya Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira katika muda uliowekwa ili nao wafaidike na huduma zitakazotolewa chini ya sheria hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwa ushirikiano wao na kwa kukubali kufanya kazi kwa bidii, kwa saa nyingi kwa siku zote tatu na kwa siku mbili za mwisho wa wiki. Napenda kuwatambua kwa majina Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Gideon A. Cheyo, Mwenyekiti wetu, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Teddy L. Kasella-Bantu, Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa Joyce N. Machimu, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mheshimiwa Abdulkarim E. Shah, Mheshimiwa Kaika S. Telele na Mheshimiwa Charles N. Keenja; anayewasomea maoni haya. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inawashukuru wadau wote waliojitokeza mbele ya Kamati na kushiriki kikamilifu katika kuwasilisha maoni na mapendekezo yao, ambayo yamesaidia katika kuboresha Miswada hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri, Mheshimiwa Prof. Mark J. Mwandosya, Naibu Waziri, Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza, Katibu Mkuu, Ndg. Wilson Mukama, pamoja na Watendaji wote wa Wizara na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa ushirikiano wao katika kipindi chote cha uchambuzi wa Miswada hii.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashililah, kwa kuiongoza Ofisi yake na kuiwezesha Kamati kuandaa na kukamilisha Taarifa hii. Aidha, napenda kumshukuru sana Katibu wa Kamati, Ndg. Pamela E. Pallangyo, kwa kuihudumia Kamati kwa juhudi sana katika kipindi hiki kifupi tulichokuwa nacho. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono Miswada hii. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Charles Keenja, kwa niaba ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji. Sasa nitamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, nadhani ni kwa niaba ya Mheshimiwa Salim Hemed, ambaye ninamshangaa anatoka wakati huu. Aah! Umo ndani basi ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nifanye *clarification,* mimi ndio Waziri Kivuli wa Maji na sio Mheshimiwa Salim.

**SPIKA:** Samahani sana, haya mabadiliko niliyapata, nimeghafilika. Nakuomba radhi sana. *(Makofi)*

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa afya njema na hivi sasa niko mbele yenu ili kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji wa Mwaka 2009, yaani *The Water Resource Management Act of 2009,* kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(6), Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimimiwa Spika, naomba kutoa salamu za pole kwa familia, ndugu, jamaa, pamoja na Wananchi wote wa Jimbo la Biharamulo, kwa msiba mkubwa uliowapata wa aliyekuwa Mbunge wao, Mheshimiwa Phares Kashemeza Kabuye; na wote waliofariki katika ajali ile. Vilevile tunatoa pole kwa wale wote ambao wamepata majeraha. Vilevile umetutangazia kifo cha aliyekuwa mke wa Marehemu Adam Sapi Mkwawa, tunatoa pole pia kwa niaba ya Kambi ya Upinzani. Roho yake ilazwe mahali pema peponi, Amina.

Mhesimiwa Spika, mbali na hayo, naomba kwa dhati kabisa, kutoa pongezi kwa waziri, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Mbunge, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Injinia Christopher Kajoro Chiza, Mbunge, pamoja na timu nzima ya Wataalamu wa Wizara hii, kwa kutayarisha Musada huu wa kutunza rasilimali za maji.

Mheshimiwa Spika, kama sote tunavyoelewa, maji ndio kila kitu katika uhai wa binadamu, maji ni kilimo, maji ni viwanda na kubwa zaidi kwetu sisi kama Wanasiasa, maji ni siasa. Kwa utangulizi huo, ninasikitika sana kwamba, Muswada huu umeletwa haraka sana kiasi kwamba, umetunyima fursa ya kutosha ya kutoa mawazo mbadala, yaani *constructive criticism* na kupata mawazo ya wadau mbalimbali waliomo katika shughuli nzima zinazojihusisha na maendeleo ya maji.

Kutokana na ongezeko kubwa la idadi ya watu, wastani wa matumizi ya maji kwa mtu hadi kufikia ile dira ya 2025 ambayo ndio nguzo au kioo cha Sera ya Maji, ambapo idadi ya watu inakadiriwa kuwa itakuwa imefikia milioni 60 na wastani wa matumizi ya maji kwa mtu kwa mwaka inaweza kuwa imeshuka hadi kufikia *cubic metre* 1500 kutoka *cubic metre* 2700 mwaka 2000, ambapo Tanzania ilikuwa na idadi ya watu milioni 33. Kwa mujibu wa wataalamu, matumizi ambayo yapo chini ya wastani wa *cubic metre* 1700 kwa mwaka, inatafsiriwa kuwa ni upungufu au uhaba wa maji. Hii ni hatari sana kwa nchi kama Tanzania, ambayo maji ndio kiini cha kila kitu katika uchumi.

Mheshimiwa Spika, katika nchi zilizoendelea duniani, matumizi ya maji katika shughuli za kilimo ni 80% ya matumizi yote ya maji, 25% ya matumizi ya maji yote ni kwa ajili ya matumizi ya viwandani na 5% ni kwa ajili ya matumizi ya majumbani. Kwa utaratibu huu, sisi tunajiweka wapi katika matumizi endelevu ya rasilimali hii ya maji?

Katika sura ya nne, sehemu ya (C) ya Muswada, ambayo inatoa idhini ya kuundwa kwa Bodi ya Taifa ya Maji, pamoja na majukumu yake, Kambi ya Upinzani baada ya kupitia muundo wa Bodi na Majukumu yake ni dhahiri inaonesha kuwa Bodi hii ndio itakuwa chanzo cha ukiritimba katika utekelezaji wa majukumu ya msingi katika kuhakikisha rasilimali za maji zinaandaliwa na kuendelezwa. Ukiangalia sura hiyo hiyo ya nne, kipengele (D), inatoa mwongozo wa kuundwa kwa mabonde ya maji, *Basin Water Boards,* pamoja na muundo wake mzima na kazi zake; ni dhahiri unaona kuwa sehemu hii ndio hasa ipo kwa wadau wakuu na vilevile ipo karibu na zile Kamati za Vidakio vya Maji (*Catchment Committees),* kama vifungu vya 29 na 30 vya Muswada huu vinavyoonesha.

Kambi ya Upinzani inaona majukumu haya yameainishwa kwa ajili ya *Basin Water Boards* na ukaribu wake na wadau, kwa maana ya ushirikishwaji kama Sera ya Maji inavyosema. Utekelezaji wa dhana nzima wa ugawaji wa madaraka kwa wananchi (*D by D),* hapa ndio mahala pake na sio Bodi ya Taifa ya Maji.

Mheshimiwa Spika, hoja yetu hii inapewa nguvu zaidi na vifungu kadhaa katika Muswada huu, pale inapoonesha kuwa *Basin Water Board* ndio inayotoa na kusimamia vibali mbalimbali vya matumizi endelevu ya maji. Kwa maana nyingine, *Basin Water Boards,* ndizo hasa zipo kwa wale wanaotakiwa kushirikiana na Serikali katika

kuhakikisha rasilimali za maji zinakuwa endelevu. Aidha, kifungu cha 133 cha Muswada kinachoongelea *transfer of responsibilities to the Boards and Committees,* kinaonesha dhahiri jinsi *Basin Water Boards* zinavyoweza kufanya kazi vizuri zaidi na Serikali bila kutegemea uwepo wa Bodi ya Taifa ya Maji sambamba na hicho kifungu cha 114.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani kwa mtazamo huu inashauri vifungu vya 20 na 21 viingizwe au vihuishwe kwenye vifungu vya 22 na 23 vya Muswada huu. Tunashauri hivi kwa kuwa yale masuala ambayo yanahusu ushirikiano wa kimataifa, yatafanywa na watendaji walio Wizarani kama Wakuu wa Idara au Wakurugenzi, kulingana na masuala husika. Aidha, katika masuala yanayohusiana na ushauri katika mambo ya sera ni dhahiri yanaweza kutolewa ushauri mzuri zaidi na wale wote walio karibu na watekelezaji wa sera ambao ni wadau wa Muswada huu. Kambi ya Upinzani, inataka ipatiwe ufafanuzi pale mtu anapohitaji kutumia maji yaliyo chini ya ardhi, lakini eneo hilo si mojawapo ya *ground water controled area* kama vile ilivyoelezwa katika kifungu cha 38 cha Muswada; inakuwaje?

Aidha, Kambi inataka kujua Mamlaka ya *Basin Water Board* yanaishia wapi? Je, Mamlaka yake yanatanuka hadi maeneo ambayo si sehemu ya mabonde ya mito au ziwa? Mfano, mfugaji wa Dodoma au Kahama akitaka kuchimba kisima kwa ajili ya matumizi binafsi, kibali atapata wapi? Kambi ya Upinzani imetaka fafanuzi huo kutokana na kifungu cha 54(1). Nanukuu: *"Or any other area shall apply for a ground water permit in accordance with this Act."* Hapa neno *any other area*, ndilo hasa tunataka kuelewa ni maeneo gani mengine zaidi ya mabonde ambayo yana rasilimali za maji?

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 56(1) kinachosema nanukuu: *"No person shall be granted a Groundwater Permit for any well or borehole within distances prescribed under subsection two of this section."* Kifungu kinachofuata cha 56(2), hakioneshi hizo *distance* ambazo mtu yeyote hatakiwi kupata na badala yake kinasema Waziri ndiyo atakayetoa ufafanuzi wa *distance* hizo kwenye kanuni. Kambi ya Upinzani inaomba ufafanuzi zaidi kwenye kifungu hiki cha 56.

Kifungu cha 53(1) kinachohusiana na kumwaga maji taka kutoka viwandani au sehemu zozote ambazo ni vyanzo vya uzalishaji au utoaji wa maji taka; Kambi ya Upinzani inaelewa kuwa kuna takataka nyingine ambazo pindi zikitolewa na kuingia kwenye vyanzo vya rasilimali ya maji, madhara yake ni makubwa mno kama vile taka zenye mchanganyiko wa zebaki, yaani *mercury*, zinazotoka kwenye makampuni yanayochimba dhahabu; hasa hasa katika Wilaya ya Tarime na Geita na wachimbaji wadogowadogo wa dhahabu katika maeneo mbalimbali katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 64 kinaongelea adhabu kwa yeyote atakayetenda kosa kwa kumwaga maji taka kwenye vyanzo vya maji. Kifungu kizima hiki hakioneshi wale walioathirika na kadhia hii nzima ya maji taka hayo kwenye vyanzo vya maji watafidiwa vipi? Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi kuhusu waathirika wa uchafuzi huo wa maji, pamoja na mali zao, yaani mifugo. Muswada huu unawaangalia vipi? Suala hili lilishatokea kule Geita na serikali inalielewa vizuri.

Kambi ya Upinzani inaona kuwa jukumu la utoaji wa kibali kwa ajili ya umwagaji wa maji taka na *treatment* ya maji taka hayo ili kuyaweka katika mfumo mzima wa kuyatumia upya; yaani *waste water re-use or re-cycle,* lingekuwa chini ya mamlaka nyingine tofauti na *Basin Water Boards.* Naomba kunukuu kifungu cha 69(2): *"Every Basin Water Board shall supply without lay to the National Water Board a copy of every entry made in the water register."'* Kwa kuwa tulikwishashauri kuiondoa Bodi ya Taifa ya Maji; hivyo ni bora hiyo nakala iende moja kwa moja kwa Mkurugenzi wa Rasilimali za Maji. Hii inaondoa ukiritimba wa *middlemen,* ambao hata katika biashara za kawaida ndiye mtu anayeongeza ukiritimba na kuongeza gharama zisizokuwa za lazima katika suala zima la uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iliangalie suala hili kwa makini, kwani tunaamini kuwa, suala sio kuwa na Bodi tu kwani inatakiwa kama kuna kazi ambazo haziwezi kufanywa na asasi nyingine katika mfumo huo, ndipo umuhimu wa Bodi unapokuwepo. Kwa mfumo wa sheria hii, umuhimu huo haupo. Kutokana na muda wa kupitisha Muswada huu kuwa mfupi, Kambi imejitahidi kubaini hayo; na kwa niaba yake naomba kuwasilisha. Hivyo, naomba pia niwasilishe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusiana na Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira kama ulivyoshauri.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kumshukuru Mungu, kwa kunipa afya njema ili niweze kusimama mbele yenu na kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Muswada wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2009, yaani *The Water Supply and Sanitation Act, 2009* kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(6), Toleo la 2007. Kabla ya kuanza kuangalia vifungu mbalimbali, ambavyo tunaona tunatakiwa kuangalia upya, kwa kuangalia Muswada huu ulivyo ni dhahiri kuwa, waziri amelimbikiziwa madaraka makubwa sana, kiasi kwamba akiupitia mtu mwingine ambaye yuko *neutral,* kwa maana kuwa si mmojawapo wa waliohusika kwa namna yoyote ile na utunzi wa Muswada huu, atashangaa ni kwa nini inakuwa hivi katika mazingira ya sasa, ambapo madaraka yanapelekwa chini kwa wananchi. Kwa mantiki hiyo, Kambi ya Upinzani, inaomba *powers* alizopewa Waziri ziangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 9(4) cha Muswada kinachosema kuwa, Waziri anaweza kutoa tamko kama Mamlaka ya Maji iwe inaendeshwa kibiashara au la kwa kuangalia vigezo ambavyo vitawekwa na Waziri mwenyewe; Kambi ya Upinzani inaliona hili kuwa ni tatizo kwani tunaamini kuwa chombo ambacho kinaweza kutoa uwezo wa Mamlaka ya Maji kuendeshwa kibiashara au la ni Baraza la Madiwani, kwani ndilo linaloelewa kwa undani hali halisi ya wananchi wanaopata huduma ya maji katika Manispaa au Halmashauri husika. Aidha, kifungu hicho kinamaanisha kuwa, Mamlaka ambazo hazijatolewa tamko la kuwa ziendeshwe kibiashara zitatoa huduma hiyo bure kwa wananchi. Kwa hiyo, tunaomba ufafanuzi wa hilo.

Kifungu cha 11 kinachohusu uteuzi wa Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi za Mamlaka za Maji za Wilaya na Miji kuwa watateuliwa na Waziri. Kwa kuangalia wingi wa Mamlaka za Maji katika nchi hii na kifungu kinavyotaka kuwa kabla ya uteuzi

atafanya *consultation;* hii *consultation* inayozungumziwa ni lazima Waziri akubaliane nayo au ni mojawapo tu ya kutimiza wajibu? Kambi ya Upinzani inaona hapa mamlaka aliyopewa Waziri ni makubwa mno, kiasi kwamba, hata ile dhana nzima ya kupeleka madaraka kwa wananchi inakuwa inapotea.

Mheshimiwa Spika, chombo kikubwa kinachosimamia mipango na utekelezaji wa Sera za Serikali ni Baraza la Madiwani, pamoja na Wakurugenzi wa Manispaa za Wilaya. Je, ni kwa nini sheria isitoe haki kwa chombo hicho? Tunaona utaratibu uliowekwa kwenye kanuni kuteua Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi za Mamlaka za Maji na Bodi hizo ziwajibike kwa Baraza la Madiwani. Kifungu cha 21(1)(g) kinasema kuwa, vifaa vya kuunganishia huduma ya maji kwa mteja vitatolewa na Mamlaka. Kambi ya Upinzani inaona kuwa, kwa kuwa sasa ni soko huria na mteja atatakiwa kununua vifaa hivyo na Mamlaka inafanya biashara, hivyo itakuwa si busara na ni kuendeleza ukiritimba kama Muswada unavyosema kuwa vifaa ni lazima vitolewe na Mamlaka tu. Kama Mamlaka itakuwa inaunganisha huduma ya maji kwa mteja bure na mteja anatakiwa aanze kulipa huduma hiyo bila ya kulazimika kununua vifaa, basi kifungu hiki kitakuwa ni sahihi.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 38(1) na (2) cha Muswada, kinaonesha ni jinsi gani ambavyo hata vikundi vya kijamii vya maji visivyokuwa na uhuru wa kuendesha shughuli zao kutokana na katiba zao zinavyosema, kwani utendaji wao wa kazi ni maelekezo kutoka kwa Waziri. Je, ni kweli kuwa hizi *community owned water supply* ni asasi zenye madaraka kamili ya kuamua jinsi ya kuendesha shughuli zao (*autonomous)* kama zinavyotakiwa kuwa? Aidha, Kambi inauliza ni vipi zile *water user associations* ambazo tayari zimeshaundwa na zinafanya kazi itabidi zibadilike kiutendaji na kufuata maelekezo kutoka kwa Waziri kama Muswada unavyohitaji? Kwa hiyo, tutaomba pia ufafanuzi juu ya hilo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. Kama nilivyosema muda ulikuwa ni mfupi sana na hayo ndio tuliyoweza kushauri. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mhonga. Hata hivyo, umewasilisha kwa ufanisi mkubwa tu.

Waheshimiwa Wabunge, hoja hii ilikwishatolewa na nitaomba muiamue. Hadi sasa nimepata wachangiaji 24 na hakuna maana yoyote ya kuendelea kupokea majina, kwa sababu hata hawa hatuwezi kuwafikia wote. Kwa uzoefu wetu hapa Mezani ni kwamba, leo wanaweza kuchangia 14 na kesho asubuhi labda watatu hivi. Kwa hiyo, nitawataja wale wanne wa mwanzo tu kwa maana ya kujiandaa. Ataanza Mheshimiwa Omari Kwaangw', Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Mohamed Abdallah, Mheshimiwa Benson Mpesya na Mheshimiwa Kidawa Saleh.

Kwa sasa hivi basi namwita Mheshimiwa Omari Kwaangw', ajiandae Mheshimiwa Mohamed R. Abdallah.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali ya Maji na pengine kabla sijafanya hivyo, ninaomba na mimi nitumie nafasi hii, kutoa rambirambi kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Babati Mjini, kufuatia kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Biharamulo Magharibi, Mheshimiwa Kabuye na misiba mingine ambayo imetokea hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii, kwanza kabisa, kumpongeza Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Naibu wake, pamoja na Katibu Mkuu, kwa kuleta Muswada huu kwa wakati. Kwa kweli pengine mengi yamechelewa, lakini ninadhani huu ni muda muafaka wa kuleta Muswada huu. Kabla sijachangia maeneo ambayo ninakusudia kuyatolea maoni, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Waziri wa Maji na Umwagiliaji, kwa kuuchagua Mji wa Babati kwenye Mkoa mpya wa Manyara kupeleka Mkutano wa Mamlaka zote za maji safi na maji taka Mjini Babati.

Mji wa Babati ni mpya na nina hakika Wizara itakuwa imejifunza ni namna gani mji mpya unakabiliana na changamoto, hasa katika kuhakikisha kwamba, sekta hii ya maji inafanikiwa. Vilevile nitumie nafasi hii, kumshukuru kwa kazi aliyoifanya ya kutembelea vyanzo vya maji kwenye Jimbo la Babati Mjini na vilevile kuzindua Mradi wa Maji kwenye kijiji ambacho kilikosa maji kwa miaka 15 mfululizo; Kijiji cha Malangi. Kwa kweli tunawashukuru sana Serikali, kwa ajili ya kuwapatia maji Wananchi wa Kijiji cha Malangi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie nafasi hii, kutoa maoni kwenye maeneo machache na hasa katika maeneo ya usimamizi wa rasilimali hizi za maji, uundwaji wa mamlaka zenyewe, ulinzi wa rasilimali, lakini vilevile nitumie nafasi hii kuzungumzia suala la udhibiti wa maeneo kama ya mafuriko na vyombo vya utumiaji maji na kadhalika. Nianze na hili la usimamizi wa maji; kwenye kifungu cha 37 cha Muswada, ulinzi wa sehemu zenye vyanzo vya maji na kifungu kile cha 38(4) vilevile usimamizi wa vyanzo vya maji chini ya ardhi na kifungu cha 107 ambacho kinatoa mambo ya jumla. Katika meneo haya, nataka nichangie eneo la fidia na nitatoa mfano; bahati nzuri Mheshimiwa Waziri alipokuja Babati alipata nafasi ya kusikiliza wananchi ambapo utafiti ulionesha kwamba, maeneo ambako wamekaa yapo maji na kwa hiyo wapo kwenye vyanzo vya maji kwenye Bonde la Maisaka.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, katika eneo hili katika vifungu nilivyovitaja, imetajwa fidia kwamba; kutakuwa na fidia endapo maeneo yatakayoonekana kwamba kuna vyanzo vya maji basi wananchi walio katika maeneo hayo watapewa fidia. Hoja yangu iko hapo kwamba, utaratibu wa fidia na viwango, najua fidia ambayo kwa sasa inaendelea kutumika inafuatia Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999, Sheria Namba 4 na Namba 5. Fidia kwa mtu ambaye amekaa katika eneo na kwamba amekaa kwa miaka mingi sana na mbaya eneo lake sasa linaonekana kwamba ni chanzo cha maji. Mtu amekaa miaka 20, 30, amekuwa akitegemea eneo hilo, halijawahi kutambuliwa na Serikali kuwa ni eneo la chanzo cha maji. Sasa unapomuondoa ukitumia taratibu hizi za kawaida, kwa kweli ni sawasawa na kuchezea maisha ya mwananchi; unapomwondoa tu kwa namna ambayo ni rahisi sana na ambayo nitaielezea baadae kidogo.

Mheshimiwa Spika, ardhi inabeba vyanzo vya maji, mafuta na madini; sasa vitu hivi unapovichukua kwa madhumuni ya manufaa ya umma, tunakubali kabisa kwamba ni jambo zuri na hasa katika kuhifadhi maji. Tunajua maji ni uhai wa binadamu na kwa hiyo, hapo wala hatuna mjadala wowote. Mtu aliyekaa pale pengine alikuwa na eka zake mbili au tatu, alikuwa anatumia katika kulima mazao na ndio anasomeshea watoto; sasa unapomuondoa kwa vipengele vile nilivyosema, kwa fidia ambayo sasa inatumika katika maeneo mbalimbali; kama ni ile ardhi kwa mfano ninayoifahamu ya Babati kwamba, eka moja kama mtu analima tu mazao ya kawaida na hana mazao ya kudumu, basi labda analipwa 350,000 au 360,000 kwa eka. Sasa kama ana eka zake mbili ambazo ndio anazitegemea kwa maisha yake yote pale, ndio unamlipa hiyo laki saba; ni lazima tujiulize anakwenda wapi huyu na atakwenda kuishi vipi na familia yake? Hili ni lazima liwe jambo la msingi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia taratibu zinazotumika kwenye Halmashauri zetu, kuna tatizo kubwa sana kwamba, hatujiulizi wananchi hawa ambao wanapewa fidia heka moja wanakwenda wapi? Nitoe mfano; kwa mfano, kwenye Halmashauri ya Mji wa Babati, kwenye eka moja inayoichukua kutoka kwa mwananchi, inaweza ikatoa ploti nane na sana sana itamwachia moja na zile nyingine saba Halmashauri itauza tena kwa bei kubwa sana na itategemea eneo hilo liko wapi; inaweza ikauza kwa milioni mbili, tatu au tano. Huyo mtu atakuwa ameachiwa ploti moja na hana pa kwenda na hana kitu chochote. Sasa fidia ya aina hii tunadhani kwamba, haimtendei haki mwananchi hata kidogo, kwa sababu atakwenda kufanya nini na shilingi laki tatu au hata laki saba wakati maisha yake yote ile eka moja alikuwa anailima vizuri au alikuwa anaitumia vizuri na kupata mapato yanayotosheleza kwa shughuli za maisha yake?

Mheshimiwa Spika, nilidhani fidia kwenye maeneo kama haya ambako ni vyanzo vya maji au hata katika maeneo mengine ni lazima iwe ya haki na sheria inatamka. Lazima tujiulize; fidia halali na ya haki ni ipi? Kwa mtizamo wangu ni fidia ile ambayo tayari wakati ule thamani ya ardhi ina soko katika eneo lile. Kwa mfano, katika maeneo ambayo naweza kusema ya Babati, thamani ya ardhi katika maeneo ya kawadia eka moja inaweza kwenda mpaka milioni moja na nusu au mbili. Tena haya ni maeneo tu ambayo yako pembezoni mwa mji. Halmashauri inatoa fidia ya laki tatu na nusu au laki tatu na elfu sitini.

Sasa fidia ya aina hii haitawasaidia wananchi wetu na mimi ninadhani hapo hatutendi haki hata kidogo. Sheria ya Ardhi iko wazi kwamba, thamani ya ardhi mtu anapoondolewa pale mahali basi ni lazima ifuatwe bei iliyoko sokoni. Sasa kama ardhi katika maeneo hayo ni milioni moja kwa heka, basi itolewe hii milioni moja lakini bado sioni kama ni haki. Kwa nini Halmashauri zinapochukua kwa mfano kama ni eneo la mtu wao wameshalipima wamelichukua, wanakwenda sasa kuliuza kwa vipimo vya *square metre* kiasi fulani shilingi kadhaa, lakini unapochukua fidia kwa mwananchi unasema tu kwamba eka moja; sasa hii haina mantiki hata kidogo.

Nilidhani kwamba ni lazima Halmashauri zetu ziachane na fidia za aina hii, kwa sababu madaraka yapo kwa Halmashauri na wala hayako Wizarani. Ardhi iko pale, taratibu ziko pale, kinachotakiwa ni bei ya soko.

Mheshimiwa Spika, najua Mheshimiwa Waziri, alipata muda wa kuongea na wale wananchi na wale wananchi wanachohitaji ni baada ya yale maeneo kutambulika kwamba ni vyanzo vya maji; ni fidia iliyo halali, fidia isiyocheleweshwa, ukiichelewesha basi inakuwa ni tatizo kubwa sana. Kwa hiyo, nilitaka niweke angalizo hilo kwenye vifungu vile vya 37(4), kifungu cha 38 na kwenye mambo ya jumla, ambapo nazungumzia kifungu cha 107, yanayohusu vilevile habari ya fidia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba niende kwenye eneo lingine ambalo ni utafiti wa vyanzo vya maji na utekelezaji wa kuchimba visima. Utafiti unachelewa na ndio maana katika maeneo mengine tunapata migogoro mingi sana. Serikali inachelewa kutafuta maeneo ambayo kuna vyanzo vya maji.

Unakuja kuvitafuta wakati watu wameshajenga miundombinu yao katika maeneo hayo na ndio haya ambayo yametokea katika maeneo ya vyanzo vya maji. Nadhani katika miji mingi, watu wengi wamekuwa wakihamishwa, nadhani hata hapa Dodoma ilifanyika katika maeneo ya Mzakwe na Makutupora kule. Watu wamehamishwa lakini unakuja wakati ambapo umechelewa sana. Watu wameshajenga katika maeneo ambayo ninayasema, kwa mfano, bonde hili la Maisaka la Babati, watu wamejenga nyumba nzuri, wamepanda mimea ya kudumu na miti. Jambo hili lingefanyika miaka mingi iliyopita, kusingekuwa na tatizo. Kwa hiyo, Wizara inachelewa, tunaomba utafiti ufanyike kwenye maeneo mengi katika muda mfupi iwezekanavyo, kujua hapa ni chanzo cha maji na watu wanafidiwa na ninadhani kwa mtindo huo tutakwenda vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, ninao mfano mwingine ambao utekelezaji ulichelewa sana; mfano wa kisima kirefu kilichogundulika Kijiji cha Singe, Babati, ambacho kinaitwa *AR 202* mwaka 1977. Utafiti ulifanyika mwaka 1977 na kwa kiwango kidogo cha fedha, baadaye katika mwaka 1989 kazi ile ilirudiwa tena. Gharama ya utafiti ilikuwa ni 153,000 na gharama ya kuchimba kisima katika eneo lile zilikuwa zimefikia 1,551,200. Leo tunapomwomba Waziri atusaidie au Wizara ichimbe kisima kwenye eneo hilo hilo ambalo kuna chanzo kikubwa na kizuri cha maji; kisima cha kawaida tu ambacho kwa mfano Halmashauri ya Mji imeomba sasa gharama yake ni zaidi ya milioni 100; kwa hiyo, tunaweza tukaona jinsi ambavyo tunachelewa. Eneo hili kulingana na maeneo hayo ambayo nimeyasema, tumeshawasilisha Wizarani ili gharama zisiendelee kwa sababu eneo hilo ni la chanzo cha maji mengi.

Wizara ifanye bidii iweke kisima hapo na eneo hilo lizuiwe vizuri ili tusiendelee kuchelewa, kwa sababau baadaye tutataka tena kuchimba visima vikubwa zaidi katika eneo hilo, ambapo watu watakuwa wamejenga. Kwa hiyo, hili ndio tatizo ambalo linatusibu kwa kuchelewesha utafiti na kuhakikisha kwamba uchimbaji unafanyika. Kama nilivyoeleza, eneo hili tangu mwaka huo wa 1977 kulipatikana maji, 1989 utafiti uliendelea, uchunguzi ukafanyika mpaka miaka ya 90, fedha ziliahidiwa haikuwezekana na sasa gharama ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, vilevile hizi Bodi ni nyingi sana. Hivi kila mahali tutakuwa tuna Mamlaka za Bodi? Gharama hizi ni kubwa sana, kwasa babu baadaye zinawekwa kwa mteja. Hivi ni lazima kuwa na Mamlaka ya Maji kila Wilaya au kila mahali tunapokwenda; na je, zinafanya kazi kubwa kiasi gani? Kwa nini tusiwe na Mamlaka za Kanda na gharama ikawa kidogo? Kule tu kwenye maeneo husika tukawa na Kamati Ndogo zile za wadau ambazo zingetosha kuainisha matatizo yanayopatikana. Kwa sababu gharama za Bodi kwa vyovyote vile ni kubwa, maana ukiona Muswada mzima kwenye maeneo haya ni Bodi zitateuliwa na zina watu na gharama ni lazima zitakuwa kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa nataka kusema kwamba ni vizuri vilevile Wizara ikaangalia eneo hilo. Ahsante sana na ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili kuweza kuchangia Miswada miwili iliyo mbele yetu. Kabla ya yote, nichukue nafasi hii, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Pangani, nitoe rambirambi kwa msiba wa Mheshimiwa Kabuye, aliyefariki hivi karibuni; tumwombe Mungu amuweke mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu Waziri, kwa kuuleta Muswada huu wakati wote ulikuwa wa *emergency,* mpaka tutamaliza dunia hii bado *emergency* ya maji itakuwepo. Kwa hiyo, kila tukiendelea kuweka sheria nzuri zaidi kwa matumizi ya maji katika dunia hii, tutakuwa tuna mafanikio makubwa. Tunatabiri kwamba, vita kuu inayofuata huko mbele ni kwa sababu ya maji.

Mheshimiwa Spika, mimi nianze na Muswada huu wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2009. Nina maeneo matatu madogo tu; kwanza, Miradi ya Maji Vijijini, ambayo Serikali inaisimamia na kutoa fedha nyingi kama Miradi ya *Quick Wins* na mingine ambayo itakuwa inafadhiliwa na World Bank. Niipongeze Serikali, imejitahidi sana wamechimba visima vingi, lakini kwa bahati mbaya visima hivi vimebaki na maji chini na wananchi hawayapati. Tatizo kubwa ni suala zima la miundombinu ya umeme.

Kubwa katika suala la umeme ni *transformers*, nafikiri Wabunge wengi humu ndani wana visima ambavyo viko *dormant* pale vinasubiri viweze kutumika; lakini sasa kidogo inatupa tabu kwa Serikali nzima kwamba hivi utatuzi wa hizi *transformer* ni nini? *Of course,* tunajua *transformer* mtekelezaji mkuu ni TANESCO; sasa hapo kuna Wizara ya Maji, utakuta kuna Wizara ya Nishati, halafu kuna chombo kingine kimeanzishwa cha *REA.* Sasa mimi ninavyoona hii *REA* ndiyo wenye matatizo sasa, maana yake mmeshaongeza chombo kingine kati yake, kati ya Wizara ya Nishati na Madini ili kiweze kuratibu na kupitisha pesa zipite huko. Sasa sijui mtafanyaje, naomba ulitazame hili Mheshimiwa Waziri. Kama unavyofahamu, hata kwako 2010 inakaribia, sasa tukibaki na mashimo ya maji na tusipokuwa na maelezo itakuwa ni tatizo kwa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia ni suala zima la ulipaji fidia katika maeneo ya vyanzo vya maji. Vyanzo vya maji tumekwisha vianisha katika wilaya zetu na taarifa zimeshakwenda Wizarani na wale watu sasa wanatakiwa waondoke katika yale maeneo ili vile vyanzo viweze kutunzwa tusije tukachelewa zaidi. Kwanza, kwa kuendelea kuharibu mazingira ya eneo lile kwa sababu ya uchimbaji wa vyoo katika maeneo yale ya makazi, watu wanatakiwa waondoke.

La pili, gharama ya ulipaji fidia kila tukichelewa inaongezeka. Mimi kwa Pangani nilikuandikia barua Mheshimiwa Waziri, bado tunasubiri ulipaji wa fidia katika chanzo cha maji cha Mjini Pangani, ambacho kipo Boza. Wizara yako inafahamu na naiomba tafadhali na Katibu Mkuu anasikia, hebu tuharakishe tulipe fidia hawa watu waondoke, wala sio pesa nyingi hazizidi milioni 60.

Mheshimiwa Spika, suala lingine uchafuzi wa mazingira; maji yanayotoka viwandani na sheria zilizokuwepo kwa ajili ya kudhibiti haya yasiharibu mazingira. Mimi ninayetoka Tanga, tunapofika Tanga Mjini ambayo ndiyo Makao Makuu ya Mkoa wa Tanga, ndiyo kwenye viwanda vianavyomwaga maji katika mfereji mkuu unaopeleka maji baharini, mfereji ule umewekwa kwa ajili ya kutoa maji ya mvua.

Sasa wameutumia mfereji ule kwa kutoa maji ya kiwanda ya rangi nyekundu na bluu umechanganyika na ukienda baharini utakuta mazingira yaliyoharibika katika eneo lile. Sasa hivi hakuna samaki anayevuliwa; Manispaa imepiga kelele imeshindikana. Tumezungumza kwenye Vikao vya RCC, hakuna hatua inayochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri kama kuna Kamati Ndogo, iende Mjini Tanga ijionee hali halisi. Ikifika nitashukuru, kwa kuwa nilipewa taarifa ili niwepo, kwa sababu hii hoja nimeieleta hapa Bungeni kuwathibitishia suala hili.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia ni suala zima la usimamizi wa rasilimali za maji za mwaka 2009. Katika Sheria hii, mimi kwanza naishukuru Serikali kwa uamuzi wake mzuri wa kuhamishia suala zima la miradi ya umwagiliaji kwenda Wizara ya Maji. Hilo ni jambo zuri sana na litakuwa linaondoa mgongano nani ambaye atasimamia umwagiliaji wa maji ni Wizara ya Kilimo au Wizara ya Maji; sasa iko wazi kwamba masuala ya maji yako Wizara ya Maji. Wataalamu wote ambao wapo katika miradi hii ya umwagiliaji wanatoka Wizara ya Maji; wapo katika kanda mbalimbali, hilo tunalipongeza; lakini tunaomba muongeze wataalamu ili miradi ya umwagiliaji iweze kuongezeka na hasa katika hali ya uchumi wa dunia sasa hivi, suala la chakula ni muhimu sana na maji bado tunayo ambayo yatatiririka kwenda baharini ambayo hayatumiwi vizuri.

Vilevile Bajeti ya Wizara ya Maji, pamoja na kwamba, Wizara ya Maji inaomba pesa nyingi lakini kuna suala la *sealing* na kama Wizara ya Fedha iko hapa inatusikia, tumegundua kwamba, bajeti ya miradi hii au miradi ya maendeleo ya maji katika Wizara kwa miaka ya 2005/2006, 2006/2007, 2007/2008, *trend* yake imekuwa inashuka. Sisi tunataka kuendeleza kilimo cha umwagiliaji, tunataka kuendeleza visima maji, tunataka kuwe na vyanzo vipya vya maji, tuna matatizo mengi ya maji katika Miji Mikuu kama

Dar es Salaam, lakini ikiwa *trend* ya bajeti kila mwaka inapungua, hatutofika tunakotaka kwenda.

Kwa mujibu wa taarifa ambayo tumeipata sisi kwenye Kamati ya Hesabu za Serikali, Wizara inahitaji angalau kila mwaka ipate bilioni 70 kwa ajili ya miradi. Sasa sio pesa nyingi kuweza kutengeneza miundombinu mizuri ya maji na kuhifadhi maji, hatimaye baada ya miaka michache tutaona fidia kubwa. Wataalamu wetu wameshakutengenezea michanganuo mingi tu, sasa isibaki ile michanganuo ikawa iko kwenye *shelf* kwa sababu ya bajeti.

Pamoja na kwamba, ile michanganuo baada ya muda itakuwa imepitwa na wakati halafu tutengeneze mingine, hiyo ni kuzidisha gharama na hatimaye malengo yetu hayatatimia kama Ilani ya Uchaguzi inavyosema. Kwa hiyo, naiomba Wizara na Wizara ya Fedha, mtizame upya miradi ya maji angalau ipate fedha za kutosha, kuweza kukamilisha malengo ya miradi waliyokuwa nayo, hatimaye tuweze kuondoa haya matatizo; bila pesa hizo, tutapiga kelele hapa mpaka tutamaliza muda wetu, watakuja wengine watapiga kelele; kama pesa za kutosha kwa ajili ya miradi ya maji hazitatolewa ni tatizo kubwa sana.

Lingine ninaloomba kwa kupitia sheria hii, mtazame upya vilevile suala zima la kuhifadhi maji katika mabwawa makubwa, ambayo yapo *along* au sambamba na mito mikubwa ambayo tunayo hapa nchini.

Kutengeneza hifadhi za maji au mabwawa makubwa ya maji wakati wa ukame tusiwe na matatizo ya upungufu wa maji. Kwa mfano, Mto Ruvu hujenga mabwawa makubwa ya kuhifadhi maji ili kupunguza uhaba wa maji. Ile *flow* ya maji iwe *constant*, wakati wa kiangazi na wakati wa mvua. Hii itasaidia kuhifadhi maji kwa wingi, kwa sababu maji yale yanatiririka yanakwenda baharini bila ya matumizi yoyote mengine katikati; hatuna miradi ya umwagiliaji, hatuna *reserve* za mabwawa ya kuhifadhi maji na hizo *reserve* za mabwawa pia zinaweza zikatumika katika matumizi ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia hapa ni udhibiti wa matumizi ya maji na halisi ya Mto Pangani, ambao unaanzia katika Milima ya Kilimanjaro na vyanzo vingine. Chemchemi nyingi zilizoko njiani mpaka unafika Nyumba ya Mungu hatimaye tunafuata. Sasa sisi Watu wa Pangani tumeathirika sana na matumizi haya ya maji, ambayo udhibiti wake umekuwa ni mdogo sana. Mheshimiwa Waziri unafahamu kwamba, Mto Pangani unaishia baharini, lakini wakati wa maji kujaa au *high tidy* chumvi inafika mpaka kilomita nane ndani ya mto; mashamba yote ambayo yapo karibu au kati ya kilomita nane hizi ya minazi na mpunga yamekwishaathirika hivi sasa kwa sababu ya chumvi iliyokuwepo pale.

Maji ya bahari yakiingia, mto ule unavimba kwa kuwa maji mengi ya bahari yanaingia ndani na yana kasi, kwa sababu ya upungufu wa maji baridi ambayo yanatoka *upstream*. Sasa nimeshalipigia kelele hili, Mheshimiwa Waziri wewe umeshafika Pangani pale, umeona tuna tatizo kubwa sana la kuingia maji ya chumvi ndani ya mto, kwa sababu ya upungufu wa maji yanayotoka juu.

Matumizi hayakuratibiwa vizuri, yangeratibiwa vizuri kusingekuwa na hili tatizo; ukienda *upstream* huko *along the river* utakuta kuna maji mengi yanamwagika bila sababu yoyote na kwa sababu ya kukosa udhibiti. Naamini sasa kwa sheria hii, hilo litasaidia kudhibiti hiyo hali.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na hayo ya kuzungumza, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na niseme naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuchangia katika Miswada yote miwili iliyoletwa na Waziri wetu wa Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nitoe shukrani zangu za dhati na pongezi nyingi kwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara hii, kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kushirikiana na sisi na mimi nikiwa mmojawapo wa Wanakamati katika kuhakikisha kwamba, tunaifanikisha kazi hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nataka niseme kwamba, sheria hii imekuja kwa wakati wake na ina mtazamo wa mashirikiano zaidi kati ya mtoa huduma na mteja, kuliko ilivyokuwa sheria ya mwaka 1949, ambayo ilikuwa na ukandamizaji kidogo na upungufu mwingi. Sheria hii inakusudia kuwajali zaidi wananchi; kama unavyojua, Dira ya Taifa ya Mwaka 2025 inaeleza wazi kwamba, maji ni moja kati ya nyenzo za kupiga vita umaskini. Kwa hiyo, unaweza ukaona kwamba ni muhimu sana kuwepo na maji, lakini vilevile ninaamini kwamba, sheria hizi zote mbili kwa pamoja zitatatua tatizo tulilonalo kwamba, karibu asilimia 44 ya Watanzania wote katika nchi hii hawapati maji safi na salama. Ninaamini kuwepo kwa sheria hizi mbili, kutaondoa na kupunguza kwa kiasi kikubwa, tatizo hili la Watanzania kutopata maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nielekeze mchango wangu katika Muswada ule wa Usimamizi wa Rasilimali za Maji wa Mwaka 2009, hasa sehemu ya nane, kipengele cha 43, juu ya vibali vya matumizi ya maji.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili, ninaomba niseme kwamba, katika maeneo ambayo kuna vyanzo vya maji, wananchi wanaoishi maeneo yale wapewe nafasi ya kwanza katika kupata vibali vya matumizi ya maji kuliko wale wengine ambao wanakuja. Nayasema haya, kwa sababu watu wale ambao wako kwenye vyanzo vya maji, ndiyo hasa wanaotunza vyanzo vile.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mfano wa wananchi wangu kule Mbeya Mjini, kwenye miteremko ya Mlima Mbeya, Kata ya Iziwa, hawa wanaotunza vyanzo vya Mto Mfwizimo, lakini hawajapata nafasi ya kutumia maji yale. Bahati nzuri, wanaishukuru sana Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Mbeya Mjini, ambao walipochukua maji yale angalau walijitahidi kupitisha maji na kuwapatia wananchi. Maji yale kwa kiasi kikubwa yamechukuliwa na kambi yetu ya Jeshi la Ulinzi 44KJ kule Mbalizi.

Mheshimiwa Spika, wananchi hawa maji ni mali yao ya asili, hawana urithi mwingine zaidi ya maji haya, lakini sasa wamepigwa marufuku hata chini ya mto hawaruhusiwi kuyatumia maji yale kwa matumizi mengine yoyote. Huu ni ukandamizaji, kwa sababu ile ni mali yao asili, wameruhusu Mamlaka ya Maji Safi imechukua maji, Jeshi letu limechukua maji tunakubali, lakini kwa nini wananchi hawa sasa wanaozunguka yale maeneo wanaambiwa wasiyatumie yale maji kwa matumizi mengine hata katika vishamba vidogo vidogo vya umwagiliaji?

Tulikuwa na sheria kandamizi ya mwaka 1949, ninaamini kupitia sheria hii, wananchi wangu wa Iziwa sasa watapata nafasi ya kupewa kibali cha kuyatumia maji ya Mto Mfwizimo, kama linavyotumia Jeshi la Wananchi wa Tanzania na kama inavyotumia Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka. Tusiwanyanyase na tusiwagandamize; ni watu huru katika nchi yao.

Mheshimiwa Spika, naomba nielekeze mchango wangu mwingine kwenye Muswada wa pili wa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira, sheria ya mwaka huu wa 2009. Naomba nijielekeze sehemu ya pili, kifungu cha nne, juu ya lengo la Muswada.

Mheshimiwa Spika, ibara ya 13 inazungumzia juu ya matumizi ya maji ya Umoja wa Mataifa; imetamka kwamba, maji ni haki ya msingi kwa binadamu na ni matarajio yangu kwamba, kupitia sheria, Mheshimiwa Waziri utatueleza wale wanyonge, wale maskini, tunajua kwamba tuna yatima wengi katika taifa hili; tuna wazee, tuna wajane na wengine ambao hali zao haziwaruhusu kuvuta maji ndani ya nyumba; tunawasaidiaje kuhakikisha kwamba wanaipata haki hii ya msingi?

Katika lengo la Muswada, imeelezwa wazi kwamba, lengo ni kutimiza hili; ninaamini utakuwa na kanuni ambayo itaelekeza wazi kwamba, watu hawa wanastahili kupata kiasi gani cha maji na kila mtu anastahili kupata kiasi gani cha maji kwa siku ili tusiwanyime haki yao ya msingi ya kupata maji ambayo ni haki kama inavyoainishwa na ibara ya 13 katika majukumu ya Umoja wa Mataifa juu ya maji.

Mheshimiwa Spika, ukienda sehemu ya sita ya Muswada, hasa kipengele cha 57, juu ya mamlaka ya udhibiti; mimi naomba niseme hapa juu ya EWURA tumekuwa na malalamiko. Nakubaliana kwamba, wapo watu wanaiba maji na wanaitia hasara Serikali na jambo hili lazima lidhibitiwe kwa kutoa elimu ya kutosha. Upo upande wa pili, EWURA; inapaswa sasa ijue kupitia sheria hii kwamba, mamlaka za maji nazo zinawaibia wateja; kama ninalipa bili ya maji wakati sijapata maji wiki nzima na nalazimika kulipa kwa wiki hiyo, huu nao ni wizi kama si wizi basi tuuite unyang'anyi. Haki haiwezi kuwa ya upande mmoja, haki lazima iwe ni *two way traffic*; kama wenzetu tunatakiwa tulipe bili ya maji na wao wanatakiwa watoe maji kwa kiwango kinachotakiwa. Tunasemaje EWURA, lazima iangalie yale maji yanayotoka kama *drip* ya mgonjwa wa hospitali, unalipa kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, kwa sababu unaweza ukamaliza hata wiki mbili, tatu, hujapata maji, lakini bili iko pale pale, sasa naamini EWURA itakata mzizi wa fitina kama inavyotoa vifungu vile vya sheria vinavyoeleza kwamba, mtu akipatikana anaiba

maji, kifungu gani kitalipa; mbona kifungu hakielezei na yule anayenyimwa maji mwezi mzima, lakini bili anapelekewa atafanyiwa nini? Kipindi hiki tuache zile sheria za mwaka 1949, ambazo ni kandamizi kwa wananchi. Sheria hii sasa ni ya kujenga mahusiano kati ya mteja na mtoa huduma, lazima tuelewane hapa.

Mheshimiwa Spika, nalizungumza hili kwa ukandamizaji uliopo pale, maeneo mengine anapatikana mwizi aliyeiba maji, lakini unakuta hawa wafanyakazi wa Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka wanakuja wanakata maji kwa eneo zima. Inawezekana pale ni *locality,* ambayo ina watu zaidi ya 100 na aliyeiba maji ni mtu mmoja na wanamjua, lakini matokeo yake wanakata bomba linalopeleka maji kwa watu mia moja ambao hawana hatia. Huu nao ni ukandamizaji, lazima sheria ionyeshe huyu mlaji wa maji atakuwa na haki zipi. Aliyeiba maji mnamfahamu na amekatiwa, lakini mnakata maji kwa bomba zima ambalo lina-*supply* eneo lile lote. Tunaomba hili nalo mliangalie kwa jicho ambalo linatakiwa tujenge mahusiano mazuri kati ya mtoa huduma na mtumiaji wa maji, ule ubabe kupitia sheria hii sasa uishe.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya saba ya Muswada huu, kipengele cha thelathini na moja kinaelezea juu ya asasi za kijamii zitakazotoa huduma za maji. Ningependa niweke wazi hapa, katika maeneo mengine hizi asasi za kijamii zilishaanzisha miradi ya maji. Asasi za kijamii zilikuwa na miundombinu yake zilikuwa zinatoa maji, lakini sasa kwa sababu hazina uwezo tena wa kuweza kukidhi mahitaji ya watu wao wanaoongoza, lazima kuwe na *intervention* ya Serikali. Mahali hapa sheria inasemaje, ambapo wananchi walikuwa na mradi wao wa maji, sasa imekuja mamlaka ya maji inasema sasa tunaunganisha hizi nguvu? Tunashukuru kwa sababu naamini ni tendo zuri na sasa tutapata maji ya kutosha kupitia hilo.

Unasemaje juu ya hii mali ambayo mmeirithi kutoka kwa hao watu? Mheshimiwa Waziri unajua, ninazungumzia juu ya Bonde la Uyole, wananchi wa mitaa kama Utukuyu, Mwahala kule Uyole, Iduda, Ibara, Ilove, ambao walijiwekea mradi wao wa maji, hatimaye mradi huo ukachukuliwa na mamlaka ya maji bila makubaliano, bila *memorandum of understanding*. Matokeo yake, kabla wananchi hawajakaa sawa, wanashtukia wanaletewa bili, tena bila kuimarisha kitu chochote katika miundombinu ile. Analiona ni bomba lake, alichangia kwa kuchimba mfereji, maji yamefika sasa analetewa bili na mtu ambaye hakumwona akishiriki katika kuleta maji yale. Tunaleta manung’uniko na masikitiko yasiyokuwa na sababu.

Ninaomba hili limalizwe, haiwezekani mtu unajua vya bure vilikwisha siku nyingi, huwezi ukawa unarithi miundombinu ya watu bila hata kuwa na maelewano, nasema tukae tuangalie tunawafidia nini. Mheshimiwa Waziri, nimeshakudokeza juu ya suala hili, naomba lipatiwe ufumbuzi wa kutosha kupitia sheria hii.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa, nizungumzie juu ya sehemu ile ya kumi na mbili, juu ya kanuni nafikiri za usimamiaji wa kazi, lakini sijaona kipengele kinachozungumzia juu ya teknolojia sahihi. Kwa nini nalizungumza hili? Sasa hivi lazima tubadilike, kama alivyozungumza Mheshimiwa Kwaangw’, hakuna mtu atakayekuwa anakubali au hata kama atakubali kwa mujibu wa sheria, lakini tutakuwa

tunawaumiza kutoa ardhi yao kubwa waondoke waende mahali pengine kwa ajili ya kupisha miradi kama hii.

Nilifikiri kwamba, tukizungumzia juu ya teknolojia sahihi, tunazungumzia juu ya mabwawa ya maji safi na maji taka; lazima itumike teknolojia ambayo mabwawa haya hayatachukua eneo kubwa zaidi. Iwepo teknolojia ambayo itarahisisha. Eneo linalotosheleza katika teknolojia hii, nakupa mfano wa eneo langu lile la Kalobe, lenye mabwawa ya maji machafu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mpesya, unalipenda sana jimbo lako na wewe ni askofu, kwa hiyo, umezoea kuhubiri kwa muda mrefu.

Waheshimiwa Wabunge, muda uliosalia hautuwezeshi kumwita mchangiaji anayefuata; lakini kwa faida ya kujiandaa, saa kumi na moja tutaanza na Mheshimiwa Kidawa Salehe, atafuatia na Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Kaika Telele na Mheshimiwa Pindi Chana. Hao ndio wanne wa kwanza kwa saa kumi na moja.

Sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa kumi na moja jioni.

*(Saa 06.57 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirejea)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Zubeir Ali Maulid) Alikalia Kiti*

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami nitoe mchango wangu wa Miswada hii miwili ambayo iko mezani sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mmoja kati ya Wajumbe wa Kamati ambao tulichambua Miswada hii kwa kina na kupitia kifungu kwa kifungu kwa hiyo, hivi sasa nitakuwa na mchango wa jumla tu kwa Miswada hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuungana na wenzangu kutoa pongezi kwa Waziri na timu yake kwa kuleta Miswada hii Bungeni, ni Miswada muhimu sana kwa nchi yetu na wananchi wote wa Tanzania. Muswada umekuja kwa wakati muafaka kwa sababu kuna matatizo mbalimbali ya ukame, uhaba wa maji na usimamizi wa maji. Kwa hiyo, Muswada huu umekuja kwa wakati ili raslimali maji ziweze kusimamiwa vizuri na wananchi walio wengi waweze kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubaliana wote kuwa maji ni uhai kwa maana kuwa bila maji hakuna maisha, mimea inategemea maji, wanyama wanategemea maji, viumbe hai vingi vinategemea maji, maji yakikosekana hakuna chakula, watu wanafariki

na mfano hai ni binadamu mwenyewe asilimia kubwa ya mwili wa binadamu ni maji. Kwa hiyo, tukikosa maji tunaondoka duniani wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonyesha dunia hii ambayo tunaishi kuna maji mengi sana, karibu 70% ni maji lakini kati ya hiyo 70% ni 67.5% ni maji ya chumvi ya bahari . Kwa hiyo, hayawezi yakatumika kwa mahitaji ya kawaida ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia iliyobaki yaani 30 ndiyo maji baridi, lakini maji yenyewe baridi ni 2.5% ambayo yanaweza yakatumika kwa matumizi ya binadamu na mengine yote yako katika hali ya barafu ambayosi rahisi kuyatumia. Kati ya hayo 2.5% ni na 70% ambayo ni 1.75% ni maji ambayo kama nilivyozungumza ni maji ya barafu lakini 30% tu iliyobaki ambayo ni 0.75% ya 2.5% ndiyo maji ambayo yako kwenye unyevunyevu wa udongo na maji ambayo yako juu na chini ya ardhi na kati ya hayo 0.25% tu ndiyo maji ambayo yako katika hali ya maziwa na mito ambayo ndiyo yanaweza kutumiwa na binadamu na yako katika kina cha chini ya ardhi ambayo tunaweza tukachimba visima ili kuyatumia kwa shughuli za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimetoa hapa takwimu hizo kuonyesha hali ya maji ulimwengu ni hizi ni *data* za kiulimwengu kuwa tuna 0.25 tu ya maji ya maziwa na mito ambayo tunaweza tukatumia kwa ulimwengu mzima. Kwa hiyo, hii asilimia ikigawanywa kwa nchi zote za ulimwengu tuone ni kijiasilimia kidogo sana cha maji ambacho ndicho tunaweza kuyatumia. Tukiangalia nchi yetu ya Tanzania tunaweza tukajisifia tunashukuru Mwenyezi Mungu ametusaidia tuna mito mikubwa, tuna maziwa makubwa tukaona tuna maji mengi. Lakini maji haya kama hatukuyahifadhi, kama hatukuyatumia vizuri, kama vianzio vya maji havikutunzwa, yanaweza yakatoweka kwa sababu vyanzo asilia vya maji, yaani maji asilia hayaongezeki, huwezi ukatengeneza mto mpya, huwezi ukatengeneza Ziwa wewe binadamu, hili lipo limeumbwa na Mungu, yoyote yanayotengenezwa yanakuwa ni *artificial* unaweza akatengezwa mto *artificial*, linaweza kutengezwa bwawa *artificial* lakini mabwawa na mito hii inayotengenezwa na sisi binadamu inategemea maji asilia kuyajaza.

Lakini maji haya haya ya asilia yanaweza yakaondoka kwenye ramani ya dunia kama hatukuyahifadhi na hatukuyatumia vizuri, mto unaweza ukaondoka moja kwa moja hata uwe mkubwa kiasi gani kama hatukulinda vyanzo vya maji, tukaharibu mazingira, mto unaweza ukakauka na ukaondoka kabisa katika ramani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimezungumza haya ili wananchi wote tujue kuwa hali ya maji inaweza ikahifadhiwa na sisi wenyewe na tunaweza tukaiharibu sisi wenyewe tukazidi kukosa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji ya maji yameongezeka kwa sababu watu tunaongezeka, tunazaliana kwa wingi kila watu wakiongezeka shughuli za kiuchumi zikiongezeka, kwa hiyo, mahitaji ya maji yanaongezeka lakini vianzio viko palepale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni muhimu sana elimu ya kuhifadhi vyanzo vya maji itolewe na Wizara isituambie kwamba inatoa kwa njia ya televisheni, redio au

vipeperusi au mabango. Wazazi wangu kule vijijini baba na mama hivyo vipeperushi haviwafikii. Hiyo televisheni wala hawaangalii na wala haipo kwa sababu hata huo umeme kijijini haupo, muda wa kusikiliza redio hakuna maana mama yangu kule kijijini kutwa nzima yuko kondeni. Lakini la kufanya, sisi hapa Tanzania tuna bahati, Serikali ina mtandao mzuri wa vyombo vyake kuanzia ngazi ya juu mpaka kule vijijini, kuna Wenyeviti wa Vijiji, Watendaji wa Vijiji na kadhalika. Tukiangalia chama tawala ina mtandao mpaka chini kwenye eneo la nyumba kumi, kwa hiyo, tutumie viongozi wale waweze kutoa elimu hii ya kuhifadhi maji na itakuwa ni rahisi zaidi kwa sababu wanaweza wakaelimishana kwa kutumia hata lugha ambayo wanazungumza pale vijijini, wote tunajua kwamba katika vijiji vingi wanandungu ndiyo wanaishi pamoja, kwa hiyo, wanaweza wakatumia hata ile lugha inayofahamika pale wakapeana hiyo elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ushirikishwaji wa wanajamii katika udhibiti wa vyanzo vya maji ni jambo muhimu sana na ninashukuru sana katika Muswada huu imeonekana kwa sababu wale wenyewe ndiyo watakaosaidiana kupangiana zamu kuangaliana nani anaharibu maji, kukanyana na wakaweka ulinzi madhubuti wao wenyewe baada ya kuelewa umuhimu wa utunzaji wa vyango vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ijaribu sana kutibu au kutafuta majawabu kabla madhara hayajawa makubwa, kama tumeona kuna mwelekeo kuwa jambo fulani au shughuli inaweza ikaharibu vyanzo vya maji, au inaweza ikaharibu mazingira, kwa hiyo, i-*act* haraka kutafuta suluhu ya tatizo lile. Natoa mfano, tatizo lililotufika la Ihefu walianza kwenda ng’ombe makundi madogo madogo, wakaendelea na kuendelea, lakini wananchi wapo wanawaona, viongozi wapo wanawaona mpaka wamekuwa tena ng’ombe wengi mno wameharibu vyanzo vya maji tunaona pale bwawa la Mtera likapungua maji, umeme ukawa shida na kadhalika kwa kuchelewa kuchukua hatua za haraka lakini ingekuwa tangu pale mwanzo, tatizo linapojitokeza haraka haraka tunatafuta suluhu hili tatizo lisingetokea na ambalo mpaka leo bado linahangaisha vichwa vya Viongozi wa Serikali na Viongozi wa vyama wanaohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kudhibiti matumizi ya maji yasiwe holela ni suala letu sote wanajamii, lakini pamoja na Serikali kwa mfano, unaweza ukakuta katika eneo fulani bomba la maji limepasuka, linatiririsha na kupoteza maji na kuna maeneo mengine watu wanahitaji maji hawayapati. Kwa mfano, kule Sinza kuna wakati unanunua dumu la maji Sh. 400/=, kwa mtu ambaye ana uwezo wake anaweza kununua, kwa wale ambao hawana uwezo linawashinda hilo, lakini wakati huo huo kuna maeneo mengine bomba la maji limepasuka, maji yanatiririka watu wanayaona wanakuwa hawana habari nayo. Kwa hiyo, nasisitiza kama tatizo limetokea haraka haraka lirekebishwe ili upotevu wa maji usitokee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ya mito yanayotiririka baharini wenzangu wamezungumza, tujitahidi tusiyakose yale maji, tuyafanyie utaratibu na tutafute teknolojia itakayotuwezesha kuyahifadhi yasimwagike baharini, maji tunayahitaji kwani wakati wa ukame maji yanakuwa hayapatikani na yale yanatiririka tu yanakwenda zake kumwagika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la *trans-boundary waters*. Mwaka juzi kulitokea tatizo baina ya nchi zinazotumia maji ya bonde la *Ziwa Victoria* ikawa vikao huku na huku, makelele na mgogoro ukaingia. Hivyo basi, tujitahidi kuheshimu yale makubaliano ambayo hizi nchi tofauti zimekubaliana, kama si hivyo tutapata migogoro baina ya nchi na nchi kwa maji ambayo yanatumika nchi zote. Uganda wenzetu walianza kupampu maji ya *Ziwa Victoria* yakaanza kupungua na vyanzo vya kuleta maji kwenye Ziwa vikawa vimeharibiwa. Kwa hiyo, maji yakaanza kupungua. Kwa hiyo, tukubaliane ile mikataba nchi zote husika iisimamie kama tulivyokubaliana, vinginevyo kutatokea migogoro baina ya nchi na nchi na kwa nchi jirani sio vizuri kuwa na migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine muhimu ni la utafiti. Tumesema maji ya mito na maziwa yanaweza yakapungua, yanaweza yakaondoka yasirudi tena, lakini tuna maji chini ya ardhi tuendelee kufanya utafiti wa kina kwa yaliyoko chini ya ardhi eneo kwa eneo. Tuangalie ubora wa maji, tufanye utafiti hali ya upatikanaji wake ili kuweza kuchimba visima mbalimbali na kusaidia wananchi wetu, maeneo mengine ni kame hawana maji. Kwa hiyo, katika umaskini wetu tujitahidi kufanya utafiti na kuchimba visima ili wananchi wetu waweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuwa na mpango mzuri wa kufundisha wataalamu wa maji ni muhimu sana hatuwezi tukaenda tu bila wataalamu. Wataalamu wanastaafu, wamebakia wachache hawatoshi kabisa, tunahitaji Wahandisi wa Maji, Madaktari wa Maji ili matibabu yaweze kufanyika vizuri na yaweze kupatikana ya kutosha yakiwa safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafi wa mazingira kwa maana ya muswada huu ni maji taka. Lakini usafi wa mazingira vilevile ni mambo ya ujenzi wa vyoo suala ambalo linasimamiwa na Wizara ya Afya. Kwa hiyo, Wizara ya Maji ishirikiane na Wizara ya Afya kwa tatizo hili kwa sababu kama watu hawajengi vyoo wanakwenda kujisaidia tu porini au milimani, ikija mvua uchafu wote ule unateremeshwa kwenye maji. Kwa hiyo, kuwa wajibu kabisa baina ya Wizara ya Maji na Wizara ya Afya kusimamia hili kwa sababu utafiti unaonyesha kwamba asilimia kubwa ya Watanzania hawana vyoo wanajisaidia kiholela popote pale, hili litaharibu mazingira ya maji na badala ya kuwa maji ni uhai inakuwa maji ni sumu. Mwenzangu mmoja alizungumza kuwa maji yanakuwa ni sumu kwa sababu yanasababisha maradhi ya matumbo na vipindupindu. Kwa hiyo, mshirikiane na Wizara ya Afya ili hili nalo la ujenzi wa vyoo liwe linatiliwa mkazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema kutakuwa na mfuko wa maji na vyanzo vyake vimetajwa kwenye sheria kuwa vianzio vya ndani lakini vilevile washirika wa maendeleo pia wataweka mkono wao kutusaidia. Hizi fedha zikipatikana zitumike vizuri kwa kazi ambazo zimepangiwa, hatutaki tena kupata *scandal* kwamba wamekuja waliotusaidia wanakuta badala ya fedha kutumika katika Sekta ya Maji zimekuwa *diverted* na zimetumika kwa mambo mengine ambayo sio hasa madhumuni ya kuundwa kwa mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ni mengi na nimekwenda haraka haraka lakini nasema lingine la muhimu ni kuwa na zile *master plans* za upatikanaji wa maji katika Wilaya na hata katika Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, kwa mchango mzuri sana na sasa namwita Mheshimiwa Kabwe Zubeir Zitto atafuatiwa na Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele na Mheshimiwa Pindi Hazara Chana ajiandae.

**MHE. KABWE ZUBERI ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Miswada hii miwili inayohusiana na jinsi gani ambavyo tunaendesha raslimali ya maji na jinsi gani ambavyo tunawezesha raslimali hii kuweza kuwafikia watu kwa matumizi ya binadamu lakini vilevile kuweza kufikia katika matumizi mbalimbali ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili nilikuwa napenda nieleze wazi kwamba tumekuwa tukijadiliana juu ya raslimali ya maji kama maji ya kunywa, kuoga labda kidogo na kufanya *irrigation* yaani kumwagilia. Lakini tayari taarifa mbalimbali za kiutafiti za Serikali na hasa taarifa ya hali ya umaskini nchini ya *latest* ya mwaka 2007 ilianza kufikiria kuonyesha ni jinsi gani ambavyo tutaifanya raslimali ya maji iweze kutumika kwa ajili ya maendeleo kama *enabler of growth,* yaani kama kichocheo cha ukuaji wa uchumi. Kwa hiyo, jinsi gani ambavyo tunamiliki raslimali za maji, ni kitu cha msingi sana katika kuhakikisha kwamba uchumi wetu unakua namna gani na matumizi ya maji yanakwenda namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa uchumi wetu katika upande wa maji unategemea sana maji ya mvua na hiyo inafahamika na imeelezwa sana na mfano dhahiri ni mwaka 2006 tulipopata tatizo la ukame sekta ya mazao iliporomoka kwa 20% kwa sababu ukuaji wa sekta ya mazao ulikuwa ni takribani 5% lakini kwa mwaka 2006 kufuatia ukame ikashuka mpaka 4%. Kwa hiyo, ilikuwa ni takriban 20% *drop* kwenye sekta ya mazao kwa sababu ya tatizo la ukame. Hivyo hiyo sekta ndogo ya umeme na maji iliporomoka kutoka ukuaji wa zaidi ya 8% mpaka kukua kwa asilimia hasi 2.5%. Kwa hiyo, inaonyesha dhahiri kwamba kwa kiasi kikubwa tunategemea sana maji ya mvua si tu katika masuala ya kilimo lakini vilevile katika shughuli nyingine ambazo zinahitaji mahitaji ya maji.

Kwa hiyo, nilitarajia kabisa kwamba Muswada huu wa matumizi ya raslimali ya maji *Water Resources Management Act* ungeweza kuwa ni Muswada ambao ungefanyiwa utafiti wa kina zaidi, ungefanyiwa *impact study* kwa sababu tayari tunakwenda kwenye juhudi za ku-*commoditise water* kuingiza maji katika soko wakati hivi sasa dunia nzima inaangalia ni jinsi gani ambavyo dola, yaani *State* inaweza ikabakia kwenye maeneo fulani fulani. Lakini hii Miswada miwili inanitia wasiwasi sana kwamba inatupeleka kwenda kwenye *neo liberalism,* yaani tunapeleka maji inakwenda kuwa *commodity* ambayo raia wataipata kutokana na uwezo wao wa kiuchumi, ndiyo wasiwasi

mkubwa kutokana na Miswada hii miwili ambayo iko hapa na bahati mbaya sana Miswada imekuja *under certificate of agency*.

Kwa hiyo, nje ya Serikali, Serikali inawezekana kabisa imefanya utafiti wa kina kwa sababu Miswada inakwenda kutekeleza sera ya maji ya mwaka 2002 na kuangalia mazingira ya sasa yaliyopo, lakini hakuna tofauti yoyote kati ya raslimali ya ardhi, madini, gesi na raslimali ya maji na ndiyo maana hapa pamoja na kwamba maji bado yanabaki kuwa ni ya umma chini ya Mheshimiwa Rais, lakini watu wataanza kupewa *water rights* kama jinsi ambavyo watu wanavyopewa *mineral rights,* kama jinsi ambavyo watu wanapewa hati za kumiliki ardhi. Sasa mfumo mzima wa jinsi ambavyo Muswada huu umekuja, yaani huu wa *Water Resources Management Act* unanitia mashaka sana na unanitia mashaka kwamba inawezekana kabisa tunasukumwa na watu ambao wanatusaidia maana yake nimesikia na sina uhakika na Waziri labda atatudhibitishia kwamba tumeambiwa tusipopitisha hizi Sheria msaada wa kibajeti kwenye sekta ya maji hautakuja.

Sasa tunakwenda kwenye matatizo makubwa kama nchi wakati mwingine ni lazima tuwe na uwezo wa kusema hapana. Muswada huu wa *Water Resources Act* pamoja na kwamba unaweza kuwa na madhumuni mazuri sana, lakini jinsi ambavyo umekuja unanitia mashaka sana na kwa maana hiyo mimi binafsi sitauunga mkono kwa sababu haujapata *impact study* ya kitaalamu ya kutuambia nini maana yake hivi; tuna move hapa kwenda huku; itakuta athari gani kwa sababu tunakwenda kuyaweka maji kwenye soko, kwa hiyo, nguvu ya soko ndiyo itakayo-*determine* nani anapata maji. Hilo ndiyo tatizo kubwa ambalo mimi naliona katika Muswada huu na ningependa kwa kweli Mheshimiwa Waziri na bahati nzuri yeye mwenyewe ni mtaalamu angeliambia Bunge na kawaida Miswada kama hii ya raslimali ingepaswa kuja na *summary* ya *impact study* nini maana yake kifedha, nini maana yake watu kupata hiyo huduma na kadhalika, lakini hakuna. Imenitia wasiwasi zaidi kwamba hata katika madhumuni ya Muswada hayaendani kabisa na *strategy* ya nchi ya kuifanya sekta ya maji kama sekta kichocheo kwa ajili ya ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitasoma upande ule wa *objects and reasons* wa Kingereza kwa sababu umeeleza lakini wa Kiswahili uko kimya. Unasema; "*The new act in terms to ensure that the nations water resources are protected, used, developed, concept, managed and controlled for basic human needs for the present and future generation*." Kwa hiyo, Muswada huu ni *for basic human need.* Yaani maji ya kunywa na kuoga, Muswada huu kwa *objects* hizi labda mpaka hapo Mheshimiwa Waziri atakapotufafanulia, haielezwi ni vipi ambavyo tunaweza na tukalinganisha mahitaji ambayo yanaingiliana ya maji kwa uzalishaji wa umeme inaendana vipi na *irrigation* na masuala mengine mbalimbali. Kwa hiyo, ningependa kupata hayo maelezo. Upande wa Kiswahili hapakuwa na hayo maelezo, sasa sijui ni kwa nini waliweka kwenye Kiingereza tu na labda Mheshimiwa Waziri anaweza kuwa na jibu zuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sisi ambao tunatoka kwenye maeneo yenye maji mengi kama Kigoma *basin* yetu ina vyanzo vingi sana vya maji na tunapopata Sheria ambazo zinaweza zikaingialia ile hali ya kawaida ya utamaduni wa kutumia maji, yaani

maji ya Ziwa Tanganyika au maji ya mto Lwiche au maji ya Malagarasi na kadhalika. Vilevile inaweza ikatufanya tukashindwa tukaondolewa ile *right* kwa sababu tayari hapa Bodi za Maji zinakuwa na nguvu sana, zile *water basis* za mabonde zinakuwa na nguvu sana tofauti na zile hali za kawaida za matumizi ya maji.

Kwa hiyo, mimi napenda nipate ufafanuzi na hasa wa kitaalamu ni vipi ambavyo sheria hii ya *Water Resources Management Act* inaweza isiathiri hali ya kiasili ya matumizi ya maji na nina wasiwasi sana kwa sababu sehemu kubwa ya Jimbo langu mimi linapakana na Ziwa Tanganyika isije kuwa leo watu wa Mwamgongo wakitaka kuchota maji ziwani kwa ajili matumizi lazima aende Kigoma mjini kupata *water right*, isijekuwa leo watu wa Zashe wakitaka maji lazima waende Kigoma mjini kupata *water right*.

Kwa hiyo, ningependa kupata maelezo ya kina kabisa ni jinsi gani ambavyo matumizi ya kiasili ya maji ya sisi watu ambao tunatoka kwenye maeneo ya maji mengi yanalindwa bila kuathiri masuala ya kisoko kwa sababu nina wasiwasi kwamba tuna *commodities* kama nilivyosema, majina, inaweza ikatuletea madhara makubwa sana huko baadaye na Muswada wenyewe umekuja *under certificate of agency*, ni vipi ambavyo umeelezea jinsi gani ya ku-*settle disputes* za matumizi ya maji hata miongoni mwa raia kwa raia wa na nimeona vyombo vingi sana vinaundwa katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la Muswada huu wa *Water Supply and Sanitation Act* kwa kiasi kikubwa inaweka taasisi jinsi gani ambavyo watu wanapata maji, jinsi gani ambavyo maji safi yataepukwa na maji machafu, jinsi gani ambavyo Mamlaka za maji zitafanya kazi zake. Sasa hivi tuna tatizo kubwa sana, kwa mfano Dar es Salaam kuna mgongano mkubwa sana kati ya *DAWASA* na *DAWASCO*.

Kimsingi mambo yale yale ambayo Kampuni ya *City Water* tuliyoifukuza ilisababisha ifukuze watu wa *DAWASA*, wanasema ndiyo hayo hayo ambayo yanatokea kwa *DAWASCO*, lakini vilevile *DAWASCO* inasema kwamba tatizo ni miundombinu mibovu na ni ya zamani sana. Ni 7% tu ya watu wa Dar es Salaam hivi sasa ambao wanapata huduma ya maji safi na nusu tu ya wakazi wa Dar es Salaam ndiyo wanaopata huduma ya maji safi na tumeambiwa na watu wa *Water Aid* kwamba gharama kwa mtu wa kawaida ambaye hajaunganishwa na maji gharama ya mtu wa kawaida ambaye hachoti maji yake kwenye mabomba anachota au ananunua kwenye madumu ni kubwa mara 15 ya mtu ambaye anapata maji yake kwenye bomba. Kwa maana hiyo ni kwamba mtu maskini analipa zaidi kwa ajili ya maji kuliko mtu mwenye pesa ambaye anaunganishiwa maji na *anyway* hawalipi maji na wakitaka kukatiwa maji na *DAWASCO* tunawalinda tunasema kwamba watu wasikatiwe maji na kadhalika, lakini inabidi kuangalia kwa kina sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kinachonitia wasiwasi ambacho ningependa nipate maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, tunaunda Mamlaka za Maji kwenye Wilaya, Wajumbe wa hizi Bodi wanateuliwa na Waziri wa Maji *of course* kwa kushirikiana na Waziri anayehusika na Serikali za Mitaa. Ma-*CO* wa hizo Bodi wanateuliwa na Waziri wa Maji, huyu Waziri wa Maji anakuwa *very powerful*, atakuwa

ni mtu mwenye Mamlaka makubwa sana, kuna Halmashauri za Wilaya, Miji na Manispaa nyingi sana katika nchi hii.

Kwa hiyo, mtu mmoja kuteua zaidi ya watu 2,000 inanitia mashaka sana kama kutakuwa na ufanisi. Kwa nini Mamlaka hizi za Maji katika ngazi za Halmashauri, Miji na Manispaa Bodi zile zisiteuliwe na Mabaraza ya Madiwani? Mabaraza ya Madiwani yateue Waziri abakie na jukumu la kuteua kutokana na ushindani kama ambavyo imeelezwa katika Muswada, wale Ma-*CO* yaani *Chief Executive Officers* kidogo hiyo inaweza kwanza ikawafanya hata wale watu wenye Mamlaka ya Maji wasijikute wanawajibika kwa mtu ambaye yuko Dar es Salaam, kama mtu wa Kigoma wajikute anawajibika kwa watu waliochaguliwa na wananchi pale pale Kigoma.

Lakini hii ya kulundika Mamlaka zote chini ya Waziri inatia mashaka sana, ninaomba eneo hili lijaribu kuangaliwa kuona ni jinsi gani ambavyo Mabaraza ya Madiwani yataweza ku-*play role* katika eneo hilo ili kupunguza Mamlaka ya mtu mmoja kuweza kuteua Bodi za Mamlaka za Maji katika Mikoa yote, Wilaya zote na miji yote maana yake Mamlaka za Serikali za Mitaa ni mpaka Mamlaka ya Mji mdogo kama mji mdogo wa Kibaigwa Waziri anakaa Dar es Salaam anateua Maji kwa mfano nimekuteua fulani bin fulani mjumbe wa Mamlaka ya Maji Kibaigwa, inawezekana hata mtu mwenyewe hamjui na hata ufanisi wake haufahamiki.

Kwa hiyo, naomba hili la uteuzi tulishushe liende kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa na wateua Madiwani hilo la *CO* linaweza likaangaliwa jinsi gani ya kufanywa ili Waziri pia aweze kuwa taarifa kwa mfano *CO* anaweza kuwa ameleta matatizo na kwa sababu anatumia fedha za umma aweze kuangalia ni jinsi gani atakavyoweza kumshughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la *water supply and sanitation act* ikifanyiwa marekebisho ya kuhakikisha kwamba *powers* zinakuwa kwa Mamlaka sina tatizo nalo, nitaliunga mkono. Hili la *Water Resources Management Act* nina wasiwasi nalo sana litatuingiza kwenye matatizo kama ambayo tunayapata kwenye Sekta ya Madini sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu katika muswada huu wa Sheria ya Usimamizi wa Raslimali za Maji ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Prof. Mark J. Mwandosya pamoja na Naibu Wake Mheshimiwa Christopher K. Chiza na Katibu Mkuu wa Wizara na Wataalamu wote kwa kuleta Muswada huu kwa wakati mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mjumbe wa Kamati hii ya Kilimo, Mifugo na Maji na kwa hiyo, tumepitia kwa kina sana Muswada huu lakini nina mchango wa jumla na kabla sijasahau kutoka mwanzo kabisa, naunga mkono hoja yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji aliyesema kwamba maji ni uhai na maji ni maisha na maji kwa kweli yanategemewa na viumbe mbalimbali akiwemo kiumbe mkubwa kabisa ambaye ni binadamu na ambaye ndiye anasimamia mambo yote hapa duniani kwa utashi na akili ambayo Mwenyezi Mungu ametupa. Lakini maji pia yanategemewa na mifugo, wanyamapori, mimea, mazingira, wadudu na viumbe mbalimbali, na kwa maana hii maji kwa kweli ni uhai na maji ni maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu pia ametupenda sana kwani ametupa maji ya mvua, ametupa maji juu ya ardhi kwenye mito, mabwawa na katika mabonde. Hayo ni maji ambayo yako juu ya ardhi. Lakini pia kuna maji chini ya ardhi lakini kwa jinsi ya maendeleo ya binadamu na teknolojia haya maji chini ya ardhi sasa pia tunaweza tukafika mahali tukayachimba na kuyatumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba raslimali ya maji kutokana na ongezeko la watu na mahitaji na matumizi makubwa ya maji, huko mbele ya safari maji yanaweza yakawa kinyang’anyiro kwa mataifa makubwa kutaka kuyang’anya mataifa madogo maji yao, ndugu yangu Mheshimiwa Rished Abdallah alizungumzia hilo leo asubuhi. Ndiyo maana Muswada huu sasa unaletwa ili kurekebisha mambo fulanifulani na tuwekeane sheria na mikataba ya kimataifa ambayo nchi yetu itakuwa inaridhia ili baadaye tusije tukaingiliana na kunyang’anyana yaani mkubwa kumnyang’anya mdogo.

Hilo linawezekana kwa sababu wakoloni walipora rasilimali za Bara la Afrika na kupeleka kujenga kwao lakini hata ukiangalia Marekani wameingia kule Iraq kwa sababu ya suala la rasilimali ya mafuta wakawaletea matatizo makubwa sana. Lakini sheria hii inafafanua mikataba hii ili pande zote zinazohusiana na mataifa yanayopakana na yanayaotumia maji shirikishi waweze kuingia katika mikataba hii na kukubaliana ili tuyatumie wote kwa heshima bila kuparuana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa maji kwa wananchi, mdau mkubwa kabisa ambaye anapaswa kufanya kazi hii ni Serikali kupeleka maji kwa wananchi, lakini vilevile sekta binafsi ina nafasi kubwa sana ya kupeleka maji kwa wananchi lakini hata watu binafsi pia na Sheria hii imekuwa shirikishi tofauti na Sheria iliyopita ambayo haikuwa shirikishi, wadau wote na watumiaji wa maji wanashirikishwa katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ni kubwa na siyo maeneo mengi ya nchi yetu yana maji ya kutosha, maeneo makubwa ya nchi yetu kwa kweli ni maeneo kame na ningependekeza mabwawa yachimbwe katika maeneo ya Jimbo langu la Ngorongoro; Kakeseo**,** Olbalbal, Malambo, Masusu, Arash, Piyaya, Esilalei, Ndutu na Bulati, haya ni maeneo ambayo ni kame sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mabwawa yakijengwa kwenye maeneo hayo, yatasaidia mifugo na mtawanyiko wa wanyama pori kwa sababu sisi tuko pamoja na wanyama pori katika hifadhi ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ipo haja pia ya kufufua miundombinu ya maji ambayo ilikuwepo zamani lakini baada ya miaka mingi ikaharibika, hakuna matengenezo na kwa hiyo miundombinu hiyo ikawa imekufa. Wakoloni kwa kweli walijitahidi sana kuweka Miundombinu katika maeneo yetu ya Ngorongoro lakini tangu wakati huo, hakuna ukarabati na miundombinu hiyo imekufa; ni bora sasa kwa kutumia Sheria hii miundombinu hiyo ifufuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna majosho ya kuogesha mifugo kule Soitsambu, Oloipiri, Endule na kadharika, haya nayo yanatakiwa yafufuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwangu kulikuwa na mradi wa maji unaotoka kijiji au kata ya Oldonyo Sambu kwenda Masusu. Mradi huu ulikuwa ni mradi mkubwa sana na Marehemu Edward M. Sokoine alifanya kazi kubwa sana akaweka huo mradi ni mradi mkubwa sana lakini makosa yaliyokuwa yametendeka ya utekelezaji, mradi huo kwa kweli haukuchukua muda, wananchi wakawa wameuhujumu mradi ule ukafa kwa sababu walivyoutengeneza ule mradi waliweka mabomba kwenye chanzo cha maji wakapeleka moja kwa moja kule walikokusudia kupeleka bila kuweka *DPs* ili wananchi waweze kuchota maji ya kunywa pale, waweze kutumia kwa matumizi mengine kama ya mifugo na kadhalika. kwa hiyo wananchi wa Oldonyo Sambu wakaona kwamba maji haya yanatoka kwao yanakwenda maeneo mengine bila wao kupewa namna ya kushiriki katika kutumia maji yale. Ni mradi mkubwa ambao ningeomba ufufuliwe kupitia miradi ya *Quick Wins,* Mradi wa *World Bank* ambao sasa nafikiri baadhi ya Wilaya zime *qualify* kupata kwa ajili ya kazi hii.

Lakini kwa upande wa mradiwa *Quick Wins* niipongeze sana Wizara kwa sababu ndiyo mradi ambao tunaona katika kutekeleza miradi, ndiyo fedha ambayo tumeweza kupata kwa haraka kidogo, ile ya World Bank mpaka leo tuna subiri ingawa tumetoa ahadi kwa wananchi kwamba Serikali inafanya jitihada na wafadhili watoe fedha hizo ili miradi hii iweze kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo kule hifadhi ya Ngorongoro kwa mambo ya *Environmental Impact Assessment*, lakini sheria hii pia imezungumzia suala la *Environmental Impact Assessment.* Ukiangalia ile Part Two ya sheria hii ukurasa wa 13 kifungu 9 naomba ninukuu: *"Any proposed development in water resource area or watershed to which this Act applies, whether that development is proposed by or is to be implemented by a person or organisation in the public or private sector shall carry our an Environmental Impact Assessment in accordance with the provisions of Environmental Management Act."* Kule Ngorongoro tuna sheria nyingine ambayo inasema "*any construction within the conservation area it must under go Environmental Impact Assessment*."

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naogopa sheria hizi mbili ambazo lazima *Environmental Impact Assessment* ifanyike itachukua muda mrefu sana sisi kutekelezewa miradi na hasa kwa sababu kuna shule ya sekondari ya Namokanoka na Ochalbali huu ni mwaka wa nane hatujapata kibali cha *NEMC* kujenga sekondari ile, sasa naogopa sana.

Hii sheria nayo ikiungana na hii ya Ngorongoro tutakuwa nyuma sana katika utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo nataka niliseme, nafurahi kwamba sheria hii inatambua watunzaji wa vyanzo vya maji. Kule kwangu kuna kabila moja wanaitwa Wabatemi au Wasonjo, ni wazuri mno katika kutunza vyanzo vya maji. Kule Kisangiro, Samunge, Digodigo wametunza vyanzo vya maji; ni watu wakali, hawataki mzaha na ndiyo maana kipindi kile Wamasai wanapambana na Wasomali, hiyo ni *corridor,* hawawezi kukanyanga kule kwa Wasonjo kwa sababu watapigwa mishale, lakini wanapita kwenye maeneo ya Wamasai kwa sababu ni ma-*gentleman* kidogo, wale watu hawapendi shari sana.

Ninafurahi kwamba sheria hii imewatambua wanaotunza vyanzo vya maji, tuwasaidie kwa kutumia sheria hii. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maji ambayo pia yanatumika katika Bonde la Ngorongoro kuna mito inapeleka maji huko, lakini kutokana na ujenzi mkubwa wa hoteli za Kitalii, maji mengi yanakwenda kwa ajili ya matumizi ya hoteli na ni kidogo sana yanakwenda kwa ajli ya matumizi ya wananchi wa pale pamoja na wanyamapori wanaoishi katika Bonde la Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii habari ya *water right,* tunawapa watu wachache matumizi makubwa ya maji na watu wengi wanaweza kukosa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kuna kitu tunaita *waterfall* katika kijiji cha Ngaresero inamilikiwa na jamaa mmoja anaitwa Kamakya, lakini *waterfall* inakwenda *Lake Natron,* inatumiwa na wananchi zaidi ya 4,000, kambi za kitalii, pamoja na *flamingo* waliopo *Lake Natron.* Lakini hii imeachiwa mtu mmoja. Lakini kwa kuwa sheria hii sasa inakuwa shirikishi mwananchi huyo tunaweza kumpa msukumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maji shirikishi ya Ziwa Victoria amekwisha zungumzia Makamu Mwenyekiti wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niishie hapo na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Telele ahsante sana. Ninamwita Mheshimiwa Pindi Chana atafuatiwa na Mheshimiwa Herbert James Mntangi na Mheshimiwa Paschal Degera ajiandae.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo, nami niweze kuchangia katika Miswada hii ambayo ipo miwili inayohusiana na Masuala ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwanza kwa kutoa pole kwa wenzetu ambao wamefariki miongoni mwa Waheshimiwa

Wabunge. Tulikuwa naye Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba na Mzee wetu Mheshimiwa Phares Kabuye, lakini vilevile niungane na Wanyalukolo wote wa Mkoa wa Iringa kwa kifo cha mke wa aliyekuwa Spika wa Jamhuri ya Muungano Chifu Mkwawa ambapo msiba huo unafanyika kule Kalenga. Mungu aziweke roho za Marehemu mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naipongeza Wizara kwa kuleta Miswada hii ambayo imerekebisha ile ya nyuma. Kadri siku zinavyozidi kwenda maendeleo yanakwenda kwa kasi na ni wakati wa utandawazi. Kwa hiyo, ipo haja kabisa ya kuboresha Miswada na Sheria zetu mbalimbali katika nchi yetu ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na Muswada unaohusu *Water Resource Management Act*, umeelezewa vizuri sana, niwapongeze wataalam wetu. Lakini tukienda pale eneo la tafsiri kifungu cha tatu wanapotafsiri mara nyingi wananukuu kifungu kwa mujibu wa kifungu cha 17, 22 pale kwenye tafsiri eneo la tatu. Kwa sababu sheria hizi zinasomwa na wakulima, wafanyakazi na watu wote ni muhimu sana wanaponukuu kifungu kingine kama kifungu cha 22 au 17, wasema kwamba kifungu cha 17 au 22 cha sheria hii, kwa mfano, eneo la kwanza wanapotoa tafsiri ya neno *"appellate authority"* wamesema kwa mujibu wa kifungu 107 cha Sheria hii. Sasa ni vyema huku chini wanaponukuu kama ilivyoelezwa katika kifungu 22 au 17 waseme cha sheria hii. Maana inaweza ikawa ni kifungu hicho cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano au cha sheria nyingine. Tuamini kwamba wanaosoma Sheria hizi sio Wanasheria, ni watu wa kada mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambasamba na hilo, tukienda kwenye tafsiri ya maneno kwa mfano, neno maji, pale ukurasa wa 10 na ukurasa wa 11 tafsiri ya neno watumiaji maji na vibali vya maji na *association* za maji, kuna hili neno ambalo limetumika mara nyingi sana, neno "au", ambalo Kiingereza chake wanasema "or*"*. Katika tafsiri ya neno *"water"*, maji neno *"or"* limetumika mara saba. Unapokwenda kwenye tafsiri ya neno "kazi", *work* neno *"o"r* limetumika mara nane.

Nilikuwa tu natafakari kama wanaweza wakatumia lugha nyingine nzuri maana yake unatafsiri kazi, maana yake hii na hii au hii na hii. Lakini lile neno au, *or, or* limetumika mara saba katika sentensi moja kutafsiri neno moja. Ningeomba wataalam wetu waliangalie. Kwa mfano, unapozungumza *work include canals, channels* unakwenda *for "or" connection,* unakwenda *or abstraction, or for protection, or any other, or for drainage, or for the use,* lile neno *"or"* limetumika mara nane, sehemu nyingine mara saba. Kwa hiyo, waangalie namna bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale pale kifungu 4(c) kuna neno *"promoting the efficient, sustainable and beneficial use of water in the public interest."* Mimi ninaomba kushauri badala ya kusema *in the public interest* tuseme *for public interest*, lakini wataalam wetu watatusaidia zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umekwenda vizuri sana, kifungu cha saba ukurasa wa 13, kinaeleza juu ya wajibu wa kutunza vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wajibu huu wa kutunza vyanzo vya maji umeelezea kwamba kila mtu atakuwa ana wajibu wa kutunza vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miswada hii mizuri maeneo mengi sana umezingatia mtu. Kwa mfano, mtu atakuwa na wajibu wa kutunza vyanzo vya maji, ukienda pale kifungu 43 cha Muswada huu kinaeleza mtu yeyote atakuwa na wajibu wa kufanya jambo fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunavyozidi kwenda na maendeleo, matumizi ya maji hayapo kwa mtu peke yake, Kampuni zinatumia maji, Taasisi zinatumia maji na Mashirika yanatumia maji. Sasa Muswada huu haujazingatia endapo makampuni katika matumizi ya maji imeghafilika ikavuka maji kinyume na taratibu; kampuni hiyo itachukuliwa hatua gani? Hata unapokwenda kwenye masuala ya *offences* imeeleza kwamba mtu yeyote atakayekuwa amekwenda kinyume na taratibu za Muswada huu atachukuliwa hatua moja, mbili, tatu, lakini haujatambua kwamba yanawezekana ikawa ni kampuni, yanawezakana likawa ni shirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi watumiaji wengi wakubwa wa maji sio tu *individuals, a person* yaani mtu, watu wengi wakubwa wa maji ni Mashirika. Yapo Mashirika yanayotegemea sana maji, kwa mfano, Mashirika yanayotengeneza bia, Mashirika yanayotengeneza vinywaji vya soda na kadhalika *Organization Body Corporate*. Kisheria zipo taratibu ambazo zinaweza zikachukuliwa kwa kampuni au Shirika wanaweza wakazuiwa leseni yao ya kufanya kazi wakatakiwa wakalipie fidia na kadhalika. Wataalam wetu wa sheria wanatambua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika kuupitia Muswada huu, maeneo mengi nimeona inazungumzia pale ambapo mtu anakwenda kinyume na taratibu na siyo Shirika au Kampuni. Nilidhani nitoe ushauri huo kwamba hayo ni maeneo ambayo ni vyema yangezingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niupongeze sana Muswada huu katika kifungu cha 4(1)(b) umezingatia kuhusu masuala ya maji safi na umeelezea wazi kwamba maji safi na salama ni haki ya msingi ya mwanadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji maji safi na salama katika nchi yetu, lakini ni jambo ambalo lazima tutafakari kwa pamoja kwamba tunafanyaje. Sasa hivi tuna idadi ya watu milioni 40, tuna shule nyingi sana za msingi na za sekondari ambazo kimsingi miundombinu ya maji bado hazijafikiwa. Sisi kama Taifa na kama wawakilishi, tunawajibika moja kwa moja kuhakikishia miundombinu hiyo ipo katika maeneo yao na sasa hivi katika nchi yetu tunatoa maji safi si salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya nchi wakati ninatembelea katika ziara zangu mbalimbali nimeshuhudia kabisa maeneo kwa mfano ya *Airport*, wale wanaofanya usafi,

anakwenda kwenye bomba anaposikia kiu anakinga maji anakunywa, maana yale maji ni safi na salama. Lakini maji yetu katika nchi ya Tanzania ni safi lakini sio salama, lazima uyachemshe. Katika Muswada huu au sheria hii tumeeleza kwamba endapo mtu atakwenda kinyume, kwa mfano, kuna miundombinu ya maji akavunja bomba atakuwa ametenda kosa. Lakini Wizara inawajibika kutoa maji safi na salama. Sasa kama Wizara au Taasisi hazijafanya wajibu wake tunafanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake mambo haya lazima yaende pande zote, mwananchi afanya wajibu wake na Taasisi zifanye wajibu wake. Naipongeza sana Wizara kwamba imezingatia masuala ya ushirikishwaji wa sekta binafsi na umma kwamba inawezekana kabisa kukawa na *ushirikiano* katika kutengeneza miundombinu ya maji au ugawaji wa maji na watu wakalipa bili ambayo itakuwa imepangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika misingi hiyo tunapoingiza sekta binafsi tusipoweka mikakati ya kumlinda huyu Mtanzania, ile sekta binafsi inaweza ikawa inafanya vitu kienyeji, lazima tuseme kwamba *water authority* zitakazokuwa zinatoa huduma ya maji ni vyema nazo zikazingatia taratibu, kanuni na sera ambazo zipo. Lakini ombi langu kwa Serikali ni kuzingatia yale maeneo ya Taasisi kama shule za msingi na za sekondari kwamba ni muhimu sana zikawekewa miundombinu ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwamba Muswada huu umezingatia pia masuala ya mabwawa. Bado lipo tatizo licha ya kwamba tunavyo vyanzo vingi sana vya kutosheleza kuwa na mabwawa, mabwawa ni machache sana ambayo tunayo. Tuna bwawa la Mindu na bwawa la Mtera. Lakini pia kwa mfano katika Mkoa wetu wa Iringa kuna eneo la Mto Ruaha, baadhi ya maeneo unapopandisha katika Mkoa wa Iringa kuna eneo linaitwa Ipongolo, tunaweza kabisa tukatengeneza mabwawa ya maji. Mheshimiwa Waziri wakati anatusomea taarifa yake alituambia kwa kweli Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo hazina maji ya kutosheleza, maji ni machache. Kwa hiyo, tunawajibu kutunza maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna ile sera *(re-cycling policy),* yapo maeneo wanatumia maji. Sasa yale maji yasiende moja kwa moja, baadhi ya maeneo wanaweza wakaya-*re-cycle* yale maji. Kwa mfano sio sawa na Mkoa kama Dar es Salaam ambako kuna bahari pale pale, bado baadhi ya maeneo ya Dar es Salaam hawapati maji kila siku, labda ni Jumatatu, Jumatano na Alhamisi. Hii kwa kweli ni changamo kubwa ambayo tungeomba sana taasisi ambazo zinashiriki katika masuala mazima ya maji watafakari na tuangalie kwamba tatizo ni nini kama miundombinu ipo? Maana yake hapo tunahitaji usambaji bora wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeomba sana tuzidi kufikiria kutunza maji ya mvua, lakini vile vile maeneo yale ambayo inawezekana kabisa kuweka mabwawa tuweke mabwawa. Ombi langu la kwanza ninaanzia na Mkoa wa Iringa eneo *the little* Ruaha lakini vile vile katika Wilaya ya Ludewa kuna maeneo mengi sana ambapo maji husimama na tunaweza tukayatunza kama tutashirikisha sekta binafsi, tutashirikisha sekta nyingine zozote na tunapokuwa na lile bwawa linaweza likasaidia umwagiliaji, uvuvi, kupendezesha mazingira na mambo mengine mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo eneo ambalo limeelezea masuala ya *Chief Executive Officer* kwamba awe *appointed* kwa muda wa miaka minne. Naomba kushauri kwamba awe *appointed* kwa muda wa miaka mitano kwa sababu akienda kinyume *appointing authority* ina haki ya ku-*hire* na ku-*fire*. Lakini vile vile pale kwenye *schedule* imeelezea kwamba kwenye *section* Waziri anaweza akavunja Bodi. Lakini *schedule* ile haijaelezea sababu ambazo zinaweza zikampelekea Waziri kuvunja Bodi. Sheria inataka Muswada huu ueleze ni sababu zipi zinazoweza zikampelekea Waziri kuvunja Bodi. Mamlaka hizo zipo lakini ni vyema sheria ikaelezea kwamba endapo kutakuwa na sababu moja, mbili, tatu, basi Waziri atakuwa na mamalaka ya kuvunja Bodi. Lakini pale *section* 4 inaelezea tu kwamba: "*The Minister may dissolve the National Water Board"* bila kuelezea kwamba ni kutokana na sababu zipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kwamba ushauri wangu utazingatiwa na baada ya kueleza hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa salamu za rambirambi zimekwishatolewa kwa niaba yetu, naomba tu kusema kwamba nawapa pole wale wote ambao wamefikwa na misiba. Lakini la pili nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili ni niweze kuchangia katika Miswada hii miwili ambayo kwangu naiona ni muhimu sana. Kitaifa nina hakika Miswada hii ni muhimu na ninawapongeza wale wote ambao wameshiriki katika kuhakikisha Miswada hii inakuja Bungeni hata katika mpango huu wa dharura, ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasilimali za maji ni nyingi sana, Watanzania wengi wanazifahamu, wanajua kwamba bahari ni sehemu ya rasilimali za maji, maziwa, mabwawa, mito, chemichemi, pamoja na visima hivi tunavyovichimba na kwa sababu kitaifa katika dunia tunafahamu kwamba kumekuwa na matatizo makubwa ya maji na ukweli unadhihirika kwamba hata hizi rasilimali zilizokuwepo za maji zinapungua mwaka hata mwaka, Kwa hiyo, upo umuhimu mkubwa sana wa kuzihifadhi rasilimali hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Muswada huu, upo utaratibu unaotuelekeza kwamba rasilimali hizi lazima zimilikiwe kwa maana ya kwamba lazima zitambulike, zipimwe rasmi na zitolewe hati ya kumiliki. Tunazo rasilimali nyingi sana katika Wilaya ya Muheza peke yake, utatushangaa sana kwamba tuna matatizo ya maji. Lakini tuna rasilimali na vyanzo vingi vya maji katika milima ya Magula, Kicheba, ambapo zinatoa maji katika mradi wa maji wa Mlingano, *Water scheme*, tuna Mto Zigi ambao ndiyo unaotoa maji ya uhakika kabisa kwa Jiji la Tanga; tuna chanzo cha maji cha Mlima wa Magoroto ambao ndio kinasaidia pamoja na kwamba ni kwa uhaba mkubwa kutoa maji katika Mji wa Muheza; tuna chanzo cha maji cha Ubembe Kwemuhusi ambacho chanzo hiki kimekwishajengwa, lakini mpaka sasa hivi hakijaanza kutumika. Ni rasilimali ipo ipo tu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunavyo vyanzo vingine vikubwa vya mto Derema kule Amani na hata huko huko Amani kuna vyanzo vingine ambavyo vingine

ambavyo vimeanza kutumika. Lakini vyanzo hivi ambavyo nimevitaja kwa uwingi wake katika Wilaya yetu ya Muheza havijapimwa wala havina hati miliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu tukiviachia vyanzo hivi bila kuvipima na kuvihifadhi, ni dhahiri kabisa vyanzo hivi vitavamiwa na wananchi. Kutakuwa na vurugu na hatimaye itachangia katika kuongeza upungufu wa rasilimali maji. Lazima tuchukue hatua za haraka katika kuhakikisha upimaji unafanyika na umiliki sahihi unafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika umiliki, ningependa kutoa ushauri ufuatao: kama ambavyo tumefanya katika ardhi kwamba tumekuwa wazi kabisa, tumesema ardhi ni mali ya umma. Hata tukipima ardhi na tukatoa hati, tunatoa hati kwa miaka maalum. Lakini kikubwa zaidi, tumesema kwamba Mheshimiwa Rais anayo madaraka ya mwisho ya kuweza kufuta hati za ardhi zilizotolewa. Tunapokuja kuanza kupima vyanzo vya maji na kuanza kuweka hati miliki tukumbuke mfano huu na utaratibu tuliojiwekea katika ardhi ili tuweze kuutumia vizuri pale tutakapoona upo ulazima kwamba hati imetolewa kama ni kwa mtu binafsi, sekta au shirika la umma, lakini uwepo utaratibu wa muda maalum, lakini na uwepo utaratibu unaomwezesha Mheshimiwa Rais kuzifuta hizo hati pale tutakapoona kwamba hazitumiwi vizuri na pale tutakapoona ipo haja ya kubadilisha matumizi ya rasilimali hizo. Kwa hiyo, tuwe makini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachonifurahisha zaidi katika mojawapo ya hii Miswada ni utaratibu wa kanuni za sheria zinazoelekeleza majukumu ya kazi kwa Waziri wa Maji. Mimi namwita Waziri wa Maji na Umwagiliaji maana ndiyo inavyoitwa hiyo Wizara yake. Lakini katika Muswada imeandikwa tu Waziri wa Maji, ninaridhika, naamini kweli ni Waziri wa Maji, lakini anayo sekta nyingine ya umwagiliaji, lakini majukumu kati yake na Waziri wa Serikali za Mitaa. Sasa ni kwa nini majukumu hayo yameainishwa vizuri ni kwa sababu moja kubwa. Moja hapa Bungeni tumeshawahi kusikia Waziri wa Ardhi akitoa maagizo kwa Halmashauri zetu zipime vyanzo vya maji. Suala la kujiuliza ni kwamba, hivi baada ya maagizo hayo, hivi kweli nchi nzima Halmashauri zote zimetekeleza? Sio rahisi! Halmashauri moja ambayo kwa kweli haijatekeleza ni ya Wilaya ya Muheza. Lakini najua zipo Halmashauri nyingine. Kwa hiyo, yapo maagizo yanatolewa kitaifa, tunadhani Wizara ya Ardhi ndiyo ina majukumu ya ardhi, lakini vyombo vingine vilivyopo hazitekelezi. Ukimfuata Mkurugenzi atakuambia mimi siitikii kwa Waziri wa Ardhi, naitikia kwa Waziri wa TAMISEMI. Sasa unaona hapo tofauti, matatizo hayo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri hapa limetokea jambo kama hilo, Waziri wa Maji anayo mamlaka juu ya maji. Lakini Waziri wa Maji hana mamlaka juu ya Mhandisi wa Maji kwa sababu Mhandisi wa maji katika Halmashauri ameajiriwa na Halmashauri. Kwa hiyo, Waziri wa Maji anaweza akasema tu na akatoa maagizo hapa, lakini hayatatekelezwa. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Maji, wiki chache zilizopita alikuwa katika safari yake ya kwenda katika Wilaya ya Handeni. Lakini aliona umuhimu wa kusimama Muheza ili aweze kutushauri Muheza namna ya kutumia vizuri fedha wanazotuletea za *quick wins* ili Muheza iweze kuondokana na matatizo ya maji. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa ushauri aliotupa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka nimhakikishie kwamba baada ya yeye kuondoka na ushauri mzuri ambao ungewezesha kupunguza matatizo ya maji pale, haukutekelezwa. Halmashauri wamepata fedha za *quick wins,* Waziri amekuja ametushauri na akatuambia fedha kwa ajili ya Muheza bado zipo mlete mahesabu ya kazi ya fedha tulizowaletea awamu ya kwanza na ya pili ili muweze kuomba awamu inayofuatia tuwaletee fedha kwa mpango wa pili mnaotaka kuutekeleza ili kuwapunguzia matatizo ya maji watu wa Muheza, hili halikutekelezwa. Mnaona matatizo! Hapa angekuwa ni Waziri anayesimamia Halmashauri, angemchukulia hatua yule Mhandisi au Halmashauri kwa jumla. Lakini kwa sababu ni Waziri wa Maji, hana mamlaka huko ya usimamizi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mhandisi wa Maji hakuyatekeleza. Muheza bado wanalia, bado hawana maji; kurudisha *returns* kwa hela walizopewa hawakurudisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya matatizo hayo, najua Mheshimiwa Waziri wa Maji hawezi kumchukulia hatua sisi katika Baraza la Madiwani wiki moja na nusu iliyopita baada ya kuona hilo aliloagiza Mheshimiwa Waziri wa Maji halitekelezwi, tulichukua hatua kama Baraza la Madiwani. Tumetoa azimio la kumkataa Mhandisi wa Maji kwa sababu hata haya maagizo aliyotoa Mheshimiwa Waziri na kutuhakikishia kwamba tungepata maji ambayo kwa Muswada huu yanatakiwa kugawiwa kwa usawa, halikutekelezwa. Licha ya idadi kubwa ya vyanzo vya maji nilivyovianisha hapa, watu wa Mji wa Muheza wanalia usiku kucha, mchana kutwa kwa matatizo ya maji. Licha ya kuwa na mhandisi mwenye uwezo mkubwa kama kweli alikuwa na uwezo mkubwa na *commitment* kwa wananchi wale tusingepata matatizo haya kwa sababu tuna vyanzo vizuri vya uhakika na vikubwa zaidi ya vitano. Mhandisi huyu kuwa na *degree* inatusaidia nini sisi watu wa Muheza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mhandisi huyu kukaa kwa miaka 20 ndani ya Halmashauri ya Muheza na *degree* anatusaidia nini? Rasilimali maji zipo na hakuna kazi inayofanyika. Kwa hiyo, nitamfahamisha Waziri wa TAMISEMI sasa uamuzi wa Baraza la Madiwani wa Wilaya ya Muheza kuhusu utendaji wa Mhandisi huyo. Kwa sababu tuna shida ya maji, lakini tutawezaje kuzipata fedha zilizoandaliwa kwa ajili ya mpango wa maji bila ya kurudisha *returns* ya fedha ambazo tulikwishaletewa awamu ya kwanza na ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nasema, Muswada huu ni mzuri sana. Nimeyatazama yale majukumu jinsi yalivyo katika Miswada hii miwili, lakini nataka niseme kwa ushauri wangu, haya niliyoyasema mkayasikia, yanaweza kufanya Waziri wa sekta muhimu kama ya maji hivyo hivyo chakula, hivyo hivyo ardhi, hivyo hivyo elimu wanaweza wakatoa maagizo hapa na maagizo yanaishia katika vyombo hivi tunavyosikilizia, hapa siyo vizuri. Lazima tuweke utaratibu utakaomwezesha Mheshimiwa Waziri wa Sekta aweze kutoa maelekezo na yakafuatwa. Kama ni lazima, basi amwagize Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI aandike na kuzipelekea Halmashauri zetu. Sasa huo ni mzunguko ambao kwa kweli *bureaucracy* kama hiyo haitasaidia Taifa hili katika kuongeza ufanisi wa kuwapa wananchi huduma wanazozihitaji.

Lazima tujiangalie vizuri, lazima tufanye marekebisho, lazima tuboreshe sheria zetu na kanuni zetu, Muswada huu unatuelekeza huko. Hata kama kweli umekuja kwa dharura na haukuchambuliwa, huu ndio mwanzo, halafu tutakwenda taratibu hatua kwa hatua tutafanya marekebisho. Mimi ninaamini kabisa kwamba Muswada huu ni muhimu kwa sababu Kitaifa lazima tukubali kwamba moja ya kipaumbele kikubwa kabisa na kama sio cha kwanza, basi cha pili ni maji. Kila unapokwenda nchi nzima kilio cha maji kipo, sijui wapi watu wameridhika kwa kupata maji. Sijui wenzangu kama wameridhika, lakini sehemu nyingine kila mahali unapokwenda tatizo la maji liko pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kuleta Miswada hii miwili na mimi naridhika kabisa kuiunga mkono kwa dhati kabisa yote miwili. Lakini nasema tuanze kuitumia tuangalie jinsi inavyotekelezeka tuangalie na kubuni utaratibu utakaowezesha kuboresha Miswada hii ili kweli Watanzania wapate maji, rasilimali za maji tulizokuwa nazo zilindwe na vyanzo vya maji tunaposema vipimwe, vipimwe kwa uhakika tuondoe migongano inayoweza kutokea kati ya wananchi wanaokaa karibu na maeneo ya vyanzo vya maji na wale ambao tunahitaji maji kwa ajili ya jumuiya za wananchi waliokuwa wengi na wenye shida ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo narudia tena kusema kwamba ninaunga mkono hoja hii. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kama ilivyo ada nianze kwa niaba ya wananchi wa Kasulu na hasa Jimbo la Mashariki kutoa pole kwa wanafamilia wote waliofiwa na ndugu na wapendwa wao akiwemo Marehemu Mheshimiwa Faustine Kabuzi Rwilomba, Marehemu Mheshimiwa Phares Kabuye na Marehemu mama yetu Mama Asha Adam Sapi Mkwawa. Mwenyezi Mungu awarehemu. Amen.

Lakini naomba pia kwa namna ya pekee niwapongeze sana uongozi wa Wizara, Mheshimiwa Waziri, Professa, Naibu Waziri Mheshimiwa Eng. Chiza, katibu Mkuu, Ndugu yangu Mkama, Naibu Katibu Mkuu na timu yake yote ya wanataaluma katika Wizara hii muhimu sana ya Maji ambayo kama wenzangu walivyosema kwa kweli maji ni uhai. Kabla sijachangia, nilikuwa naomba kwa namna ya pekee kabisa nimshukuru Waziri, Naibu Waziri na timu yake ya wataalamu wa Umwagiliaji Kanda ya Magharibi kwa kusimamia vizuri mradi mkubwa wa umwagiliaji katika kijiji cha Rungwe Mpya kilichopo katika Wilaya ya Kasulu na ambayo kwa kweli kwa Mkoa wa Kigoma ndio mradi mkubwa katika Mkoa mzima wa Kigoma na mradi mkubwa wa umwagiliaji tangu tumepata uhuru wa nchi hii. Kwa hiyo, Professa na Naibu Waziri hongereni sana na kwa kweli kupitia Bunge hili namshukuru sana Kiongozi wa Timu ya Wahandisi wa Umwagiliaji Kanda ya Magharibi Eng. Bayaga kwa kazi nzuri kwa kujituma, nina hakika kwa kuwa na fikra mpya na kuanza kubaini maeneo mapya yaliyojaa *potential* nyingi za kilimo katika nchi yetu, nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuunga mkono Miswada yote miwili, kwa kweli imekuja kwa wakati wake, mimi nimeisoma pamoja na kwamba ilikuja kwa haraka sana, lakini tumeipitia, tumeiona, tumeisoma imezingatia mambo makubwa

mawili. Kwanza, sera yenyewe ya maji ya mwaka 2002 na kubwa zaidi, tafsiri yangu ni kwamba Miswada hii ambayo hatimaye itakuwa sheria itakuwa pia ndio kichoteo mahsusi cha kuchota fedha za bajeti kuja kuhudumia miradi ya maji katika nchi yetu.

Mimi katika mchango wangu nitakuwa nazungumzia Miswada yenyewe hii, lakini na *interchangeable* na sekta yenyewe kwa sababu huwezi kuzungumzia maji bila ya kuzungumza sekta yenyewe. Ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, Miswada hii yote miwili inajikita katika utekelezaji wa Sera ya Maji ya mwaka 2002 ambao kwa kweli shabaha kubwa ni kumfikia kila Mtanzania ili kupata maji safi, maji yaliyokuwa salama lakini sio yaliyokuwa salama tu pia wakati wote maji safi, maji salama na kwa wakati wote. Hili limenivutia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajielekeza zaidi kwenye Muswada huu wa *Water Supply and Sanitation.* Nilikuwa naangalia pale *powers of the Minister* ukurasa wa 10 sehemu ya (3) inabainisha kipengele cha (d) juu ya Wizara na Waziri katika ku-*coordinate and to provide technical and financial support for construction of water supply and sanitation schemes and expansion or rehabilitation of existing schemes of national character of national importance.* Sasa hii itatuondolea ule utata ambao kila mara ilikuwa ni nijue Halmashauri zetu kupitia vyanzo mbalimbali kuhangaika. Sasa hapa jukumu la Wizara yenyewe limetamkwa kisheria kwa mujibu wa Muswada huu kwamba Wizara nayo itakuwa sasa na wajibu wa kusimamia miradi hii au *schemes* za namna hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba nizungumzie maji yetu ya Mto Malagarasi. Maji yetu ya Mto Malagarasi na Mheshimiwa Waziri nadhani unafahamu kwa sababu ulikuwa kwenye Wizara ya Mazingira, unajua Mto wetu Malagarasi ni Mto ambao unashirikisha nchi mbili, maji yanatoka Burundi na mengine yanatoka Tanzania lakini hatimaye sisi tulikuwa na bahati Mwenyezi Mungu akatupendelea zaidi huo Mto ukajielekeza katika nchi ya kwetu. Sasa iko miradi mingi ambayo imejikita katika eneo lile ningeomba sana kupitia sheria hii mpya Wizara isaidiane na sisi Halmashauri ya Kasulu ili kutumia vizuri rasilimali za Mto Malagarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jimbo la Kasulu Mashariki kuna vijiji 10 ambavyo haviko mbali sana na Mto Malagarasi, ni kama kilomita 10 tu kutoka kwenye Mto Malagarasi. Sasa nilikuwa naitazama sheria hii na *powers* za *Ministry* niki-*relate* na jinsi ambavyo sasa wakati umefika sheria hii na nguvu hii ya Waziri iweze kutusaidia sisi Halmashauri kuweza ku-*tap* yale maji ya Mto Malagarasi kuja kuhudumia vijiji katika Kata ya Midaho, Makele, Mvugwe, Nyarugusu, Herushingo, Kitagata kwa sababu maeneo hayo yako jirani sana na Mto Malagarasi. Nilisemee hili kwamba, mwaka jana nilitembelea Wizara ya Maji, kwa kweli Katibu Mkuu aliyekuwepo Ndugu Rutta amenipa ushirikiano mkubwa sana, akanipa wataalam kuutembelea Mto Malagarasi na hiyo ripoti ipo na ni matumaini yangu kwamba ripoti hiyo sasa tutaingia awamu ya pili ya *design* na ni matumaini yangu kwamba sasa Wizara mtatusaidia sisi Halmashauri ya Kasulu kuweza ku-*design* awamu hii ya pili ya mradi huu wa kutoa maji ya Mto Malagarasi na kuyaleta katika vijiji kama nilivyoeleza vya Makele, Herushingo, Nyarugusu, Mvugwe na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hayo kwa mujibu wa sheria hii, sasa naitazama kama haya maji ya Mto Malagarasi ambayo sasa tuna-*share* na nchi jirani nadhani chini ya sheria hii tutakuwa na nguvu zaidi Mheshimiwa Waziri kuweza kufanya hayo tunayotaka kuyafanya, tuna uhakika chini ya uongozi wa Wizara yako. Wale Wahandisi waliokuja Kasulu walishirikiana na Wahandisi wa Halmashauri ya Wilaya na kwa kweli wamefanya kazi nzuri na ni matumaini yangu kwamba Mheshimiwa Waziri awamu hii ya pili na kwa sheria hii mpya ambayo naitazama kama kichoteo cha fedha za bajeti ni matumaini yangu kwamba utatupa kipaumbele huko mbele ya safari kuweza ku-*design* mradi huu. Hilo lilikuwa la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nilikuwa najielekeza ukurasa wa 17 wa Muswada kifungu cha 20(b) kinachozungumzia juu ya usalama wa maji, alizungumzia habari ya *continues treatment of the water and monitoring of the quality of water*. Kifungu hiki nacho kimenivutia sana. Sisi pale Kasulu na Mheshimiwa Waziri unafahamu hili, sisi maji tunayo mengi lakini hayako salama na muda wowote tumekuwa tukiomba tupatiwe *treatment plant* ili maji yale ambayo sisi kwetu ni maji ya *gravity* yanashuka toka milimani kuja bondeni yaweze kuwa *treated* na hatimaye yaweze kusambazwa. Sasa chini ya sheria hii kama ilivyojibainisha ukurasa wa 17, ubora wa maji nao umezingatiwa na Mheshimiwa Waziri na timu yako niwaombe sana Mji wa Kasulu tunahitaji *treatment* ya maji. Maji sio maji tu, basi ubora wa maji na kuongeza mtandao wa usambazaji wa maji katika Mji wa Kasulu na viunga vyake. Niseme tu kwamba pale Kasulu sisi maji yetu ni ya *gravity* yako mengi na yanahitaji kupata *treatment* na nashukuru kwamba tayari wataalamu wameshakuja na matumaini yangu ni kwamba kwa sheria hizi mbili zitakuwa ni kichoteo cha fedha za bajeti ili kuweza kutekeleza mradi huu wa *treatment plant* pale Kasulu Mjini na usambazaji wa maji katika Mji wa Kasulu na viunga vyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haraka haraka nikumbushie hii miradi ya *World Bank* ya vile vijiji 10. Tunaisubiri kwa hamu sana na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu ni kati ya Wilaya ambazo zime-*qualify* lakini hatujapata fedha. Nimefuatilia kwamba wenzetu wameshapata na sasa nafikiri Mheshimiwa Waziri hebu sukumasukuma *machinery* yako tuweze kupata fedha hizo chini ya vile vijiji 10 chini ya Mpango wa *World Bank*. Tuna shida katika vijiji vilivyoko mbali kidogo na maeneo yenye maji kama Kijiji cha Nyumbigwa, Kasangezi, Kigogwe, Muzeze ni maeneo yenye shida kubwa sana ya maji, nina hakika maeneo hayo yanahitaji fedha. Niseme tena Mheshimiwa Waziri sisi tume-*qualify* kwa vigezo vyote vilivyokuwa vinahitajika, nafikiri sasa ni *machinery* ya Wizara yako iweze kutuma fedha hizo haraka iwezekanavyo ili miradi hiyo ya Nyumbigwa, Kasangezi, Kigogwe, Muzeze iweze kutekelezwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu naomba nijielekeza ukurasa wa 28 kwenye fedha *(source of funds).* Ukurasa wa 28 kifungu cha 36(d) kinaeleza pamoja na mambo mengine *source of funds* kinasema: "*Any moneys that the community organisations may obtain with the approval of the Minister responsible for local government from donation, loans and other financials assistance*". Kwa tafsiri yangu, nafikiri pale kuna kasoro. Kwa nini *donation* ihitaji *approval* ya Waziri wa TAMISEMI?

Sioni kama kuna hoja ya msingi hapa!  Nilikuwa naomba wataalamu waweze kulitazama hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchana nili-*consult* na Wanasheria tukawa tunashangaa pamoja kwamba hizi fedha hii *donation*, inaweza kuwa ni ya tajiri au Kanisa au Shirika lolote, kwa nini ihitaji *approval* ya Waziri?   Lakini kwenye *amendment* ukurasa wa nne, *clause* 37 inazungumzia juu ya fedha zinazotolewa na Serikali, lakini kipengele kile cha 36 kinazungumzia fedha ambazo ni *donations* kutoka kwa *donations loans and financials assistance*.  Ushauri wangu katika jambo hili nilikuwa nafikiri kile kipengele kingebadilishwa, isiwe lazima kwa mtu ambaye ana *donate* kwenye Mifuko ya Maji ya taasisi hizi ahitaji kibali cha Waziri wa *Local Government.* Kwa nini ahitaji kibali? Hivi kweli mtu anachangia maji huko Kasulu au Ngorongoro, kwa nini ahitaji kibali cha Waziri wa TAMISEMI?  Sioni mantiki *(logic)* kwa nini ahitaji kibali cha Waziri wakati yeye anasaidia na Makanisa yanasaidia.

Makanisa yanasaidia, Taasisi zinasaidia, matajiri wenye mapenzi mema wanasaidia, sasa sioni kile kipengele (d) kwa maoni yangu ningeomba Wanasheria mkitazame upya, naona kama hakipendezi sana na sioni kwa nini iwe lazima Kanisa linapotoa msaada wa mchango wa maji mpaka Waziri wa *Local Government* ajue. Kwa nini?

Lakini ukija kwenye uhitajio wa matumizi wa zile fedha, ukiangalia kwenye *amendment* ukurasa wa tano inazungumzia juu ya zile fedha za Serikali. Nafikiri hapa Wanasheria pia mngelitazama kwamba hata fedha zikiwa *donated* na Taasisi yoyote, basi iwe mtumiaji maji au *organization* yoyote ile iwajibike kuwa *accounted for,* nadhani ingejikita katika sheria ile itakuwa vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naunga mkono hoja hii na hoja nyingine iliyobaki.  Nashukuru sana.  *(Makofi)*

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:**  Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii leo na mimi niweze kuchangia Miswada miwili ambayo iko mbele yetu.  Kabla sijafanya hayo, naomba na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa niaba ya wapiga kura wa jimbo la Kondoa Kusini kutoa rambirambi na pole kwa familia, ndugu na jamaa wa aliyekuwa Mbunge wa Busanda Mheshimiwa Marehemu Faustine Rwilomba. Aidha, nitoe pia pole kwa familia za ndugu wa Marehemu Mheshimiwa Phares Kabuye na Mama Asha Adam Sapi Mkwawa, Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu pema Peponi.  Amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niungane na Wabunge wenzangu kutoa pongezi kwa maandalizi mazuri ya Miswada yote miwili.  Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara.  Maandalizi katika muda mfupi yamefanyika mazuri na ndio maana tuna Miswada hiyo miwili tunayochangia hapa Bungeni.  Kwa hiyo, nawapongeza sana kwa kazi nzuri ambayo imefanyika.  Baada ya maneno haya ya utangulizi sasa naomba nichangie maeneo machache ya Muswada na mimi nitajikita katika Muswada unaohusu

Sheria ya Huduma ya Maji na Mazingira ya mwaka 2009. Muswada ule mwingine sitakuwa na mchango mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia kifungu cha 16 cha Muswada huo. Kifungu hicho kimeweka utaratibu wa kukabidhi miradi ya maji kwa mamlaka mbalimbali zitakazoundwa na kinasisitiza kwamba miradi yote ambayo itakabidhiwa kutoka Serikalini kwenda kwenye mamlaka za maji zitakazoundwa miradi yote itatolewa bila fidia yoyote ama gharama yoyote. Kwa mara nyingine ni kwamba, mamlaka zile zitakazohusika zitapewa miradi hiyo ama zitakabidhiwa miradi hiyo bila kugharamia chochote, kwa maana nyingine ni bure. Lakini kuna kipengele kimoja ambacho kimewekwa katika kifungu hicho kinachosema, pia kukabidhi madeni ya miradi husika. Sasa nina wasiwasi hapa kwamba ukishakabidhi mradi na madeni yake, sina uhakika kama miradi hiyo itakuwa endelevu.

Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba pamoja kina kipengele cha pili ama kifungu kidogo cha pili kinasema kwamba endapo hayo madeni yatakuwa makubwa sana, basi Mheshimiwa Waziri mwenye mamlaka ya maji atawasiliana na Waziri wa Fedha ili aweze kuona namna ya kuweza kuondoa ama kuchukua madeni hayo na kuyalipa kupitia Wizara ya Fedha. Lakini kwangu naona kama hiyo haitoshelezi. Kwa mfano, kama Waziri wa Fedha hatakubaliana na ombi la Waziri wa Maji itakuwaje? Hofu yangu ndio iko hapo. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba badala ya kusema tunashauriana na Waziri wa Fedha, iwe moja kwa moja kwamba miradi hiyo inayokabidhiwa ikabidhiwe kwa mamlaka husika bila madeni. Kwa maneno mengine ni kwamba, napendekeza madeni yote yachukuliwe na Serikali na miradi ya maji inayokabiliwa kwenye mamlaka ikabidhiwe bila madeni ndilo ombi langu na naomba kipengele kile kifanyiwe marekebisho ili jambo hili likae vizuri kadri nilivyokuwa nimeelezea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia kipengele au kifungu cha 16, naomba sasa nihamie sehemu ya saba ya Muswada huu. Sehemu ya saba ya Muswada huu inazungumzia juu ya uundaji wa Jumuiya za watumia maji ama *water users associations.* Mlolongo wa taratibu zote umeelezwa katika sehemu hiyo na imeeleza kwamba Serikali aidha kupitia Halmashauri itasimamia uundaji wa Jumuiya za watumia maji kuanzia kutangaza nia ya kuweza kuunda Jumuiya za namna hiyo; pili, kusaidia kutengeneza Katiba; tatu, kuunda Bodi na mwisho kukabidhi mradi husika ambao umeundiwa Jumuiya. Kwa hiyo, utaratibu huo ni mzuri, lakini utekelezajii wake nina wasiwasi nao kwa sababu katika sheria hii, haijasema kwamba miradi yenye hali gani ndio inakabidhiwa. Nina wasiwasi kwamba isije zikaundwa Jumuiya na kukabidhiwa miradi ambayo haifanyi kazi na wasiwasi wangu unakuja kwa sababu tayari katika utekelezaji katika Wilaya yangu kitendo cha namna hii kimekwishafanyika na nataka nieleze hofu yangu kwa mfano huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mwaka 2006/2007 Wizara ya Maji kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa iliunda Jumuiya ya watumiaji maji wa mtaro wa Ntomoko. Bodi imeundwa na mradi umekabidhiwa lakini cha kusikitisha ni kwamba mradi haufanyi kazi. Ni kama vile Serikali umeutelekeza ule mradi wa wananchi. Sasa kwa kweli nasikitika kusema kwamba Serikali Kuu haikutenda haki kwa watu

wanaotumia mtaro wa Ntomoko kuukabidhi bila ya kuukarabati. Nafikiri ni aibu kubwa sana kwa Serikali.

Mimi naomba utaratibu huu usirudiwe wa miradi itakayokabidhiwa kwa watumiaji ya maji katika maeneo mengine na kwa upande wa Ntomoko dosari ama mapungufu hayo yaondolewe. Mradi huu ukarabatiwe, fedha zitolewe, tusiendelee kuwa na aibu ya namna hiyo, kukabidhi mradi ambao umekwishakufa kwa watumiaji wa vijiji 18 ambao sasa hivi hawana maji kwa sababu Serikali imezembea sana kukabidhi mradi ambao haufanyi kazi. Naomba sana Waziri na Serikali kwa ujumla ichukue hatua za haraka kurekebisha dosari hiyo, vinginevyo hii Miswada tunayotunga itakuwa haina maana. Kwa masikitiko makubwa, kwa kweli kwa niaba ya wapiga kura wangu natoa ombi hili kwamba dosari ama kosa hilo lililofanyika kwa kutelekeza mradi mkubwa kama huo bila kuukarabati naomba usirudiwe na naomba marekebisho yafanyike ili mradi huu uweze kuwa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nilitaka kuchangia ni kuhusu vyanzo vya mapato ya Jumuiya za watumia maji. Katika sehemu ya nane ya Muswada husika, utaratibu umeelezwa vyanzo gani vitatumika. Baadhi ya vyanzo naweza kuvitaja hapa, ni ada ya maji ambayo italipwa na watumiaji, kuna michango ya watumiaji wa maji na misaada ambayo inaweza kutolewa na mtu yoyote na michango ya Halmashauri pia. Hofu yangu ni kwamba, hizi Jumuiya hazitafanya kazi kama vyanzo ndio hivyo. Hazitafanya kazi kwa sababu mchango wa uhakika kabisa ni ule wa ada za maji, hii mingine yote ni misaada tu. Hivi unaweza kuendesha mradi kwa kutumia misaada? Lazima Serikali ama Wizara irejee tena kwenye Muswada huu na kuona kwamba ni vyanzo gani vya uhakika vitapatikana ili hizi Jumuiya ziweze kufanya kazi na kuweza kutoa huduma iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi wangu ni kwamba, kwanza vyanzo vyenyewe ni vichache; pili, havina uhakika wa mapato. Sasa kama una vyanzo vya namna hiyo, una uhakika gani kama miradi ya aina hii itakuwa endelevu? Ni kama vile tunataka kuwadanganya tu watumia maji ama Jumuiya hizo kwa kuitelekeza hiyo miradi na isiweze kufanikiwa. Ukweli wenyewe kama hatutaweza kuzingatia kuwapatia vyanzo vya mapato ya kutosha ya kuweza kufanya miradi hiyo iwe endelevu ni kwamba tutakuwa tumesababisha nchi nzima kukosa maji. Kwa hiyo, tuwe waangalifu na sheria kama kuna utaratibu wa kuongeza vyanzo, basi tuangalie vyanzo.

Mimi napendekeza kwamba lazima kuwe na bajeti kutoka Serikali Kuu kwa sababu kule unakosema pesa zitakazopatikana ni kidogo mno, kule kuchangia debe moja sijui Sh. 20/=, hiyo itachangia mradi gani? Unasema msaada wa Halmashauri, Halmashauri zenyewe ziko hoi, utatoa msaada gani kwenye bajeti ile? Halmashauri zote ama nyingi zinategemea fedha kutoka Serikali Kuu ama ruzuku. Sasa unawapachikia tena mzigo wa kuchangia miradi ya Jumuiya za watumiaji maji, sioni kama kuna kitu kitakachofanyika! Naomba sana Wizara iangalie suala hili ili angalau miradi yetu tunayoikabidhi kwenye Jumuiya za watumiaji maji iweze kuwa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka niliseme hapa ambalo kwa kweli imesababisha miradi ama huduma ya maji katika nchi yetu kwenda chini sana ni ule utekelezaji wa Sera ya Maji wa mwaka 2002. Sera ile imesisitiza kwamba miradi ya maji ya vijiji itasimamiwa na Kamati za Maji. Lakini uendeshaji wa vyanzo hivi vya maji hasa visima virefu ni ghali mno. Kwa sasa hivi Kamati zimeshindwa kabisa kumudu, kwa sababu vipuri vya mashine ni ghali mno ukilinganisha na mapato yanayotokana na kuuza maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hizi Kamati hazina mafundi na hawana wataalam wa kutengeneza mashine, wanategemea wataalam kutoka Wilayani. Sasa kinachotokea ni nini? Wale wataalam wanapokwenda wanadai kwanza kijiji kigharamie usafiri kwa maana ya gari, posho ya wataalam na huwa wanakwenda sio chini ya wataalam watatu. Kwa hiyo, wanadai posho na posho ya kijijini Sh. 35,000/= kwa kila mtu watakaa wiki nzima. Kwa hiyo, ile mifuko ya maji yote inakwenda kwenye posho na vipuri. Kwa mfano, Wilaya ya Kondoa tulikwishafikia kuwapatia wananchi wetu maji karibu asilimia 65, hivi ni asilimia 30 tu ndiyo wanaopata maji safi na salama. Miradi mingine imekufa kwa sababu ya utaratibu huu wa kamati za maji. Kwa hiyo, tuangalie namna tutakavyosaidia hizi Kamati za maji ziweze kuwa endelevu ama tuangalie namna ya kufufua halafu pia namna ya kusaidia kamati za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba Wilaya ya Kondoa ipatiwe Mhandisi wa Maji. Naunga mkono Muswada huu, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye hoja iliyoletwa mbele yetu. Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji Prof. Mark Mwandosya pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri Chiza, Katibu Mkuu na wataalam wote kwa kutuletea Miswada hii miwili ambayo tumeisubiri kwa muda mrefu. Niwapongeze sana kwa kutuletea Sheria hizi, moja ikiwa inahusu huduma za maji na usafi wa mazingira ambayo ndiyo hasa nitajikita na nyenzake inayohusu usimamizi wa rasilimali za maji nao ni wa mwaka huu. Nawapongeza sana na naanza kusema naunga mkono hoja hii iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kabisa katika suala la maji wananchi wa Kongwa wakiona hoja ya maji inazungumzwa hapa Bungeni mpaka inaisha Mbunge wa Kongwa hajasema chochote, watashindwa kunielewa. Kwa sababu katika vipaumbele vya shida mbalimbali za wananchi wa Kongwa cha kwanza ni maji. Ukifanya zoezi la *PRA* vijijini, kila kijijini unachokwenda ukawaambia hebu yapimeni kwa uzito matatizo mliyonayo halafu myapange la kwanza, la pili na yanayofuata, basi mahali pengi watakwambia maji ni tatizo la kwanza kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jinsi hiyo, nimesimama hapa kuishukuru sana Serikali kwamba mwaka 2002 tuliingizwa katika Wilaya 14 zilizofaidika na kupata mradi wa Benki ya Dunia. Kama nilivyosema, juzi mradi ule umetekelezwa, lakini kwa kweli haujaenda vizuri. Panahitajika juhudi mahususi kutoka Wizarani kushirikiana na TAMISEMI ili kuhakikisha kwamba miradi ile ambayo haijamalizika sawasawa

inakwisha sawasawa. Kule Mahutya na Leganga bado hakuna maji pamoja na fedha ya Benki ya Dunia tangu mwaka 2002 na wananchi wa kijiji cha Mahutya peke yake kuchangia milioni sita, Leganga karibu milioni saba, kwa Tanzania mwaka 2002 wengi wasingeweza kuchangia kiasi hicho na wote wengine Chamae, Manungu, Iduo, Hembahemba na Kiteto, hakuna maji, Kongwa mjini ni shida vilevile. Zile mashine nilizozisemea juzi kwenye swali ambazo huyo mkandarasi aliyezileta hizo mashine toka nje ya nchi alipewa kandarasi na Wizara. Mashine zile kote katika vijiji ninavyotaja hivi hazifanyi kazi na mpya kabisa, zimefungwa pale, ama haiwezi kupandisha maji kufikisha kwenye *tank* ama *nozzle* mbovu ama kitu fulani kibovu. Matatizo kibao!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio Kongwa peke yake, hata wenzetu wa Kondoa baadhi ya mashine hizi wamezikataa, baadhi ziko stoo mpya. Ni vizuri jambo hili Serikali ikafuatilia, kwanini mashine mpya za gharama kubwa lakini hakuna huduma kwa wananchi? Tulitazame kwa umakini jambo hili, ziangaliwe kama ni mitumba imepakwa rangi au nini. Halmashauri peke yake haiwezi jambo hili. Kwa hiyo, tunaomba Wizara itume wataalam wanaoelewa mambo haya ya mashine za maji, waje watazame na waseme ni nini kinachoendelea. Kama huyu mtu ametuletea mashine mbovu azitengeneze yeye kwanza maana ni mpya hazijatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii pale ambapo inakamilika; kwa mfano kijiji fulani, labda mradi wake ni milioni 200, kijiji fulani milioni 300 ukishakamilika kijiji kinakabidhiwa mradi ule, Serikali kwa namna moja au nyingine inajitoa inabakia Serikali ya kijiji. Hivi mradi wa milioni 300 Serikali ya kijiji inaweza ku-*maintain* kweli? Baada ya miaka minne au mitano wanakijiji hawa wataweza kweli! Kwa hiyo, tusipoangalia, baada ya miaka kadhaa miradi yote hii itakuwa *white elephants*, maana itakuwa ni vigumu sana wanakijiji kuweza kuihudumia peke yao. Kwa hiyo, naiomba Wizara wasiiache moja kwa moja, TAMISEMI wasiiache moja kwa moja miradi hiyo, vijiji viwajibike lakini waendelee kuilea vinginevyo wanakijiji hawataweza hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, alipokuwa anazungumza Mheshimiwa Degera, amesema Kondoa walikuwa wamefikia asilimia 65 ya huduma ya maji kwa Wilaya ile. Kuna wakati watu wa maji wamewahi kusema kwamba Kongwa imefikia asilimia 75. Hizi asilimia Mheshimiwa Waziri zisikudanganye kule Wizarani, nyingi ni asilimia bandia. Unakuta kijiji kina pepeo, kule kwangu Kongwa, wanakijiji wamekaa wanasubiri upepo; limekaa siku hiyo hakuna upepo na madumu yao wamekaa pale, hakuna maji. Lakini watu wa Idara ya Maji ya Wilaya wameweka tiki hapo kwamba hiyo ni asilimia fulani. Huduma ya maji. Mashine hizi mbovu ninazozungumza mradi wao walishaweka mashine siku moja wameshaweka tiki kwamba huduma ya maji tayari. Ni shida kubwa sana! ni vizuri asilimia hizi zikawa *realistic* hivi. Kweli huduma ya maji ni asilimia ngapi kwa wananchi wale? Tuiangalie sana hii. Mahali pengine maji ni machungu. Akina mama wanajua kwamba maji haya ukipikia maharage hayaivi. Kwa hiyo, Idara ya Maji ukisema umepeleka maji pale umehangaika tu. Maji mengine kufulia hayafai, kupika vitu vingine hayafai; sasa tusiseme tu maji halafu tukaweka tiki. Ni maji ya aina gani? Ni maji ambayo kweli wananchi wanayahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Zimbabwe kwenye kijiji fulani waliwahi kwenda wazungu fulani wakakaa na wanakijiji, wakasema nyie mna shida ya maji kwa sababu mnachota maji kama kilomita mbili kwenye korongo ambalo wakati wa kiangazi wanachimba mchanga halafu maji yakijaa kidogo ndiyo wanachota. Wazungu wale wakatoa msaada wa mashine ya maji kilomita moja na mtoni ilikuwa kilomita mbili. Wakatengeneza Kamati ya maji baada ya maji waliporudi wakakuta ile mashine ambayo wamewawekea wale wananchi hakuna hata anayechota yale maji kwa sababu maji yale yalikuwa machungu, bado wakina mama na madumu yao wanakwenda mtoni kule kule, wanafukua fukua na kutumia kwa matumizi ya nyumbani na ile mashine ni *white elephant*. Wale wafadhili walishaweka tiki kwamba pale huduma ya maji tayari. Kwa hiyo, ndiyo nilikuwa nazungumzia mtego kama huu Wizara isiingie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sheria hii ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2009 kuna maeneo ambayo yanazungumziwa kuhusu uundwaji wa miradi ya kijamii. Mradi wa Maji Kijijini ni Mradi wa Kijamii. Mradi wa maji kama pale kwangu Kibaigwa, Mji mdogo ni mradi wa kijamii. Tuna Bodi pale.

Sasa angalizo ambalo napenda kulitoa hapa ni kwamba tuwe makini kwa sababu kuna ile jamii ina mradi wao halafu kuna watu wanaitwa waendeshaji hujitokeza. Wanakijiji wanaingia Mkataba na mwendeshaji, mikataba hii, Sheria hii iseme ni marufuku kwa mradi wa jamii kuingia mkataba na mwendeshaji bila mkataba huo kuwa umeangaliwa angalau na Halmashauri ya Wilaya husika. Kwa sababu angalau pale tuna uhakika wataalam wa maji wako pale. Kwa sababu mikataba ambayo wanaingia kati ya waendeshaji hao na jamii mingi inaumiza jamii. Wasiweke sahihi mkataba bila kuwa umetazamwa vizuri na kwa miji midogo mkataba huo ikiwezekana Wizara ya Maji muuone kabla ya kukubaliwa mradi huo uweze kuendeshwa na Mwendeshaji kupitia Halmashauri ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya mapato ya miradi ya jamii yaeleweke vizuri, itakiwe kabisa katika Sheria masuala ya matumizi yao: Je, utaratibu wa matumizi ya hela za umma au wakishakua Kamati pale wanatumia tu, kama wanavyotaka wao? Wana mwongozo wowote wa matumizi ya fedha? Tumeona mahali kadhaa matumizi yanakuwa ya hovyo tu. Ufungaji wa vitabu vya mahesabu upo? Tuwatake mambo haya yafanyike, ukaguzi wa hesabu. Sisi tuna Bodi ya Maji pale Kibaigwa sikumbuki imewahi kukaguliwa mwaka gani na ni mahali ambapo miradi ya maji inaingiza fedha nyingi sana kwa mwaka mmoja na kama imewahi kukaguliwa, hesabu zilizokaguliwa za mradi ule nani amewahi kuziona?

Mambo haya yatizamwe na mahesabu yakishakaguliwa ripoti wapewe wananchi ambao ndiyo wajumbe wa mradi huo lakini vilevile Halmashauri ya Wilaya ipewe nakala. Litakuwa ni jambo la maana sana, ili lijadiliwe katika vikao vya Halmashauri, wawaone wanakwenda vizuri au wanahitaji msaada fulani. Kwa sababu ni kikundi cha kijamii Afisa Ushirika anaweza kukagua, Mkaguzi wa Ndani wa Halmashauri anaweza kukagua hesabu hizi. Miradi ya maji inaingiza fedha nyingi ni vizuri ikaangaliwa vizuri na ikisimamiwa vizuri inaweza kabisa kujiendesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miradi hii ya kijamii wasiruhusiwe kabisa wale wanaoendesha ile miradi kupanga bei ya maji. Wakipanga bei ya maji watapanga vitu vya ajabu tutaumiza watu wetu. Maji ni uhai na wakitaka kubadilisha bei ya maji iwekwe katika Sheria na nadhani sijapata *amendments.* Nadhani Mheshimiwa Waziri atakuwa ameshaikubali wawatake katika kikao angalau cha Halmashauri kwa miji mikubwa Halmashauri, Makao makuu ya Wilaya ni vizuri wakitaka kubadili bei ya maji walete kwako Mheshimiwa Waziri, maji ni uhai, maji ni siasa. Hawawezi watu wakajipangia tu bei za ajabu ajabu. Itaumiza wananchi wetu itaiweka Serikali yetu mahali ambapo hatuhitaji kuwepo. Kwa hiyo, jambo hili ningependa kabisa Sheria iliweke vizuri watu wasijipandishie bei za maji bila ya kuwa Serikali inajua kwa hatua fulani nini kinataka kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi za Maji kama ile ya Kibaigwa na nyingine Sheria isema, uwajibikaji wake ukoje. Hii habari ya kusema chombo cha wananchi halafu kiko huru; ndiyo, lakini uhuru wowote una mipaka. Uwe huru kuendesha mambo yenu, lakini lazima muwajibike kwa kutoa taarifa sehemu moja, mbili, tatu. Wale wanajifanyia mambo yao wenyewe, peke yao. Pakiwa hakuna maji pale Kibaigwa ni tatizo la *DC,* ni tatizo la Mbunge, ni tatizo la Halmashauri. Lakini taarifa hazitoki, hesabu hazijulikani ziliko, ni jambo ambalo lazima tulirekebishe katika Sheria hii. Watakapokuwa wanaomba kuandikishwa upya ni vizuri kabisa uwazi uwepo kwa taarifa kufika katika vyombo vya Serikali kusudi kujua maana huwezi kuwa na mji mdogo huduma yake ya maji inaendeshwa na kikundi fulani halafu haieleweki mule ndani hasa ni nini ambacho kinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, salamu za wananchi wa Kibaigwa kwa Mheshimiwa Waziri, ni kwamba zitakapoandikishwa Bodi mpya, paangalieni sana pale Kibaigwa namna gani mambo yake yataendeshwa. Kongwa haina shida kwa sababu Bodi yake ni ile ya Serikali ambayo inaundwa kwa utaratibu wa kiserikali ambapo Waziri wa Maji anamteua Mwenyekiti na wajumbe wanapendekezwa na Halmashauri ya Wilaya. Mwisho, katika Sheria hii kuna *codes of workmanship.* Naunga mkono jambo hili kuwabana wakandarasi wote, kuwabana wahandisi, wasanifu ambao kwa kule Kongwa miradi imejengwa hovyo kwa sababu ya matatizo ya wasanifu, wahandisi na wanaoendana nao. Ni vizuri sasa Sheria hii inaongelea habari ya ubora wa kazi ili watu hawa wawajibishwe. Akiharibu Kongwa asiende mahali pengine na kwa miradi mingi ya maji ilivyo, kampuni moja inapewa Kongwa, Mpanda, Mtwara, inapewa Musoma kampuni moja, matokeo yake inaharibu kila mahali. Tuweze kuwajua ni akina nani na wadhibitiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo, napenda kusema kwamba naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii na mimi nianze kwa kutoa rambirambi kwa niaba ya wananchi wa Ludewa kwa vifo vilivyotokea hapa karibuni, tunawapa wafiwa wote pole sana. Pili, niwapongeze sana Waziri na Naibu Waziri na wataalam wote kwenye Wizara hii kwa mawasilisho haya mazuri sana. Nasema ni mazuri sana kwa vile Miswada hii

naielewa vizuri na imeletwa vizuri kwa wakati wake na sikushangaa kwa sababu namwamini sana na kumthamini Prof. Mwandosya na Naibu wake kwamba kwenye Wizara hii wanaweza. Kwa hiyo, ninakuwa na imani kwamba Muswada wa namna hii unapoletwa na watu hawa unakuwa umeangaliwa na umezingatiwa na ni wa makini sana. Kwa hiyo, nilitegemea na kwa kweli nimesema ni Miswada miwili mizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita kwenye Muswada mmoja tu wa *Water Resources Management* na nitakwenda kwa *clauses* ili wenzangu wanipate vizuri kwenye mambo machache ambayo nilitaka kuchangia. Kwenye *clause* ya sita 2(b) nilikuwa naomba wa-*substitute* neno *reserve*. Mimi naona wasitumie neno "*reserve"* badala yake watumie "*conservation*," kwenye kile kipengele na sidhani neno *reserve it makes sense,* badala yake tuzungumzie *environmental conservation rather than environmental reserve.* Kwenye *clause* ya nane, wamezungumzia kuhusu *strategic environmental assessment* ifanyike kwenye *project* ya maji. Nataka kusema kwamba *strategic environmental assessment* inafanywa kwenye *programs* na sio kwenye *project*. Kama tunataka kuzungumzia *strategic environmental assessment,* basi tuzungumzie *water programs*, kama ile ya Chalinze *is not a project* ile ni *program*. Kama tunazungumzia *strategic environmental assessment* ile ni *program* na sio *project*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *clause* ya 12 (2) naomba *water harvesting works* zozote zile zizingatie *environmental impact assessment* hata kama ni ndogo lakini kwa sababu tuna *deal* na *water resource* ni vema tukathibitishiwa kwa kufanya *environmental impact assessmen.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *clause* ya 22, kuhusu *Basin Water Boards;* naomba kusema kwamba mimi ni Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Uendelezaji wa Bonde la Mto Rufiji. Sasa hizi *Basin Water Boards* zinazungumziwa kwa ujumla naamini pamoja na Bonde la Mto Rufiji, najua kuna *Water Basin Board* tayari lakini nataka kusema Muswada huu unapuuza kwamba kwenye Bonde lile kuna *Rufiji Basin Development Authority* ambayo ina majukumu ya kusimamia matumizi ya maji *among other things*, kwa mfano ku-*regulate*, kuzingatia matumizi mabaya na mazuri, kujua kuna maji kiasi gani kwa ajili ya miradi mbalimbali. Sasa haizungumzii uhusiano wa *Water Boards* na *Rufiji Basin Development Authority*. Inaelekea kwamba, *RUBADA* haina kazi na badala yake ni *New Water Board* ndiyo itakuwa inafanya kazi. Nafasi ya *RUBADA* iko wapi hapa? Nitapenda kupata ufafanuzi wakati Mheshimiwa Waziri anafanya majumuisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *Clause* 31 nakubaliana na wazo la kuwa na *integrated management plans* ambalo linahusisha suala la *water balance*; nadhani wana maana vile vile *water budget*. Ni suala zuri sana lakini niseme tu kwamba, wazo hili ni *over ambitious*. Nadhani tunategemea mambo makubwa sana kwenye hii, lakini hayatawezekena. Kwa sababu *demands* za kwenye *water basin* kwenye Bonde *demands* zinabadilika *overtime*. Unaweza ukaja na *plan* ya wakati fulani lakini *after five years, demands* za maji zimebadilika kutokana na miradi inayoendeshwa au inataka kuanzishwa kwenye maeneo hayo. Sasa najua huko mbele wanazungumzia kwamba watakuwa wana-*review all the time*.

Lakini niseme kwamba ni *ambitious* kwa maana ya kwamba ni kazi kwelikweli kuhakikisha kwamba *management* plan inayokuwa *recommended* kwa *catchments* basin inaweza kuwa endelevu, ama ikafanya kazi. Nitaomba maelezo kama wanadhani kweli itafanyakazi. Lakini vilevile tunapozungumzia kwenye *supply side* nayo inabadilika kila wakati kwa sababu *climate change* ipo, kwa hiyo, maji yana-*shrink* kwenye mito. Sasa unapotaka ku-*determine* una maji kiasi gani ni kazi ngumu sana. Lakini vilevile suala la ku-*monitor* kupima, kupata *data* ni *very expensive* kama kila *catchments* basin, mito mikubwa, mabonde makubwa na madogo yote yatafanyiwa *integrated water resources management plan* namna ya kupata *data* na *statistics* zile ni gharama kweli kweli. Nataka nielezwe wana uhakika gani kwamba haya yataweza kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *clause* ya 34 kuna suala la ku-*prohibit* kuzuia matumizi, *human activities beyond sixty metres* za *water source, among other things*. Nilitaka kusema tu kwamba *I hope* kumekuwa na mawasiliano mazuri na Idara au Sekta nyingine kwa mfano upande wa kilimo na upande wa mazingira kwamba *we are beyond sixty metres*, wote tumekubaliana, maana kulikuwa na mtafaruku kwamba kila sekta wanazungumzia *statistic* tofuati. Sasa kama wote mmekubaliana ni vyema. Lakini vilevile tatizo langu ni *designation* ya *water source*. *I have always asked water sources* maana yake ni nini? Kwa hiyo, ninaposema *sixty metres* kwa mfano kwenye chemchem kubwa, sasa *sixty metres from where?* Kwa hiyo, nitaomba nifafanuliwe hapa wana maana gani utakaposema *water source* kwenye chemchemi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *clause* ya 35(2), kuna uwezekano kuwa na *cancellation or reduction of permits* kama kuna ukame kwa mfano. Lakini pamoja na kuwa itakuwa *by proportionalities* kwamba *permits* zile zi-*allow* kuchukua maji kila shirika kila Kampuni kiasi fulani. Kwa hiyo, tunasema kwamba tukiwa na ukame tutapunguza *permits* zile *proportionately*. Nataka kusema kwamba pamoja na kuwa na *proportional reduction au cancellation* tuzingatie suala la umuhimu wa *demand*, kwa mfano *public water utilization* ni *more important* katika mazingira kama hayo kuliko maji kwa ajili ya *irrigation farming*. Kwa hiyo, huwezi ukasema kwamba permits zitapunguzwa *proportionately* tu, lakini lazima kuwe na vipaumbele. Maeneo yale ni lazima yapate maji na yale ambayo si lazima sana katika mazingira kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *clause* ya 37 na 38 nasema ni wazo zuri sana kuzungumzia mambo ya *po* asilimia mia moja na hasa kwenye maeneo ya ukame. Ni wazo zuri sana. Kwenye *clause* ya 54 ningependa *ground water permits* zipewe *as a last resorts*. Mimi naamini *ground water* ni *storage*. Tunahitaji kwanza kutumia tunapokuwa tuna-*exhaust surface water*. Tukianza *hazardly* ku-*extract ground water sources* tunajiletea matatizo sana. S*o I hope* tutazingatia hilo kwamba ni *last resort unless* tumemaliza, tume-*exhaust surface water*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *clause 63*, ni vema *to state minimum level/amount of discharge. To state exactly* ni *level* gani itaonekana kama ni *minimum* ili kuruhusu *discharge* ya *waste*. Usisahau katika mazingira fulani *small discharges cumulatively* zinakuwa na *major impact*. Kwa hiyo, ni vyema tuka-*state* tukawa na uhakika kwamba

*level* fulani ya *discharge* haitakuwa na *significant implication* kwenye *environment*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *clause* 98, 99 na 100 nashukuru ziko kwenye *Act* hii na nadhani hapa sasa Wizara hii inakuwa na nguvu sana kwenye mradi wa magadi kule *Ziwa Natron*. Kwa sababu hii ni *trans boundary resource* na hapa tumejiwekea kwenye sheria hii kwamba Wizara hii itakuwa na nguvu sana katika maamuzi ya matumizi ya maji kwenye *Lake Natron*. Nitaomba kujua kama hivi ndivyo.

Lakini ya mwisho kasoro moja; nakubaliana na hoja aliyoitoa Mheshimiwa wa upande wa upinzani Mheshimiwa Mbunge wa Kigoma, kwamba Muswada huu unaelekea haukufanyiwa *regulatory impact assessment*. Ni nyeti sana na nilitegemea kwamba ungeletwa na *EIA implication* zake. Lakini nakubaliana na hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ingawa napenda kupata maelezo kwanini hakuna *Regulatory Impact Assessment* iliyoambatanishwa na Muswada huu? Lakini kama kutakuwa na maelezo, *I have no problem* nitaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, napenda kutumia nafasi hii kuishukuru Wizara na Mawaziri hawa. Ludewa tumepata miradi ya umwagiliaji miwili, tumeshapata fedha za mwanzo Manda na Lifua. Tunashukuru sana na tunategemea kwenye bajeti ijayo kutakuwa na fedha za kutosha kwa ajili ya miradi ile miwili. Lakini vilevile nashukuru kwa fedha inayotolewa na itaendelea kutolewa kwa ajili ya maji kwa ajili ya mji wa Ludewa. Ahsante sana na naunga mkono hoja zote mbili. *(Makofi)*

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia. Awali ya yote, napenda na niungane na wenzangu kwa kutoa rambirambi kwa ndugu na jamaa waliofiwa kwa sababu kiti kimeishatoa rambirambi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye Muswada huu, napenda niseme kwamba Muswada huu kuna maeneo ambayo yamegusa na ni ya wakati wake hasa kuleta Muswada huu. Lakini kuna maeneo ambayo nafikiri wangekuja kwanza wakatupa na tathmini waliyoifanya ya kutuelekeza ni vipi wamefikia kuweza kuleta baadhi ya sheria kwa wananchi, kwa sababu sote tunajua maji ni uhai na tunajua maji ni muhimu. Napenda tu nikumbushe kwamba watumiaji wakubwa wa maji katika jamii ni wanawake. Sasa katika Muswada huu sikuona mahali popote ambapo pamesisitiza umuhimu wa maji haya na sheria hii kwa jinsi gani itamlinda mwanamke katika matumizi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwenye suala la hifadhi ya maji, wanazungumzia kwamba kule kutakakokuwa kumetengwa kwa ajili ya maji, wanaposema kilomita 60, kama alivyosema msemaji aliyepita, kuanzia wapi kuelekea wapi? Kuna wale ambao wanaendesha maisha yao kwa kilimo cha mboga mboga, kuna akina mama ambao wanategemea kupata maji kutoka maeneo hayo. Sasa maeneo yale, kwa mfano; yatawekewa uzio, yametengwa na lazima mtu apate kibali kuingia kuchota maji kule ndani, hawa wakulima wa mboga mboga, hawa akina mama watakuwa na

*access* ipi ya kupita kuweza kwenda kupata maji na hawana kibali cha kusema wataruhusiwa kuchimba maji yaliyokuwepo ardhini. Sijui katika Muswada huu kipengele hiki wanakiangaliaje.

Ninaomba nipate ufafanuzi wa jinsi gani watu ambao watakuwa wamezuiwa wasiingie kuchota maji na wakawa na shida ya maji na sisi sote tunajua kwamba nchi yetu tunapata maji kwa msimu na tunategemea sana maji ya mvua, sasa ni vipi tutaweza kuwasaidia na wakati huo huo tunawaambia watu walime mboga mboga ili waepukane na kwashakoo na maradhi mengine ambayo yanatokana na kukosa vitamini A. Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri hilo waliangalie kwa makini na waweze kutusaidia tutalifanyaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwa wachimbaji wadogo wadogo. Wachimbaji wadogo wadogo halikadhalika na wakulima wengi wao, nikianza na wachimbaji wadogo wadogo, wanatumia madini ya aina mbalimbali. Madini haya wanapotumia lazima watumie maji. Kuna wengine wana maji ya kutosha na wengine hawana maji ya kutosha.

Lakini kwa wale wenye maji ya kutosha, maji yale yenye madini na kemikali mbalimbali yanatiririka yanakwenda kwenye vyanzo vya maji au yanakwenda kwenye mito ya maji au mabwawa. Wananchi wanatumia pamoja na mifugo maji hayo hayo. Ni vipi Muswada huu utaweza kuwalinda wananchi wale au mifugo ile itakapotumia maji yale, japokuwa madhara yake hayataonekana kwa siku zile zile za karibuni?

Madhara ya maji yale yataonekana baada ya miaka, lakini hapo tutakuwa tumepoteza nguvu kazi, tumepoteza watoto wetu na jamii kwa ujumla. Je, Mheshimiwa Waziri, katika Muswada huu kuna kipengele chochote ambacho atakiweka ili kutulinda sisi jamii ambayo iko karibu na hivyo vyanzo vya maji ambako yanatiririshwa maji ambayo yana kemikali za aina mbalimbali au yenye dawa za aina mbalimbali za kilimo na mbolea? Ninaomba pia hilo nipatiwe ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kina mama ndio watumiaji wakubwa wa maji. Sote tunatumia maji, wanaume na wanawake, lakini wingi wa maji anaotumia mwanamke, hauwezi kulingana na anaotumia mwanamme. Ndoo mbili za maji kwa mwanaume, anaweza akatumia hata wiki nzima, lakini mwanamama hawezi ndoo mbili za maji kutumia wiki nzima. La kwanza, yeye mwenyewe anahitaji kupikia, anahitaji kutumia kutunza wagonjwa, anahitaji watoto wake awaogeshe kwa kutumia maji hayo hayo, anahitaji ayachemshe ili watu wanywe ndani ya familia yake.

Sasa Muswada huu sijaona mahali popote panapoonyesha au panapomlenga mwanamke kumlinda katika hilo na bado wamewekewa vizuri kwamba kuna watu ambao watakuwa wamehodhi maeneo. Ninaomba pia nipate ufafanuzi katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi, Mheshimiwa Waziri anasema zitaundwa Bodi, mimi naomba nitoe tahadhari; Bodi hizi zisilenge kuchukua wanaume peke yake. Kuna chombo ambacho kinasimamia, moja ya shughuli zake za usimamizi wa maji ni *EWURA*. Sitaki kulaumu, lakini ninachotaka kusema twendeni tukitoka hapa au wale

wanaofahamu, menejimenti yote ye *EWURA* ya wanaume watupu. Leo chombo hiki kina jukumu la kusimamia moja ya shughuli za maji.

Sasa isije ikaja ikaundwa Bodi ambayo ndani yake wanawake wakakosekana. Mwanamke ana uchungu wa kujua kuyatafuta maji, mwanamke ana uchungu wa kujua matumizi ya maji. Tunaona jinsi gani wanawake wanadhalilishwa, jinsi gani wanawake wanateseka, kuna rushwa mpaka za ngono kwenye maji. Sote tunajua! Kwenye magodauni ukienda, kwenye visima kama vina walinzi wanaume, sasa hili litafutiwe ufumbuzi na ufumbuzi wake ni katika huu Muswada ambao umeletwa mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu tunategemea kilimo cha mvua na maji yale yanaposhuka kutoka juu, Mwenyezi Mungu anapotujaalia yanapoteremka, hatuna elimu ya kutosha jinsi ya kuvuna yale maji, matokeo yake yanaingia kwenye mito, yanaishia baharini, hayo yanaondoka zake. Mashule, hawana maji, lakini kama kutawekwa utaratibu madhubuti na elimu ya kutosha ya uvunaji maji, nina hakika katika mashule, watoto wetu hawatapata taabu.

Ninazungumzia hivyo kwa sababu ninatoka kwenye Mkoa ambao tuna utajiri wa mito, tuna utajiri wa mabwawa, lakini bado utakuta wananchi wetu wanapata shida ya maji japokuwa maji ya mvua ni mengi.

Leo hii ukipiga simu Dar es salaam, watakuambia mvua inanyesha toka juzi. Ukiuliza watu wangapi wamevuna maji na lita ngapi za maji zimevunwa, hakuna hata mmoja, matokeo yake maji yale yanaleta mafuriko, yanaleta athari, yanakutana na maji taka, matokeo ya hayo maji taka ni maradhi, vipindupindu ambavyo haviishi katika baadhi ya Mikoa hasa Dar es salaam, Morogoro na kwingine. Sasa ni lini tutaweka mkakati madhubuti wa kuweza kutusaidia ili tuweze kuwa na uhakika wa uvunaji wa maji ya mvua katika maeneo yale ambayo hakuna maji ya kutosha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sitaki kupoteza muda. Haya niliyosema, nina hakika yametosha na yana msingi na yakifanyiwa kazi, nina hakika maji haya tunayosema maji ni uhai, yatakuwa kweli ni uhai kwa sababu tunahitaji maji safi na salama kwa jamii yetu. Baada ya kusema hayo, napenda niunge mkono hoja, lakini kwa roho upande kwa sababu sijaona mahali ambapo mwanamke huu Muswada utakapomlinda sawa sawa. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kuwapongeza walioleta Miswada hii. Mheshimiwa Mwenyekiti, Miswada hii imekuja, kwa kweli imechelewa. Sera ya Maji ni ya mwaka 2002, lakini sheria inayohusiana na maji hayo inakuja leo 2009 kwa maana ya *Water Resource Management Act* na *Water Supply and Sanitation Act.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanazuoni wanasema, “Kama kutatokea vita kuu ya tatu ya dunia, itasababishwa na maji.” Kwangu mimi hili ni jambo kubwa sana. Kwa hiyo, lazima tunapofanya mipango yetu namna ya kulinda rasilimali maji na namna ya kuyatumia maji haya, tufikirie *generation* inayokuja. Kwa vyovyote vile, lazima mipango

ya maji iangalie *population group* ya nchi hii kwamba baada ya miaka mitano tutakuwa Watanzania wangapi na Watanzania hao watahitaji maji kwa kiasi gani.

Baada ya miaka kumi itakuwaje? Baada ya miaka ishirini itakuwaje? Kwa kufanya hivyo, tutaweza kupanga vizuri sasa namna ya kutumia raslimali hizi za maji pamoja na namna ya kuyagawa maji yenyewe. Kwa maana hiyo, lazima tuweze ku-*integrate* hii *resource* vizuri kwa maana ya kuangalia *land use planning* ya nchi hii, kwamba unapoangalia suala la *land use planning* ujue tuna mifugo nchi hii, itapata maji wapi, tuna watu wetu, watakunywa maji wapi, tunataka kufanya kilimo cha umwagiliaji, tutafanya wapi. Yote haya ni ya msingi sana katika kulinda rasimali maji na namna ya kuyagawa maji haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nimeanza kwa kusema sheria hii ni ya msingi sana. Lakini, pamoja na uzuri wa sheria hizi mbili, kama tusipojipanga kwa kuangalia huko tunakokwenda mbele, tutakuwa na sheria nzuri, lakini bado matatizo ya maji yataendelea kuwepo. Suala la *environment* ni la msingi sana katika kulinda rasilimali maji. Mimi nafahamu tumekuwa vijijini kwetu huko, kulikuwa na mito, leo mito ile haipo. Ni kielelezo tosha kwamba huko tunakokwenda hii raslimali itakuwa ya maana sana katika maedeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe jambo moja tu, tukifanikiwa leo kama nchi, tukawapa Watanzania wote maji safi na salama, tutakuwa tumepunguza magonjwa kwa asilimia hamsini. Kwa hiyo, ina maana hata bajeti yetu ya afya itapungua kwa asilimia 50. kwa hiyo, Wizara hii ni ya msingi sana kwa maendeleo na kwa maisha ya watu wetu. Ndiyo maana nimesema sheria hizi kwa kweli zimechelewa, maana kama tulipounda Sera ile ya maji ya nchi, muda mfupi baadaye tungeunda na sheria hizi. Leo nadhani labda baadhi ya maeneo tungekuwa tumeyalinda vizuri, tungekuwa tumeishajua mipango ya maji, namna ya kulinda raslimali maji na namna ya kugawa maji yetu, lakini tumekaa miaka tisa. Ni matarajio yangu sheria hizi ambazo tunazipitisha leo au kesho, sasa nazo zitakwenda kutungwa sheria zake haraka ili tuanze kutekeleza, tuweze kulinda kizazi kijacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji ni la msingi sana na kuna mambo ambayo wengine tukijiuliza hatuelewi sana. Ukiangalia Ziwa Tanganyika, lina 1/16 ya maji yote yaliyoko duniani. Lakini, watu wanaozunguka Ziwa hilo ambalo maji yake ni safi kwa kunywa, hawana maji. Nchi hii imepata uhuru karibu miaka 48 iliyopita. Mji wa Kigoma ambao kwa kweli uko chini ya nusu kilomita kutoka kwenye Ziwa hilo, hakuna maji. Hakuna sababu zozote ambazo unaweza ukamwambia mtu akaelewa, hayupo! Lakini, mimi ukiniuliza sababu, naona ni kwa sababu ni mipango yetu tu.

Tatizo ni mipango tu! Leo tuna maji, wenzangu wamesema kuna maji ya mito yanamwagika kwenda baharini na kwenye maziwa. Mungu ametupa mito hii, lakini kwetu bado siyo ya maana. Hatufanyi kilimo cha umwagiliaji, wala watu wetu hawana maji safi na salama.  Sasa unajiuliza, inakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nasema, sheria hizi tunazoziunda leo, kama tutaishia kuunda sheria nzuri tu, tukazisifia, kama mipango yetu siyo kweli tuna nia ya kuwapa watu wetu maji safi na salama na kulinda vyanzo vya maji haya ambavyo sisi tumebarikiwa navyo, *then* sheria hii tutakuwa tumetunga kama sheria nyingine ambazo tumetunga na bado hatujaweza kuzitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *projection* za *National Planning*, lazima *component* ya maji na *budgetary* iwe ya muhimu sana. Mimi kama kuna kitu ambacho siamini na bado sijakiamini, suala la maji hatupaswi kukaa tunasubiri miapango ya *donors*. Tumekaa kila siku tunasema tunasubiri *World Bank* waje, tunasubiri *ADB* waje, tumeweka vijiji kumi, tunakaa miaka mitano, tunasubiri *donors*, hapana! Maji ni maisha ya watu, maji ni afya ya watu, ukiniambia tuanze kupanga mipango, suala la maji tulipaswa tulipe kipaumbele kweli kweli. Ukisema tuwasubiri *donors*, ni kweli tutawasubiri sana.

Sisi Kigoma pale tuna mradi wa *EU Water Facility*, tuna miradi ya Nordic, imesemwa kabla sijaingia kwenye Bunge hili mpaka leo sijaona kitu. Lakini ukijiuliza, tanahitaji shilingi ngapi kwa ajili ya mji ule? Mimi sidhani kama tunahitaji pesa nyingi sana na ambazo tungekuwa tumezipata leo, kesho kutwa, najua mwezi wa Mei tunafungua mradi wa maji wa kutoka Ziwa Victoria, kama Serikali hii isingeamua, tungekuwa tunasubiri *donors* na mradi ule usingekuwepo. Sasa kama tumeweza, kwa nini tusizalishe miradi mingi ya Ziwa Victoria katika maeneo mengine?

Maana sheria yetu hii ya *Water Supply and Sanitation*, kuna mtu alikuwa anasema Dar es salaam peke yake, *sewerage facility* ni asilimia sita ya watu wa Dar es Salaam. Jamani, kama nchi lazima sasa tubadilike namna ya kufanya mambo yetu. Hatuwezi kuendelea na *business as usual* tukadhani kwamba tunawasaidia watu wetu, hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema mwanzo wakati naanza, wenzetu kote duniani, suala la maji wamemaliza, wanalinda maji kwa maana wanahakikisha wanapata maji, ndio maana sehemu watu kama Wayahudi, hata maji yanayokwenda kwenye vyoo, wanaya-*treat*, yanarudi tena wanaya-*recycle*, yanafanya kazi. Maana yake ni nini, maana yake hii mali ni ya maana sana kwa maendeleo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna rafiki yangu ana nyumba kule Mbezi. *Mbezi water basin* iko karibu sana. Siku moja amemwalika Balozi wa Israel nyumbani kwake, wakati wanaongea, akamwambia tatizo la maji. Akamwambia sasa unayafanyaje, akasema kila baada ya wiki mbili, mwezi tunakuja kunyonya, tunalipa. Akasema *you are paying! Yes!* Hayo unayoyanyonya wanakwenda kuyauza? Akasema, hapana. Wanakwenda kumwaga, mimi nimelipa waninyonyee.

Akasema *don't do that*. Akamwelekeza namna ya ku-*treat* maji. Ukienda nyumbani kwa huyo bwana yale maji ambayo yanakwenda kwenye lile *septic tank* kubwa, ndiyo yanarudi tena, ndiyo anamwagia bustani, ukiyakuta ni maji safi, ukipewa unakunywa. Yamekuwa *treated*! Kwa wale wazee waliosoma *University of* Dar es Salaam zamani, maji yote yalikuwa yanakuwa *recycled* yanarudi, siyo! Imefanyika

*University of* Dar es Salaam wakati wa mwanzoni. Kwa hiyo, nataka kusema, pamoja na sheria nzuri, lakini lazima tuwe tayari kwa ajili ya kujifunza tuone tunawezaje kuyatumia maji vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine katika sheria hii ambalo ningependa kutoa mawazo yangu; kufufua na kujenga miundombinu ya maji ni la msingi sana hasa katika maeneo yetu. Ukiangalia kuna miji mingine inakua kwa haraka. Nilipoongelea suala la *population growth* maana yake kuna maeneo watu wameongezeka, lakini miundombinu haiko kule.

Kwa hiyo, lazima na sisi mipango yetu iwe ya kuongeza miundombinu ya maji. Lakini pia bei za maji lazima zilingane na kipato cha watu wa eneo hilo. Tukisema tunaunda bei za maji ni *flat rate* nchi nzima, kwa kweli itakuwa jambo gumu sana. Kwa hiyo, ningeomba sana bei za maji zipangwe kulingana na uchumi wa maeneo hayo, maji yatakapokuwa yanauzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nimalizie kwa kusema, sheria hizi ni nzuri sana, zimekuja kwa wakati, lakini lazima bajeti yetu sasa na nadhani ya mwaka unaokuja, ionyeshe kwamba sasa tumeanza kufikiri upya kwa ajili ya suala la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo wenzangu wamelisema, nilitaka tu kuomba, Halmashauri ipewe jukumu hilo la kusaidia kutengeneza Bodi hizi za Maji. Kazi ni kubwa sana, tukimpa Mheshimiwa Waziri na kazi hiyo, ajue hata na watu wa kule Kasulu, watu wa Kigoma ni nani nimpe kwenye hiyo kazi, ni kazi kubwa sana. Tuachie Halmashauri zifanye, lakini pia Halmashauri zikishaunda Bodi, jambo moja tu ndiyo itangaze kazi ya kutafuta Mkurugenzi Mkuu.

Kwa kufanya hivyo, atajua nimepewa kazi na watu hawa, ninatakiwa niifanye kazi hii kwa bidii. Lakini, kama akisema nimeletwa na Waziri, *CO* ameletwa na Waziri, nyie hata mkimwambia kitu, anaweza akasema hata leo nitahamishwa tu maana aliyenileta ananiamini na tumepata matatizo mengi sana kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalize kwa kuishukuru Wizara, wametupatia karibu shilingi milioni 400 kwa ajili ya kununua *pump* za Kigoma. Naomba watuongezee pesa nyingine tuongeze angalau nyingine *pump* mbili, lakini suala la miundombinu kwa ajili ya mji wa Kigoma ni la msingi sana, lakini pia Kigoma kutokuwa na maji haielezeki. Baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi jioni hii ya leo. Nami niungane na wenzangu waliotangulia, kwa niaba ya wananchi wa Hai nitoe pole kwa wote ambao wamefikwa na misiba. Niwape pole sana na nawaombea Mwenyezi Mungu awape uvumilivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miswada yote hii miwili ni muhimu mno kwa maisha ya mwanadamu yeyote. Niseme katika usimamizi wa rasilimali za maji na huduma za maji, yote kwa pamoja ni Miswada muhimu sana katika maisha yetu na hata kwa viumbe wengine. Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho nimekuwa nikijaribu kutafakari ni: Je, maji yana mbadala? Jibu litakuwa ni rahisi kwamba maji hayana mbadala na ni siri kubwa sana ya Mwenyezi Mungu na ndiyo maana maji yanakuwa ni kitu *universal*, ni kitu cha watu wote, hakuna mtu yeyote anayeweza kusema ana hati miliki ya maji kwamba mtu mwingine asije akayagusa. Hilo ni muhimu sana tulielewe hivyo kwamba maji ni haki ya kila mmoja wetu na kila kiumbe hai anastahili kuwa na hiyo haki ya kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu ambao wameshazungumzia sana kuhusu taratibu zote ambazo tumezisoma kwenye Miswada yote hii miwili. Namwomba Mheshimiwa Waziri na Naibu wake pamoja na timu nzima ya Wizara, naamini ni watu wasikivu, watajaribu kurekebisha hayo yote madogo yanayozungumziwa. Lakini kwa ujumla wake, niseme kwamba Miswada yote miwili ni muhimu nami naiunga mkono kwa sababu ya ustawi wa watu wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, kule ambako miradi mipya inatarajiwa kuanzishwa, elimu ikatolewe. Nasema hivyo kwa sababu sehemu zingine unakwenda kuanzisha miradi ya maji, wananchi hawajatayarishwa kwamba ni faida zipi watakazozipata kutokana na miradi ya maji. Kuna wenzetu wanasoma vyuo vya elimu ya jamii *(social workers)*, wale ni watu muhimu sana, hatujawatumia inavyopasa, ni watu wanaoweza kutusaidia katika *projects* nyingi sana hapa nchini kabla ya kuanzishwa na baada ya kuanzishwa kwa maana ya kufanya utayari wa wale wananchi wanaopelekewa mradi kuipokea na kuithamini ile miradi.

Kwa hiyo, naomba sana elimu ni muhimu mno kwa maana ya kwenda kuwaelimisha wale wananchi kwamba tunakusudia kuleta mradi fulani ambao utakuwa na faida zake nazo ni hizi na hizi, uendeshaji wake utakuwa huu na taratibu zitakazofuata ili wananchi waweze kumiliki ile miradi na kuweza kuitunza vizuri na iweze kuwasaidia kwa muda mrefu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba katika miradi hii ya maji ambayo tunaizungumzia kuanzisha kule Wilayani kwetu, Wizara inao watalaam, tumesikia wenzetu hapa wakisema kwenye baadhi ya Wilaya watalaam wa maji hawapo, lakini kule Wizarani natumaini watalaam wapo wengi na wengine wanaendelea ku-*graduate* kutoka kwenye vyuo vyetu. Tupatiwe watalaam kwenye Halmashauri zetu na Wilaya zetu ili kwamba waweze kusaidiana na wananchi ambao wanakuwa wanasimamia hizi Bodi za maji zitakazokuwa zinaundwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu katika Muswada huu, kuna upana unaozungumziwa, kwenye bomba kuu mita tano kila upande kwa maana ya kupata mita 10 ambako bomba linapita na kwenye bomba dogo mita mbili kila upande kwa maana utaacha mita nne. Hiyo ni sawa sawa kabisa haswa kwa yale maeneo ambayo ardhi siyo haba. Lakini kwa maeneo mengine, ardhi ni haba, ukisema tuache mita 10 kwa maana ya

mita tano kila upande wa bomba kubwa, tayari ni kilio kikubwa sana katika yale maeneo ambako tunatoka kuna uhaba wa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri kwamba katika maeneo kama hayo na ikiwezekana hata kwa mradi mzima, tuzingatie zaidi zile *classification* za mabomba tunayoyalaza ardhini kwa maana ya kusafirishia maji. Kuna classes mbalimbali, kwa mfano, *class B* ambayo ile *hardness* ya ile bomba ni ngumu zaidi na kwamba hata na kile kina cha kuchimbia kiwe kirefu zaidi. Kwa sababu, tukisema kwamba tuache mita 10 katika upande ule ambao tuna uhaba wa ardhi, kitakuwa ni kilio kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Mheshimiwa Waziri alivyoelezea, lakini kuna baadhi ya maeneo ambako kutakuwa na ugumu wake. Kwa hiyo, ningeomba kwamba kule tuzingatie zaidi aina na ubora wa zile bomba ambazo tunakwenda kuzitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bahati mbaya sana kwamba wakati mwingine hatutumii maji vizuri, mvua zinanyesha, maji yote tunayaachia yanamwagika kwenye mito yanakwenda baharini, hatuna mabwawa. Tunafahamu fika, wenzetu kule Zimbabwe wakati ule hali ikiwa nzuri, ile nchi ilikuwa imejaa mabwawa, ukipita juu ya anga ukiangalia chini ni mabwawa yamejaa na ndiyo ilikuwa inasaidia sana kilimo cha umwagiliaji. Kwa bahati mbaya Tanzania tunaachia maji yote, mvua zikinyesha yanakwenda baharini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, katika matumizi ya nyumbani *(domestic uses)* au katika sehemu zetu za *public*, unakuta maji wakati mwingine yanavuja tu, yanapotea. Kutoka kwenye *intake*, maji mengi sana njiani yanakuwa yameshapotea. Hata yanapoingia kwenye majumba basi, wakati mwingine watoto wanaweza wakasahau au watu wanaweza wakasahau, ukakuta bomba ulipofungua maji hayakuwepo, lakini ukaliacha liko wazi, maji yakija, yatachuruzika tu. Ningeomba sana sehemu za umma *(public areas)* hata kwenye mahoteli, ningeshauri sana wamiliki waweze kutumia hizi *cocks* ambazo unabonyeza, baada ya muda itajifunga yenyewe.

Mfano, hapa ndani ya Bunge letu kwenye hili jengo jipya, hii ni *modern technology* zaidi kwamba unaposogeza mikono yako, kuna *sensor* pale ita-*sense* kwamba maji yanatoka, ukitoa mikono maji yanajifunga. Lakini zipo *cocks* nyingine pia ambazo utaweza kubonyeza, baada ya muda maji yanajifunga. Nayo pia itasaidia kwamba tusiwe tunapoteza maji mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niombe kwamba kila mmoja wetu awe mlinzi wa hii miradi ya maji na niombe wananchi wote wawe walinzi wa miradi kwa sababu hii miradi ni kwa faida yetu sisi sote na kwa faida yao, kwa kila mmoja akiona kwamba kuna upotevu wa maji mahali, achukue hatua ya kujulisha mamlaka zinazohusika ili kuwapa taarifa kama watakuwa hawajafahamu ili waweze kupata taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini napata shida kidogo kwenye mambo ya *water rights*. Ningeomba Mheshimiwa Waziri anisaidie, kuna *water rights* zilitolewa enzi za

ukoloni kabla hatujapata uhuru. Wakati ule wananchi wetu walikuwa ni wachache, miaka imesogea, wananchi wameshaongezeka, lakini unakuta unaishi eneo fulani, kuna maji, mfereji unapita mbele ya nyumba yako au mbele ya shamba lako, huna mamlaka ya kuyagusa kwa sababu *Setler* aliyekuwepo siku za nyuma, ana *water right* ya huo mfereji wa yale maji kutoka kwenye chanzo chake.

Sasa sehemu nyingi migongano imeibuka, lakini tumezungumza na wale wengine wanaomiliki hayo mashamba, tumeomba, ni vizuri pamoja na kuwa na *water rights*, lakini ni muhimu kwamba waweze kushirikiana na wale wananchi nao waweze kupata yale maji. Haitakubalika mwananchi akae hapo hawezi hata kumwagilia mchicha, lakini kuna maji yanapita mbele ya nyumba yake au mbele ya shamba lake, lakini asiweze kuyagusa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru sana pia na Serikali yetu kwa uamuzi mkubwa wa busara uliotumika kuyatumia yale maji ya *Ziwa Vctoria* pamoja na ule utaratibu uliokuwepo siku za nyuma kwamba kuna mkataba. Mikataba mingine mimi nasema ni mikataba kandamizi, kwamba tunalo *Ziwa Victoria*, lakini jirani tu kuna ukame wa ajabu au mwananchi hawezi kuyatumia hayo maji. Mimi niseme kwamba hizi *water rights*, nimwombe Mheshimiwa Waziri atusaidie yawepo marekebisho ya *water rights* ili kuepuka migongano, lakini kuleta manufaa ya maji kwa wananchi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umiliki wa miradi ya maji: Hii miradi labda niwatoe hofu Waheshimiwa wenzangu wale ambao labda wanakuwa na hofu kidogo kwamba zile Bodi zitakazoundwa labda zitashindwa kuendesha. Mfano hai ni kule kwetu Mkoa wa Kilimanjaro Wilaya ya Hai na Siha, tunazo Bodi tano katika miradi mitano ya maji. Zile Bodi zinaendesha ile miradi kwa ufanisi wa hali ya juu sana, tulipata ufadhili kutoka *KFW* pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilichangia vizuri sana lakini ile miradi imekuwa endelevu kwa sababu wanaounda zile Bodi ni katika wale wale watumiaji wa maji ndiyo wanajiwekea viwango vyao wenyewe kiasi gani wachangie ile miradi ili iweze kuwa endelevu. Kwa hiyo, niseme ni kitu kizuri sana kwamba hizi Bodi ziwepo, lakini ningeomba kwamba ziweze kutambulika kisheria ili ziweze kuendelea kuhudumia wananchi kwa muda mrefu zaidi na ziweze kuwa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Muswada huu, kuna mambo ya *bylaws* kwamba Halmashauri zetu ziweze kuunda *bylaws* lakini naomba wenzetu wa TAMISEMI, katika hizi *bylaws* ambazo Halmashauri mbalimbali zinapeleka pale zifanyiwe haraka ili ziweze kurudi na kwenda kufanya kazi iliyokusudiwa. Mfano hai, kule wilayani Hai, sisi tulishapeleka *bylaws* pale TAMISEMI, lakini bado hazijarudi ili zikaweze kutumika. Kwa hiyo, naomba sana wenzetu pamoja na mambo mengine yote pamoja na hizi *bylaws* za maji ziweze kurudi kwenda kufanyiwa kazi iliyokusudiwa.

Katika uhifadhi wa mazingira ningeomba sana tukaelimisha wananchi umuhimu wa kutunza vyanzo vya maji na kwa mfano katika maeneo kule kwetu mlimani miti ya mikaratusi ilioteshwa miaka ya nyuma wakati neema ikiwa kubwa, ardhi ilikuwa tete mikaratusi ikaoteshwa ili iweze kufyonza maji ardhini. Lakini kutokana na hali ilivyobadilika sasa hivi tukaelimisha wananchi wetu umuhimu wa kuipunguza au

kuiondoa kabisa ile miti ili kwamba tuweze kuotesha miti mingine mbadala inayotunza mazingira zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisisitize upande wa adhabu zilishazungumziwa humu kwenye sheria lakini mahali pengine adhabu zile ndogo ningeomba ziwe ni kali zaidi. Wale wote wanaojaribu kuharibu vyanzo vya maji na miundombinu yake. Kwa ujumla wake ningeomba sheria ziwe kali sana ili watu wasithubutu kuchezea vyanzo maji na miundombinu yake. Naomba kila anayetumia maji ajue anawajibika kuyalipia na sio kuyalipia, niseme kwamba, anayachangia yale maji ili kwamba kesho na kesho kutwa aweze kuyapata na wanaokuja baada yetu sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiwe mchoyo wa fadhila, niishukuru Wizara kwa ujumla wake, imetusaidia, tuna mradi wa umwagiliaji katika eneo la tarambarare kule mijengweni ni banio ambalo lilikuwa limehitajika tangu mwaka 1982 baada ya kuzolewa na maji lakini Wizara sasa hivi imeshatupatia zile pesa tenda imeshatangazwa nadhani mchakato unaendelea vizuri, kwa hiyo, niishukuru sana Wizara kwamba lile banio likishapatikana ni ukombozi mkubwa sana kwa wale ndugu zetu wanaoishi maeneo ya tambarare kule Wilayani Hai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana kwa nafasi hii. Napenda kuwashukuru sana wananchi wa Wilaya ya Hai na Siha kwa ujumla wao, kwani ile miradi ya maji wanaendelea kuitunza vizuri na niwaombe sana waendelee kuitunza kwani ndiyo ukombozi wa maisha. Mfano hai kabisa ni mji wetu wa Boma Ng’ombe ambao ni mji mdogo mchanga umestawi kwa haraka sana baada ya upatikanaji wa maji safi na salama. Lakini naomba wananchi waendelee kuitunza ile miradi ili kwamba iwe endelevu zaidi. Nazidi kuomba miradi hii ya maji pale ambapo tunapata wafadhili tukae tukijaanda kujua kwamba huyu mfadhili hataweza kukaa milele, ndiyo maana zile Bodi ziweze kukaa na kujipangia kiasi cha malipo ambacho wananchi wataweza kuyamudu kuyalipa lakini kwa maana ya kufanya ile miradi iwe endelevu. Naomba wananchi waelewe kwamba sio kwamba wanalipia maji, bali wanachangia tu ile huduma ili iweze kuwa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi hii uliyonipatia jioni hii ya leo nilikuwa na hayo machache ya kuyaongelea lakini nizidi kuishukuru Wizara kwa kazi kubwa na nzuri inayofanya lakini niwape moyo wale wanaona kwamba tumeshinikizwa kwa sababu ya kuleta Miswada tuendelee kuacha hivyo hivyo ili Miswada muhimu kwa ajili ya ustawi wa Taifa letu na kwa nchi yetu ya Tanzania nizidi kukushukuru sana. Ahsante kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kimbita. Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji waliobaki wako kama kumi hivi, lakini muda tulionao hamruhusu hata mtu mmoja kuendelea kuchangia. Kwa hiyo, nachukua nafasi kukushukuruni sana kuchangia huu Muswada. Lakini mimi sitamtaja hata mmoja ili kumpa nafasi Mheshimiwa Spika kesho au yeyote atakayekuwa kwenye Kiti ili waweze kujua namna gani tunaweza kumalizia na uchangiaji wa Muswada huu unaoendelea.

Kwa hayo machache, napenda kuchukua nafasi hii kuahirisha kikao hiki mpaka kesho tarehe 28 Aprili, saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.33 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 28 Aprili, 2009 Saa Tatu Asubuhi)*